ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi – Tarehe 16 Aprili, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Mwenyekiti, (Mhe. Mgeni Hassan Juma) Alisoma Dua.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: (Kny: Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2011/2012. . Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 92

Utumiaji wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 94

Uendelezaji wa Dhana ya Utalii kwa wote

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: (Kny: Mhe. Fatma Mbarouk Said): Aliuliza:-

Katika kuendeleza dhana ya utalii kwa wote kimatendo kuna mpango gani wa kuhakikisha wana vijiji wananufaika na utalii kwa upande wa ajira na miradi ya kimaendeleo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 94 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, dhana ya utalii kwa wote ina lengo la kumshirikisha kila mwananchi katika kuendeleza na kulinda utalii, ili na yeye afaidike nao. Sheria nambari 7 ya mwaka 2012 imeanzisha Kamati za Utalii za Wilaya zikiwa na wajibu wa kuendeleza utalii katika ngazi za wilaya na kuhakikisha kwamba maendeleo ya utalii yanakwenda sambamba na mahitaji ya jamii na kuwanufaisha watu wote.

Mhe. Mwenyekiti, kuwepo kwa kamati hizi ambazo tayari zote tumeshaziteua na nyengine tumeshaanza kuzizindua, kutahakikisha kuwa wana vijiji wananufaika na utalii kwa kupata ajira, kuanzisha miradi itakayosaidia kuleta maendeleo ya utalii. Kwa kuwa kamati zimepewa uwezo kisheria wa kuandaa mipango ya maendeleo, katika wilaya zao na vijiji vyao ambayo itasaidia jamii husika pamoja na sekta ya utalii. Ni imani yangu kwamba kamati hizi zitatekeleza majukumu yao kwa ufanisi ili wananchi waweze kufaidika ipasavyo na utalii.

Wizara yangu kwa kupitia Kamisheni ya Utalii itashirikiana na kamati hizo, katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, katika jibu lake la msingi Mhe. Waziri alitaja uzinduzi wa kamati za utalii za wilaya. Je, Wajumbe wa kamati za utalii za wilaya ni nani na wanapatikanaje na kwa Wilaya ya Micheweni uzinduzi utafanyika lini.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wa kamati za utalii za wilaya wanapatikana kwa kuteuliwa na Waziri anayeshughulikia utalii, kwa mashauriano na Mkuu wa Wilaya husika.

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wa kamati za utalii za wilaya kwanza ni Mkuu wa Wilaya mwenyewe kama Mwenyekiti, Afisa Utalii wa Wilaya ni Katibu. Wengine ni Kamanda wa Polisi wa Wilaya, Mwenyekiti wa Masheha katika Wilaya. Wengine ni Afisa wa Mazingira katika wilaya, mwengine ni Afisa anayeshughulikia Utamaduni katika Wilaya. Pia yumo Afisa anayeshughulikia Makumbusho na Mambo ya Kale katika Wilaya. Lakini yumo pia mkulima mmoja ndani ya Wilaya. Vile vile yumo Afisa mmoja kutoka NGO ndani ya Wilaya na pia yumo mfanyabiashara mmoja wa utalii katika wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, katika Wilaya ya Micheweni tukijaaliwa uzinduzi utafanyika, kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kunipatia nafasi hii kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Waziri kwanza nikupongeze kwa nia njema ya kuanzisha hizi kamati za utalii za wilaya kwenye vijiji, katika kusaidia suala zima la utalii. Lakini kila panapo zuri basi na baya halikosi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri kuna baadhi ya wawekezaji wameanza kuleta matatizo kwa wana vijiji kwa kuziba njia za asili, ili kuweza kukaa katika maeneo yao ya fukwe kwa mahitaji mengine. Kadhia hii sasa imejitokeza Paje kwa mwekezaji Crystal.

Je, Mhe. Waziri wizara yako ina taarifa ya kuzibwa kwa njia hizi za kuendea fukwe na kama ina taarifa hizi imechukua hatua gani, ili kuwaondoshea wana vijiji kadhia hii.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na matatizo mengi katika sekta ya utalii hivi sasa na ndio maana ili kuyaondoa matatizo hayo, tukaunda kamati hizi za utalii za wilaya ambazo zenyewe ndio zitakuwa na jukumu la kuangalia matatizo yote ya utalii yaliomo katika wilaya, kwa kushirikiana na Kamisheni basi tumepata ufumbuzi.

Kwa hivyo, yale yalioko Paje tunaelewa, yalioko Nungwi tunaelewa, yalioko Jambiani tunaelewa. Lakini kwa sababu kamati za utalii za wilaya za kisiwa cha Unguja, tukijaaliwa ikifika Ijumaa zitakuwa zote zimezinduliwa na zimepewa majukumu yake kisheria. Nina imani kwamba matatizo yote yalioko katika vijiji kwenye kisiwa cha Unguja yataanza kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria. Kwa yale yalioko Pemba basi kama nilivyosema kwamba wiki moja inayofuata nazo zitazinduliwa na kwa hivyo matatizo yote yalioko katika vijiji katika kisiwa cha Pemba nayo yatakuwa yamepata ufumbuzi, kwa sababu kamati hizi zina nguvu za kisheria.

Nam. 67

Motisha kwa Wafanyakazi wa Kitengo cha Afya ya Uzazi

Mhe. Asha Abdu Haji – Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara ya Afya kwa kuona umuhimu wa kutoa motisha kwa wafanyakazi wake wa kitengo cha uzazi ni moja ya maeneo hayo, Wizara kutoa motisha (Bahashishi) kwa wakunga wanaobahatika kupokea watoto wa kiume kwa wajawazito wanaoshughulikia wakati wa kujifungua. Hapa natoa pongezi kwa hili, kinyume chake kwa wakunga wanaopokea watoto wa kike wao huwa hawapati motisha yoyote.

(a) Je, kuna sababu gani za msingi zinazopelekea wengine kupewa motisha na wengine kunyimwa motisha.

(b) Kwa kufanya hivi hatuoni kuwa tunafanya ubaguzi kwa wafanyakazi wetu.

(c) Kwa kuwa suala la uzazi ni elimu na matakwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kwa kuwa wanawake na wanaume wote ni binadamu na umuhimu wao katika dunia hii unategemeana, Je, kwa nini tunaonesha dalili za kuidhalilisha jinsia moja na kuitukuza jinsia nyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 67 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika utaratibu wa Wizara ya Afya suala la kuzalisha ni moja ya kazi zenyewe kwa wafanyakazi na ndicho wanacholipiwa, wala hakuna motisha inayotolewa kwa kuzalisha mtoto wa jinsia yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli ili huduma za mama na mtoto ziimarike, kila wilaya zinatumia mbinu zake tofauti kwa mapendekezo yao, ili kuongeza idadi ya kina mama wanaozalia hospitali kwa wakunga wenye ujuzi. Hayo yanayofanyika hayachagui jinsia ya mtoto anayezaliwa, kama ni motisha wazazi wote wanapewa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa karne hii ya leo ya 21 tuliyonayo, kama kutakuwa kuna jambo kama hili linatokea, basi anaefanya hivyo atakuwa anavunja haki za binadamu na kuwadhalilisha wanawake kijinsia.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Bwejuu wanajenga kituo cha kuzalishia kwa ukanda wa pwani. Je, kituo hiki kitafunguliwa lini?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli anayosema Mhe. Asha Abdu, kituo Bwejuu kimejengwa na karibu kinamalizika, yamebakia mambo madogo madogo tu. Ili kituo kiweze kukamilika na kufunguliwa kinahitaji wafanyakazi. Nilichokisikia ni kwamba aliyekijenga na aliyewasaidia atatia vifaa vya kazi. Itabidi kwanza tukahakikishe kwamba vifaa vyote vinavyohitajika vipo, baada ya hapo tutakapopata mgao wa wafanyakazi wapya tutahakikisha na kituo hicho tunakifungua rasmi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Mhe. Mwenyekiti, katika jibu lake Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba ni kweli kuwa hakuna hiyo motisha ya kumpa mfanyakazi katika hao wanaozalisha bali wanatumia mshahara tu.

Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kuwa iko haja, kwa kuwa hawa kinamama wanaowazalisha mama wenzao wanafanya kazi nzito ukawaongezea mishahara. Isitoshe, je huoni iko haja sasa Wizara yako wakapewa *risk allowance.*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mishahara ya wafanyakazi inatolewa kwa kiwango cha elimu yao. Kwa hivyo, kama ni kuongezwa waongezwe serikali nzima, na watu wote ambao wanapewa kwa *diploma level* ambao wafanyakazi hawa wanaofanya pamoja na cheti. Kwa hivyo, hatuwezi tukasema kwamba sisi Wizara ya Afya tuwaongezee mshahara wao.

Mhe. Mwenyekiti, Mkunga na Msaidizi Mkunga kazi yao ni kuzalisha, hiyo ndio kazi yao kubwa. Sasa kama kuzalisha kwao ndio itakuwa kazi kubwa, sijui kazi ndogo itakuwa ipi.

Mhe. Mwenyekiti suala la *allowance* inategemea na sio *allowance*, kwa sababu *nurse* kwa utaratibu wanakwenda kwa *shift* asubuhi, mchana na usiku. Hiyo ni sehemu yao ya kazi na hivyo ndivyo walivyo. Tutakachokipendekeza au kama tunaweza kuwasaidia, tumesema hivi, katika mipango ijayo yule atakayezalisha usiku au akazalisha siku sio kazi yake, lakini mwengine hayupo akamsaidia, basi wajiorodheshe tuwajue ili angalau wale kwa sababu wamefanya kazi ambayo iko nje ya utaratibu wao tuweze kuwasaidia. Huo ndio utaratibu ambao tunaweza tukaufanya.

Nam. 79

Marekebisho ya Mishahara ya Walimu

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mara kadhaa imeahidi kuwafanyia marekebisho ya mishahara yao wale walimu waliomaliza mafunzo ya *Teachers Advanced Programme* (*TAP*), jambo ambalo halijafanyika hadi leo hii. Kwa kuwa kuna taarifa kuwa walimu waliotoa mafunzo hayo waliahidiwa kulipwa nauli zao pamoja na maposho mengine, lakini na wao hawajalipwa hadi hii leo.

(a) Je, suala hili ni kweli?
(b) Kama ni kweli Wizara itaondosha lini aibu hii kwa kuwapa haki zao wale wote wanaostahiki kulipwa?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 79 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa majibu mafupi kabla sijajibu swali. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, mara kadhaa imeahidi kuwafanyia marekebisho ya mishahara yao walimu waliomaliza mafunzo ya *Teachers Advanced Programme (TAP)*, jambo ambalo halijafanyika hadi hii leo na kwa kuwa nina taarifa kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliahidi kufanya hivyo.

(a) Je, suala hili ni kweli haijafanywa marekebisho. Mhe. Mwenyekiti, marekebisho ya mishahara ya walimu hawa wapatao 50 yamefanywa na yameshapelekwa Tume ya Utumishi, kinachosubiriwa ni amri ya Tume ya Utumishi kutoa kibali ni kwamba marekebisho haya sasa yatekelezwe.

    Mhe. Mwenyekiti, nina barua hapa tuliyomuandikia Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Barua hii ni ya tarehe 24/09/2012. Barua hii imeeleza kila kitu, orodha ya majina ya wanafunzi waliosoma Michakaeni, orodha ya majina ya wanafunzi waliosomea Kiembesamaki na orodha ya majina ya wanafunzi waliosomea Dunga. Majina yao, vyeti vyao walivyopasi na mapendekezo ya nyongeza ya mishahara yao, kila kitu kiko *black and white*.

Kwa bahati mbaya sana mpaka hivi nakuja mitamboni bado sijapata kibali cha kuwalipa hawa walimu wangu.

(b) Wizara yangu imekwishawasilisha mapendekezo na tunasubiri kupata kibali cha Wizara hiyo ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili tukamilishe kuwalipa wafanyakazi wetu hawa walimu wa *(TAP).* Ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi zake na umakini wake katika kuwatumikia wananchi, katika misingi ya kuwatetea haki zao na kuwatafutia haki zao anaowatumikia. Kwa hivyo, anaonesha utumishi ulio makini, mahiri na wa uadilifu sana. Kwa hili napenda nimpongeze Mhe. Waziri mzee wangu pale.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, walimu hawa ni karibu mwaka wa tano wamemaliza hii kozi yao *(TAP),* na kwa kuwa Mhe. Waziri tayari amechukua bidii kubwa ya kupeleka majina haya katika Tume ya utumishi serikalini ambayo hadi leo hii ndani ya miaka yote mitano tangu wamalize kozi yao walimu hawa wa *(TAP)* na ambapo walimu hawa ni wa sayansi. Kuna tatizo kubwa la walimu wa sayansi, hawa wamewapa mafunzo na tayari wamemaliza mafunzo ya sayansi na wanasomesha vizuri katika skuli zetu za sekondari hapa Zanzibar kwa Unguja na Pemba, hadi leo hii Tume ya Utumishi Serikalini pamoja na kupelekewa majina ya walimu wetu hawa, bado hawajawalipa mafao yao. Swali.

(a) Je, kwa kufanya hivyo Mhe. Mwenyekiti, si kuwarudisha nyuma walimu hawa na kuwavunja moyo.
(b) Kama walimu hawa wataamua kuacha kazi na kwenda kutumikia skuli za binafsi ili kufuata maslahi, si itakuwa tumepoteza sana Zanzibar kwa upande wa serikali

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia wale wakufunzi waliowafundisha walimu hawa wa *(TAP),* wana madai na wao kwamba katika kazi yao ya kufundisha hawa walimu, walikuwa wapewe nauli na baadhi ya madukhuli na walimu hawa wananung'unika hadi leo hii kwamba wamemaliza kozi ya kuwafundisha hawa walimu na hadi leo hii hawajapewa madukhuli yao. Kwa kuwa

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, uliza swali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Je, kwa kuendelea kuwanyima hawa wakufunzi madukhuli yao baada ya kumaliza kazi, si kuwanyima haki yao ya msingi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napokea pongezi zake alizonitolea na hii ndio kazi ya Wizara yangu, inajitahidi sana kutekeleza yale tunayoagizwa na Baraza lako tukufu ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu wa kawaida na walimu tunawatengenezea haki zao ili wawe wafanyakazi wazuri.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe aliuliza kama kutowatekelezea haki zao kwa muda huu wa miezi iliyopita mitano si kuwavunja moyo. Jibu ni kwamba nimekusikia. Mhe.

Mjumbe umekuwa ukiliuliza swali hili mara kwa mara, kutokana na uchungu unaowaonea hawa walimu wetu. Sisi Wizarani tunakupongeza sana na nataka nikupe ahadi hii ni ya mwisho, kwamba tukimaliza kujibu haya maswali tu basi tunakwenda tena Tume ya Utumishi Serikalini, kupeleka tena orodha yetu hii na nakala ya barua tutakayoipeleka tutakuletea wewe kama ni Mwakilishi wao, ili hatimaye na wewe unisaidie kuifuatilia Tume ya Utumishi ombi letu hili.

(b) Linalinganana lile la mwanzo kwamba tunawavunja moyo hawa kwa kutowalipa haki zao kwa muda mrefu. Kama nilivyojibu nakubaliana na wewe sina namna ya kufanya, ila sasa nakuahidi tena kuwa nitalifuatilia kwa karibu zaidi na barua nitakayoipeleka nitakuletea nakala ili na wewe unisaidie kulifuatilia. Ahsante sana.

Nam. 99

Ada za Malipo katika Skuli za Binafsi

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko ya Wizara juu ya ada kubwa zinazotolewa na skuli binafsi, ambazo zinapishana sana kati ya skuli moja hadi nyengine, hali ambayo ilipelekea serikali kutoa ahadi kuzifuatilia ada hizo na baadae kutoa muongozo wa kiwango cha ada kitakachoruhusiwa.

(a) Ni hatua gani zilizochukuliwa na serikali katika kupunguza ada hizo.
(b) Ni vigezo vipi vinavyozingatiwa katika upangaji wa ada hizo.
(c) Je, kuna chombo chochote cha kupanga ada hizo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 99 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi anauliza ni hatua gani serikali imechukua katika kuondosha tatizo la upungufu wa ada.

(a) Mhe. Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na serikali ni zile zile kama nilivyosema katika kujibu swali la msingi lililopita, kwamba tumeshawasiliana na Tume ya Utumishi kuhakikisha mambo yetu haya yamewekwa sana, muda sio mrefu mambo yatakuwa mazuri.

(b) Kama nilivyotangulia katika maelezo yangu, vigezo vinavyotumika katika kupanga viwango vya ada katika skuli binafsi ni sifa ya skuli, huduma zinazotolewa skuli, viwango vya elimu vinavyotolewa na kadhalika. Mhe. Mwenyekiti, hizi ni skuli binafsi na sisi tumekuwa tukizipitia mara kwa mara kuhakikisha hizi huduma zilizotajwa zinatekelezwa ipasavyo. Kwa mfano, kuna skuli za binafsi zinazotoa huduma ya chakula, mavazi, vitabu, masomo mazuri sana na kadhalika. Kwa hivyo, wizara baada ya kuona

huduma hizo zinatolewa na sifa za elimu inayopatikana ni nzuri, basi wizara inaridhika kabisa na ada zinazotozwa na skuli hizo.

Hakuna chombo maalum kilichoundwa na wizara yangu kusimamia ada za skuli, bali Baraza letu la elimu ndilo linalofuatilia kuhakikisha ada zinazotozwa zinalingana na huduma za elimu zinazotolewa na ile skuli binafsi. Lakini wizara haina mamlaka ya kuwalazimisha tozeni ada kadhaa na msitoze ada kadhaa. haina mamlaka ya kuwalazimisha tozeni ada kadha na msitoze ada kadha, hiyo ni juu ya wanafunzi na wazee. Kutokana na huduma inayotolewa na skuli na kutokana na uwezo wao wazee wanachagua ni skuli ipi waende na hata skuli za serikali wengi wao wanakuja kwa sababu kule hakuna ada, ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika hapa kwa mintarafu ya kupanga mambo yetu ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri Mhe. Waziri kwa kuwa Wizara inasema haina mamlaka ya kuingilia upangaji wa ada. Vile vile kwa kuwa anasema wizara yake ina watu maalum ambao wanapitia.

(a) Je, Mhe. Waziri haoni kwamba lazima kuwe na chombo ambacho kinasimamia na kuzingatia ada za Skuli Binafsi.

(b) Haoni kwamba kuna watu wengine ambao hawawezi kulipia ambapo kama ada zinawekwa za aina mbali mbali na wakati mwengine uzoreteshaji wa skuli hizo. Hali hii si kuwanyima baadhi ya wananchi kuweza kusomesha watoto wao katika Skuli za Binafsi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nimesema hatuna chombo maalum cha kufuatilia kima cha ada skuli zinazolipa, na nikasema Baraza la Elimu ndilo lenye mamlaka ya kuzikagua hizi skuli, kuhakikisha kwamba ada wanazozitoza zinalingana na huduma walizoahidi kuzitoa. Sasa kama tunapogundua kwamba skuli ile huduma zake ni dhaifu sana kulinganisha na ada inazotoza basi skuli ile tunayo mamlaka hata kuifungia leseni isi-*operate*.

Mhe. Mwenyekiti, pili sioni kuwa ninawadhulumu wale ambao hawana uwezo wa kulipa ada kubwa zinazotozwa na Skuli za *Private*. Mhe. Mwenyekiti, jibu langu ni kwamba sioni kwamba ninawadhulumu na wala sioni kwamba hiyo ni dhima ya wizara yangu kuhakikisha kwamba nani mwenye uwezo wa kulipa ada ya skuli ya *private* na nani hana uwezo wa kulipia ada kubwa.

Kwa kweli dhima ya Wizara yangu ni kuhakikisha wale wanyonge wasiokuwa na uwezo wa kulipia skuli za *private* nafasi zipo za kutosha katika skuli za serikali na hiyo ndio kazi ambayo ninayoifanya kwa nguvu zangu zote. Sasa mwenye kutaka kwenda *private* anakwenda ni *choice* yake mwenyewe, lakini kama hana uwezo anakuja serikalini na tunampokea.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, sikuridhika hata kidogo na majibu ya Mhe. Waziri, kwa sababu nimeuliza maswali yangu anijibu kwa mujibu nilivyomuuliza na hili la pili

ameligeuza *vice versa*. Kwa hivyo, naomba majibu ambayo nimemuuliza swali langu Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha Bakari Makame, naomba kama swali langu hujajibiwa vizuri basi ulirudie, ili Mhe. Waziri afahamu na akujibu vizuri.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyoelewa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndio wizara baba au mama kwa Sera ya Wizara ya Elimu. Vile vile tunaelewa kwamba skuli za binafsi ni wao ndio wanatakiwa waangalie skuli binafsi zinakwenda vipi, na nimesema kwamba kwa kuwa wapo watu ambao wanataka kupeleka watoto wao skuli za binafsi na tunajua kwamba skuli za serikali zipo.

Je, haoni kwamba wale wanaotaka na wao kujaribu kusomesha watoto skuli za binafsi hawana uwezo kwa sababu Wizara hii haina chombo maalum cha ukaguzi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, sioni tofauti ya jibu nililolitoa na hili swali ambalo nimeulizwa sasa.

Mhe. Mwakilishi amesema hivi Wizara ya Elimu ndio wizara baba na mama katika kusimamia shughuli za elimu nakubali kwa asilimia mia moja. Vile vile nakubali kwamba Wizara ya Elimu imetengeneza sera, kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi au mtoto ambaye amefika umri wa kujiandikisha kwenda skuli anajiandikisha na anachukuliwa skuli.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba chombo cha Ukaguzi kipo na hichi sio chombo cha kuweka kiwango cha malipo ya skuli za *private* hapana. Kwa kweli chombo hichi kinakagua malipo au ada wanazozitoza skuli za *private* zinalingana na zile huduma ambazo wameahidi ambazo watazitoa na ziko skuli nyingi zenye kutoza ada kubwa na wanatoa huduma nzuri na wananchi wanataka kuwapeleka watoto wao skuli zile wanawapeleka na wanapokelewa.

Sasa suala la kwamba mtoto anao uwezo au hana, basi turudi kule katika Sera ya Serikali kwamba aliyekuwa hana uwezo halazimishwi kwenda kusoma mtoto wake *private schools* hapana, kwa sababu *private schools* zimewekwa kwa ajili ya wanafunzi au wazee wenye uwezo wa kulipia zile ada zilizowekwa na *private schools*. Skuli zetu za *government* bado zipo na nafasi ya kusoma ipo na kila mwanafunzi ambaye amefika umri wa kusoma basi tunamchukua kwa mujibu wa sera yetu.

Nam. 28

Sababu za Kupasishwa Magari kila Mwaka

Mhe. Mussa Ali Hassan – Aliuliza:-

Kila mwaka nchi yetu imekuwa na utaratibu wa kupasisha vyombo vya moto vya usafiri kama gari, pikipiki na kadhalika.

Je, ni sababu gani tatu (3) za msingi zinazopelekea vyombo vya usafiri kama magari kupasishwa kila mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 28 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kila mwaka nchi yetu imekuwa na utaratibu wa kupasisha vyombo vya moto kwa sababu kuu tatu zifuatazo:-

(a) Jambo kubwa na la msingi ni usimamizi na utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Usafiri Barabarani Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003.

(b) Kuangalia uzima wa chombo kama kinafaa kutembea barabarani bila ya kusababisha hatari. Vile vile kuangalia mazingira ya chombo kama yanaendana na matakwa ya sheria kwa kukinga wanaotumia chombo hicho na watumiaji wa barabara ikiwa pamoja na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira.

(c) Kuhakikisha usalama wa chombo kwa watumiaji wote pamoja na utunzaji wa barabara husika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Je, haihusiki katika malipo yetu ya vyombo kama tunatoa nyongeza ya kuweza kutengenezewa barabara zetu, ili vyombo vile vipite kwa usalama. Sasa kama ndivyo hivyo, kwa nini kuna baadhi ya barabara hivi sasa vyombo vyetu havifiki kwenye vijiji kwa ajili ya kuhudumia wananchi yaani magari yamesitisha na wakati tunalipa kila mwaka kwa ajili ya gari kufika huko na kuweza kuhudumia wananchi, ili wapate usafiri na kufikisha vitu vyao katika masoko. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, sikumuelewa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mussa Ali Hassan, rudia swali lako.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Ninavyoelewa zaidi ni kwamba tunalipa kuhusiana na kupasisha vyombo vya moto, kwa sababu vyombo vile vipate uhakika wa barabara zetu zinazopita vyombo vile ni nzuri. Lakini utaona kuna baadhi ya vijiji hivi sasa magari yamekatisha kabisa kufika huko vijijini au vyombo vyetu vya moto vidogo vidogo kwa sababu ya ubovu mkubwa wa barabara.

Je, tuna sababu gani ya kwamba hatutengenezewi barabara sehemu za vijijini, ili vyombo vyetu kufika kwa usalama au magari ya daladala kukatisha kabisa kwenda kuhudumia wananchi katika sehemu hizo wakati vyombo vyetu tunalipa kisheria.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, suala la ukaguzi na suala la malipo ni suala linalotokana na kukipasisha chombo ili kiweze kukidhi matakwa ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003. Hivyo suala la kukikagua, kulipishwa halihusiani na suala la barabara. Tunamhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kama kuna gari ambazo hazifiki katika kutoa huduma kwa sababu ya barabara hili atuletee tutakaa kama serikali tuna wajibu wa kuwasaidia wananchi wetu.

Ninachotaka Mhe. Mwakilishi yeye kama kiongozi aendelee kushirikiana na serikali pamoja na halmashauri husika ili tukatengeneze barabara hizo ili hayo magari yanayotaka kwenda vijijini kutoa huduma yaweze kufanya hivyo ili kunusuru changamoto wanazozipata wananchi wetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Lakini kama alivyosema kwamba Mhe. Naibu Waziri wale waliompendekeza kuwa miongoni mwa maimamu wa Msikiti wa Baraza la Wawakilishi kwa kweli hawakukosea, yaani walimpendekeza kuwa imamu kwa sababu ana majibu mazuri tena yuko makini.

Ni gari ngapi ambazo zimepasishwa kwa mwaka 2012/2013 na ngapi ambazo zinatembea bila ya kupasishwa kwa mwaka huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa utaratibu na sheria yetu husika gari zote zilizopo Zanzibar katika mwaka huu zinalazimika kupasishwa, ili ziweze kutumia barabara. Kwa kutambua kuwa suala lenyewe hili linahusu mambo ya takwimu, basi namuomba Mhe. Mwakilishi anikubalie nilichukue na nitamletea majibu.

Lakini jambo ambalo ninaloweza kumthibitishia kwamba hakuna gari ambayo itakuwa inatembea bila ya kupasishwa na kama kutakuwa na gari ambayo itakuwa inatembea bila ya kupasishwa, basi gari hiyo itakuwa inakwenda kinyume na utaratibu na sheria na tutalazimika kuikamata na kumtoza faini kwa mujibu wa taratibu na sheria zetu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa gharama za uipasishaji sasa ni kubwa mno kwa gari za mizigo na hata zile za abiria. Kwa kuwa gari za abiria hususan katika maeneo ya vijijini zinafanya kazi kwa zamu, yaani zinafanya kazi siku 15 tu katika mwezi. Vile vile gari hizo siku nyengine zinakuwa zinabaki kwa ajili ya matengenezo na marekebisho mengine.

Je, ni lini wizara yako itapunguza gharama hizi kwa gari za abiria ambazo huwa hazifanyi kazi mwezi mzima, isipokuwa huwa zinafanya kazi siku 15 katika mwezi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, sababu ya gari za abiria na mizigo kutozwa tozo hizi ni kwa sababu gari hizi ni gari za biashara, na kama Mhe. Mwakilishi maelezo yake aliyoyatoa kwamba gari hizi zimekuwa nyingi kiasi ya kwamba zinapelekea wao wenyewe kupanga zamu. Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini wingi huu pengine umechangiwa na tozo zetu kwamba ziko chini.

Lakini matarajio yangu ni kwamba suala hili la gharama tutakaa na kuliangalia na wala hatujaona sababu yoyote ya msingi ya kusema gharama hizi ni kubwa na kusema tuzipunguze, isipokuwa tunachoweza kukifanya ni kuziongeza gharama hizi kwa kutambua tu kwamba huduma hizi zinahitajika na hawa ni wafanyabiashara watalazimaka kulipa kodi kwa utaratibu huu wa kulipia magari kama wanavyolipa kodi wanyabiashara wengine katika sehemu zao. *(Makofi)*

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Wizara ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2011/2012

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, jana tulifikia michango ya Waheshimiwa Wajumbe 6 na hapa tunao Wajumbe wengine 12. Sasa kwanza ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe, kwamba yule ambaye ameleta jina lake basi atulie na pale ambapo jina lake litatajwa awepo hapa kwa ajili ya kuchangia. *(Makofi)*

Vile vile tulikubaliana tangu awali kwa utaratibu ambao tulioupanga wenyewe na tulioukubali tutakuwa tunatumia dakika 20. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba twende kwa muda huo kwenye *points* na pia tusirudie, ahsante. *(Makofi)*

Tunaendelea na mchangiaji wa kwanza atakuwa Mhe. Saleh Nassor Juma na baada ya hapo atafuatia Mhe. Ashura Sharif Ali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa siku ya leo.

Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na hatimaye kutupa afya na uwezo wa kutoka katika nyumba zetu hadi humu katika Baraza hili la kutunga sheria, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu napenda nitumie fursa hii Mhe. Mwenyekiti kukushukuru wewe kwa kuweza kunipatia nafasi, vile vile kuwapongeza mawaziri wetu watatu hawa ambao wamewasilisha taarifa zao za utekelezaji ndani ya Baraza hili. Kwa kweli taarifa zao ambazo wameziwasilisha ni nzuri sana. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi tumefurahishwa sana na uwasilishaji wao.

Kwa kweli nilikuwa na wasi wasi sana katika hawa mawaziri mmoja ni mwanamke, lakini kweli ameweza kuwasilisha vizuri kama wenzake hawa wanaume, ama kweli Mhe. Mwenyekiti wanawake mlikuwa na dhana kwamba wakiwezeshwa wanaweza.

Lakini kumbe bila ya kuwezeshwa, yaani Mhe. Mwenyekiti wanawake wanaweza bila ya kuwezeshwa kama mama yangu pale Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ameweza mtu mwenye umri wa miaka 65 je vijana wadogo hapa akina Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Shadya Moh'd Suleiman si wanaweza zaidi, kwa hiyo nawapongezeni sana. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, mafupi sasa nianze na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Naomba nianze na suala zima la majengo hususan yale ya skuli na vyuo vyetu. Mhe. Mwenyekiti, majengo ya skuli na ofisi za Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni mali za serikali na sisi kama Wawakilishi wa wananchi kazi zetu kubwa sio kupitisha mafao ya watendaji hapa, lakini ni pamoja na kuangalia matumizi mazuri ya *public assets* pamoja na fedha za walipa kodi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa huzuni kubwa sana inasikitisha kwamba majengo yetu mengi na skuli zetu pamoja na vyuo zina matatizo sana, kwa sababu ardhi yake hivi sasa imevamiwa na wafanyabiashara pamoja na wananchi na hii ni kutokana na sababu mbili kubwa. Sababu ya kwanza Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba majengo yetu ya skuli, ofisi pamoja na vyuo zimekosa hati miliki pamoja na uzio unaozunguka majengo hayo. Kwa kweli hali hii inatoa nafasi kubwa sana kwa wananchi kuvamia maeneo yale kwa ajili ya makaazi pamoja na biashara.

Kwa mfano, hapa juzi wakati Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati alisema kwamba tatizo la kwamba maji yanapungua ni kwa sababu nchi imezidiwa, kwa hiyo tulikuwa tukitumia lita kidogo, lakini hivi sasa watu ni wengi na maji yamekua kidogo kwa sababu tunatumia lita nyingi na sasa wanataka kuangalia *alternative* nyengine badala ya kutumia maji ya ardhi pengine twende kwenye bahari na tuyafanyie *desalination* maji yale.

Sasa ikiwa maji tumeyazidi kwa hiyo na ardhi itakuwa tumeizidi mno. Kwa hivyo, watu badala ya kupata viwanja vyao vya kawaida wanakimbilia katika maeneo ya skuli zetu kuanza kuishi pamoja na kufanya biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kulinusuru hili. Kwa mfano, hivi sasa tukiangalia kwenye Chuo chetu cha Kiislamu pale Mazizini pamoja na Chuo cha Kiislamu kilichoko Micheweni ardhi imevamiwa sana, jambo ambalo *public assets* zinaharibiwa kwani mifugo inaingia mule na watu wanavamia, yaani Chuo cha Kiislamu ardhi yake imevamiwa mpaka kujengwa baadhi ya maeneo ya biashara mule, kwa sababu haina uzio pamoja na hati miliki.

Kwa hivyo, mimi naomba tu pamoja na jitihada kubwa za Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na watendaji wake, lakini suala zima la uzio lazima awezeshwe. Mhe. Mwenyekiti, nadhani katika hili lazima Baraza lako Mhe. Mwenyekiti Baraza lako liwe makini, yaani pale ambapo hawa wenzetu katika bajeti zao wataleta mambo kama haya, basi ni vyema tuangalie kwa vizuri, ili tuweze kuwawezesha kujenga uzio kwa ajili ya kunusuru hii ardhi kuvamiwa na hiyo ni kazi yetu sisi. *(Makofi)*

Lakini kuna kazi ambayo ni rahisi na wala haihitaji gharama Mhe. Mwenyekiti, kazi ya kupata hati miliki, yaani gharama yake ni ndogo na kuna baadhi ya skuli na vyuo tayari wameshalipa. Kwa kweli nashangaa sana kuona kwamba hawa hawapatiwi hati miliki na taasisi inayohusika.

Kwa mfano, Chuo cha Kiislamu juzi tulitembelea pale Mazizini, yaani wao tayari wameshalipia kila kitu na huu ni karibu mwaka wa nne wameshalipa gharama na hadi leo hii bado hawajapatiwa hati miliki.

Sasa Waziri anayehusika na taasisi hii nini kimemkwazwa, kwa sababu Taasisi ya Serikali inataka hati miliki ambayo hati miliki hiyo inatolewa na Taasisi ya Serikali nyengine, hivi kuna kikwazo gani. Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kesho kutwa anakuja na bajeti yake, mpaka atupe sababu ya msingi kwa nini taasisi zetu hazipi hati miliki.

Kwa mfano, Chuo Kikuu (*SUZA)* pale wale ardhi yao imevamiwa na kesi wamekwenda mahakamani wameshindwa kwa sababu si aghalabu siku hizi taasisi ya serikali kwenda mahakamani na mfanyabiashara kushindwa, isipokuwa tutanyang'anywa mpaka utakutia hakuna pahala pa kufanya *extension* ya skuli na vyuo na hili ni tatizo kuna kikwazo gani.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, nafikiri wakati atakapokuja anaweza kutupa taarifa ni kikwazo gani ambacho kimekwaza mpaka hivi sasa, haya majengo yetu hayataki hati miliki.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Mbweni katika *Karume Institute of Science and Technology*, ardhi ina matatizo kwa sababu hiyo ya hati miliki, yaani wana mvutano na wafanyabiashara pale eneo la ardhi limevamiwa na mambo haya mpaka lini. Kwa hivyo, ninaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba muhakikishe bajeti ya Wizara Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati haipiti hapa mpaka atupe sababu za msingi kwa nini ananyima hati miliki kwa taasisi zetu za serikali na hilo moja. *(Makofi)*

Jengine kuhusu marekebisho ya walimu wa *TAP* Mhe. Waziri amelijibu kwenye swali langu. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nimeridhika sana na majibu ya Mhe. Waziri katika hili, lakini alisahau kunijibu lile la wale Wakufunzi walidai mafao na wao, vipi walikuwa kweli wameahidiwa kupewa mafao ambapo sasa wananung'unika hawajapewa.

Kwa hivyo, hayo ni kweli au ni malalamiko tu au waliahidiwa kweli na kama waliahidiwa basi mimi nashauri kwamba atumie busara zake, uzoefu pamoja umakini wake katika kuendesha mambo awalipe hao walimu haya mafao kwa ajili ya kuondoa hizi bughudha zilizopo hapa.

Mhe. Mwenyekiti, skuli ni sehemu ya kufundisha na kufundishwa, yaani inahitaji utulivu wa hali ya juu, pia inahitaji ukimya kwa kiasi fulani, ili watu waweze kupokea vizuri mafunzo. Kwa kweli inasikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba baadhi ya skuli hivi sasa kunajengwa majengo ya starehe karibu na skuli zetu, wanafunzi baada ya kuwa makini katika kusoma usiku wanasikia mishindo ya marumba pamoja na makelele ya wavuta bangi pamoja na walevi, jambo ambalo linapoteza kabisa *concentration* yao.

Sasa mimi nashangaa kwamba hili linatokea na watu wanapewa leseni kufanya biashara kama hizi karibu na majengo yetu kwa nini. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atueleze kwa mfano Skuli ya Fidel - kasro karibu na *mortuary* pale wanafunzi wanapata tatizo kuna vibaa vya ulevi pale na ile ni *high school*. Kwa hivyo waone tu kwamba kuna tatizo hili. Sasa kama Mhe.

Waziri hili analijua basi awasiliane na hawa watu wanaotoa leseni za mambo haya, kuona kwamba mahala kama mle hawatoe lesini, wala hawajengi kama ilivyo shule moja kubwa hapa Mjini, sitaki niitaje.

Sasa hilo ni tatizo Mheshimiwa, nadhani katika hili Mhe. Waziri hiyo shule ninayoikusudia keshaifahamu kwamba kuna magereji na mambo mengine. Watu asubuhi wanataka kusoma hawa wagonga vyuma, hawa wanafanya hivi, inakuwa ni tatizo kwa wanafunzi. Ilikuwe ni shule inayopasisha sana wanafunzi wake lakini sasa hivi matokeo yanakuwa mabaya siku hadi siku kwa sababu ya kuvamiwa katika eneo la shule na wafanyabiashara yakiwemo haya mambo ya mageriji na mambo mengine.

Kwa hivyo naomba sana katika hili Mhe. Waziri aje atueleze mikakati yake katika kudhibiti biashara katika majengo yetu ya shule hususan yale yanayoweka zogo kwa mfano mashine za landa, wanafunzi wanakosa raha ya kujifunza, walimuo wanakosa raha ya kufundisha kwa sababu ya zogo za mashine pale karibu na shule.

Mhe. Mwenyekiti, nende la nne sasa, kwenye mabadiliko ya tabia nchi, kwamba mabadiliko na naomba Mhe. Waziri anisikilize vizuri na sizungumzii Afisi ya Makamo wa Kwanza nazungumzia Wizara ya Elimu. Haya mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri sana nchi yetu na inachukua sana rasilimali ya nchi hii. Nisishangaliwe kwamba nazungumzia mabadiliko ya tabia nchi katika Wizara ya Elimu. Kuna ardhi ambazo zipo katika costal plain ambazo zina majengo muhimu sana ya Wizara hii ya Elimu, ikiwemo *SUZA* pale Chuo Kikuu cha *SUZA* katika *department* ya Nkuruma pale ardhi yake inamong'onyolewa sana na bahari. Hii ni kutokana na mabadiliko ya tabia nchi. Tutakwenda mpaka lile jingo la gorofa lile pale na ule Msikiti pale tuukose uingie baharini.

Mheshimiwa hili namuomba sana Mhe. Waziri ajaribu kutafuta uwezo wa moja kwa moja katika bajeti ya serikali au kwa kupinga kidogo kwa kupitia wafadhili, kusidi waweze kuweka *retaining wall* katika ile sehemu ambayo inamong'onyolewa na bahari katika Chuo cha *SUZA* pale Nkuruma.

Mhe. Mwenyekiti, kiwango cha elimu katika nchi yetu kinaanguka sana na moja kati ya sababu zinazoangusha kiwango cha elimu ni suala zima la hizi Kamati za Skuli. Kamati za baadhi ya maskuli zina tatizo. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Wanawake na Watoto ya Baraza lako hili tukufu. Nimebahatika sana kutembelea katika maeneo ya shule. Kuna kamati Mhe. Mwenyekiti haziisaidii shule na walimu wanaziogopa kamati hizo.

Kwa mfano kamati ya Skuli ya Haile Selassie, kwa taarifa nilizozipata juzi ni kwamba huu karibu ni mwaka wa sita haijakutana pale. Skuli kubwa kama ile kamati yake haijakutana na wakikutana wanataka wapate posho, lakini hawakutani kuwasaidia walimu juu ya kuendeleza shule. Iweje kamati iishi miaka sita bila ya kubadilishwa, na tumeambiwa sio sita tu karibu miaka 10 na zaidi haijabadilishwa kamati hiyo. Namuomba Mhe. Waziri katika hili aone kwamba kuna haja ya kufanya *feasibility study* kwenye kamati za skuli na ziondoke kwa mujibu wa utaratibu waliojiwekea, kama ni baada ya miaka mitatu kamati ivunjike basi ivunjike na ichaguliwe nyengine, sio kufanya *mon-archy* katika skuli, hawatusaidii hawa.

Nenda *Haile-Selassie* Mhe. Waziri utaona vituko hapo vya kamati za skuli. Hawaelewani baina ya kamati ya skuli na walimu. Wao hata wakitaka vikao lije posho tu basi lakini mambo ya kuendeleza shule hawana. Na iweje mjumbe wa kamati ya skuli awe ni mjumbe wa kamati ya skuli wakati yeye hana mtoto pale anayesoma. Na hii ndio ilivyo pale katika skuli ile, kuna wajumbe wa kamati ya skuli hawana watoto pale. Kwali watakuwa na imani ya kuitetea elimu. Namuomba Mhe. Waziri katika hilo awe makini sana.

Mhe. Sasa niingie katika Wizara ya Afya. Kwanza napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada zake pamoja na watendaji wake. Wamejitahidi sana kufanya mambo mazuri na makubwa katika hii hospitali yetu ya rufaa ya Mnazi Mmoja. Hili nampongeza Mhe. Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote katika hili. Pamoja na mambo mengi tuliyokuwa tukiyapigia kelele lakini nadhani kelele zetu zimesaidia na wamefika pazuri kama binaadamu. Kwa sababu wenzetu Waingereza wanasema usiache kumsifu mtu kwa lile zuri analolifanya. Sasa katika hili kiungwana tunawasifuni sana na mmejitahidi na endelezeni bidii katika hili. Ila kuna mambo madogo madogo ndio itabidi tuzungumzie katika hili ili kufanya vizuri zaidi jamaa zangu wa Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nizungumzie suala sima la wafanyakazi. Wafanyakazi wa Wizara ya Afya wana – *deal* na afya ya binaadamu tena katika kila kada kuanzia *orderly*, mtu wa lebo*, nurse*, daktari na kadhalika. Hawa wote ni watu muhimu sana katika kuona afya ya mtu inaimarika. Wenzetu wa Wizara ya Afya kutokana na kazi yao ilivyo nzito na ngumu hulazimika kupangiana zamu katika kazi zao, kwa sababu ugonjwa hauleti taarifa kwamba nitakuja asubuhi au nitakuja jioni au nitakuja wakati gani kwa vile ni lazima kila wakati katika hospitali kubwa kama Mnazi Mmoja pawe na daktari pamoja na sekta nyengine za kuhudumia afya. Kwa vile kuna watu wanaingia asubuhi mpaka saa 8:00 kuna wa saa 8:00 mpaka 3:00 kuna wa saa 3:00 mpaka saa 6:00 za usiku, kuna wa 6:00 za usiku mpaka asubuhi. Sasa mimi nataka niwazungumzie hawa wanaotoka usiku Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi hawa wana tatizo kubwa na wengi wao ni ma – *nurse* watoto wadogo wanaovutia sana. Inasikitisha Mhe. Mwenyekiti kuona mtoto anatoka Mnazi Mmoja hospitali mpaka kituo cha daladala usiku saa 6:00 peke yake anakwenda kutafuta daladala aende zake nyumbani kwao. Jambo hili ni tatizo na wengine pale hukamatwa wakaporo na wengine kutaka kujaribu kutaka kubakwa.

Mheshimiwa katika hili naomba wizara iwe makini sana kuwapelekea usafiri na hawa wafanyakazi wa Wizara ya Afya kutoka angalau pale Hospitali mpaka pale Mnazi Mmoja aweze kupanda daladala, hawa nurse wadogo wadogo watabakwa na wavuta unga humo barabarani, hili naliomba sana na Mhe. Waziri katika hili Ishallah ikiwa utaleta mambo yanayohusiana na hayo hapa tutakusaidia kuyapitisha kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, jengo la macho la Mnazi Mmoja limetumika karibu shilingi milioni mia moja na kufanyiwa ukarabati, jengo lenyewe juzi tumepita kwa mujibu wa wataalamu wanasema limedata, halifanyiki kazi hata wale wataalamu wa macho pale ni tatizo Mheshimiwa. Sasa ni sababu gani zilizosababisha hivyo, ni tatizo la mkandarasi au ni nini kwa sababu milioni mia moja imetolewa juzi juzi kufanyiwa ukarabati lile jengo la macho pale. Kwa nini liwe vile hoi bin taabani namna kama ile.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, mambo ya Mazingira na Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo. Pale kuna kitu kimetajwa katika ripoti ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yetu ambaye na yeye alikuwa makini sana katika kuwasilisha ni kwamba hawana kibanda cha kuchomea taka, kama kuna taka hatari sana miongoni mwa taka ambazo hazitakiwi zisambae katika maeneo basi ni taka za hospitali na za kwenye viwanda. Lakusikitisha taka zile huja zikachomwa moto kidogo nyengine zikiingia kwenye bahari huku zikiwa na maradhi, zinaingia kwenye maji *contamination* ya maji inatokezea.

Sasa nataka Mhe. Waziri akija hapa atwambie ni sababu ambazo kwa hospitali ambayo kubwa kama ile ya rufaa kukosa *incinerator*. Mnatumaliza kwa sababu there is independent of food baina ya vimbe kwa sababu samaki, sasa samaki si wanakula maradhi, halafu na sisi samaki wale tunawala, tutakuja kupata matatizo. Kunamnyororo wa chakula Mhe. Mwenyekiti, mataka wanayoyatupa yakasambaa kwenye maji ya bahari yaka *contaminate* maji, samaki wakala halafu na sisi tunakuja kula samaki huku wakiwa samaki *contaminated* ni tatizo. Wafanye haraka ili watueleze *incinerator* itapatikana pale.

Mhe. Mwenyekiti mafao ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya. Mheshimiwa kuhusu mafao nashangaa sana kuona kwamba, alisema Mheshimiwa mmoja hapa, kwamba kila mfanyakazi wa sekta ya afya ni muhimu kuanzia *orderly* mpaka kufikia daktari. Sasa nadhani wao menuse wakiingia usiku kwa mujibu wa taarifa tunazozipata wao hawana call lakini madaktari wanakuwa na call lakini *orderly* hana na wafanyakazi wengine hawana, ingawa walipwe kwa mujibu wa taaluma zao walakini wasibaguliwe kwamba mafao makubwa wapewe madaktari tu, hawa wengine wasipewe. Mimi nadhani na nurse anastahiki na yeye kama ni call kama ni *night allowance* na yeye apewe, orderly kama ni call kama ni *hight allowance* na yeye apewe, mtu wa *Xray* nay eye pia apewe kila mmoja.

Nimalizie kwa *DNA* Machine katika Wizara ya Afya. Mashine hii ni muhimu sana. Sisi Mhe. Mwenyekiti, tunahubiri siku zote demokrasia na utawala bora. Kesi nyingi Mahakamani zinapaswa kwa sababu ya kukosekana na *DNA* mashine. Na kwa sababu imeambiwa kwamba sehemu moja ya *DNA* mashine imeshapatikana ambayo sio muhimu sana kwa sababu wanaiita ni *Just DNA Extraction Machine* kuna zile *Analyzer* na *Result machine* sehemu mbili hazijapatikana.

Mimi nadhani Mheshimiwa sasa imeshafika wakati, hii Zanzibar ni nchi tuseme tukipiga magoti Tanganyika kila siku kwa ajili ya *DNA* tununue nyengine pale tuweke yetu tusinde tukipiga magoti Tanganyika. Hii ni nchi na tusijidhalilishe katika hili. Nadhani Mhe. Waziri akija hapa atatueleza ni lini watakamilisha hizo sehemu mbili. Ukiacha hii *DNA Extraction Machine* hiyo *Analyzer* na hizo *Result machine* zitapatikana lini.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa Utawi, wenzetu wa ustawi nampongeza sana yule mama. Lakini mpaka sasa hivi Mheshimiwa kuna matatizo ya kesi hizi za kubakwa watoto wetu wadogo. Mdano miye pale katika jimbo langu barazani tu kuna mtoto Badria Mohammed Ali wa Muhinani pale Vitongoji nilimtaja juzi alibakwa. Kesi yake haijenda huu ni mwaka wa nne. Kuna mtoto wa miaka sita ilimshuhudia Kamati yetu kabakwa pale Kituo cha Mkono kwa Mkono Chake Chake lakini kesi yake mpaka sasa hivi hatujui inaendeleaje.

Mimi nadhani Mhe. Waziri atatueleza hili atakapokuja, kesi hizi zimefikia vipi. Mimi namshauri Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba atuletee sheria hapa ili atakaeonekana na mambo hayo anabaka baka vitoto basi wahasiwe. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu Mkutukufu (*SW*) aliyetujaalia uhai, uzima, tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe kwa kunipatia nami nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika mada iliyokuwepo mezani asubuhi hii. Nianze na kuwapongeza mawaziri wa Wizara zote tatu waliotuwasilishia ripoti za utekelezaji wa maagizo. Lakini pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wake wa ripoti.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema nianze na kukumbuka historia ya nchi yetu, baada ya Mapinduzi ya 1964 Rais wa Kwanza hayati Mzee Abeid Amani Karume kabla ya kufariki kwake alifanya mambo mengi. Kwa muda wake huo hayati Mzee Abeid Amani Karume alijenga majumba ya maendeleo Michenzani, Mpaka, Gamba, Mkoani, Makunduchi, Wete, Kengeja, Chakechake, Micheweni n.k. Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hapo kwa kusema hivi je, sisi tumejikwaa wapi?

Mhe. Mwenyekiti, kwa utangulizi wangu huo ambao nauwekea *question mark* nianze na kuangalia ripoti ya maagizo kwa wizara ile ya Ustawi wa Jamii. Nimpongeze sana Mhe. Waziri na watendaji wake kwa jitihada wanazozichukua kuweza kuona kwamba wanafikia malengo.
Mhe. Mwenyekiti, katika agizo hili wao walianzisha vituo vya Mkono kwa Mkono One Stop Center, hili ni kweli ni hatua ya mwanzo kwa kesi kama hizi lakini kwa kweli wanakwazwa mno na tatizo la umaliziaji katika Mahakama kwa Ushahidi katika kesi hizi. Nasema kwamba vyombo vinavyohusika na hili vijitahidi sana kuona haki inatendeka katika tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, hapa hapa tunaona wazi kwamba tulipata taarifa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwamba kuna kipimo cha *DNA* kumbe haikuwa sahihi kwamba kilikuwepo kipimo hicho kwa uhakika. Wizara ya Ustawi iliamini kabisa kwamba tayari kimekuwepo kipimo hicho. Mimi ni mjumbe wa Kamati hiyo, tulikwenda huko lakini tuliambiwa kwamba kuna baadhi ya sehemu ya kipimo hicho na si kipimo chenyewe bado havijakamilika. Kwa hivyo ni kusema kwamba bado tatizo hili limekuwa sugu na gumu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa kwenye maagizo ya Kamati tuliwashauri hawa wenzetu kuwaanzishia miradi wanawake na watoto ambao wanakuwepo kule katika chuo cha mafunzo, tumeona jinsi walivyo na wanavyoishi tumekwenda kuona jinsi gani wanawake wanaishi kule. Hali tuliyoikuta kule tulipendelea mno waanzishiwe miradi ili iweze kuwanufaisha wao na watoto ambao wanakuwepo kule. Kwa bahari wamefanya mazungumzo, lakini wanahitaji ushirikiano wa kina na sekta nyengine husika ili kuona hali hizi za kuzuia udhalilishaji wa watoto basi na wao wawe wanapata huduma, ukizingatia kwamba ni muhimu sana kuweza kulinda naki za binaadamu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nione kwamba Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashataka sasa iendele kuzipitia zile sheria za kesi za jinai na kesi za madai ili kuondoa mahabusu wengi

waliolundikana ni wanawake, vijana na watoto, kesi ambazo zingefanyiwa utaratibu maalum basi suluhu yake isingefika kuwafikisha kule. Wizara hii kwa kuwa inahusika sana na vijana hao, wanawake na watoto, basi iko haja ya wizara husika kuliona hili ili washikiane nao ili suluhu ya matatizo mengine madogo yaweze kutatuliwa kwa urahisi na sio kuwalundikiza mahabusu wengi kama tulivyowakuta.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kuwepo kwa Ofisi Pemba. Serikali inakula hasara nyingi kwa kutokuwepo Ofisi au Wizara ya Ustawi Pemba. Wanatumia fedha nyingi sana kukodi kila mwaka. Ndio pale nilipoanza na kusema kwamba sisi tulijikwaa wapi? Kila unapogusa na kila wizara inapoguswa basi tatizo la jingo linajitokeza hapo. Nadhani umefika wakati sasa serikali ione ina majengo yake yote ya Ofisi ili shughuli zetu ziende kwa ufanisi basi hatuna budi kuwa na ofisi nzuri za kuwaweka wafanyakazi wetu. Tunatumia fedha nyingi kwa kukodi kama tungejiwekea mipango madhubuti ya kujenga Ofisi basi nadhani pesa hii ingetumika katika utaratibu mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Wizara ya Afya. Niseme kwamba tuliridhishwa mno Kamati yetu na kuliona jingo zuri la Mkemia Mkuu linaendelea vizuri. Lakini hiyo haitoshi niseme tena kwa upande mwengine wa pili Pemba inahitajika Ofisi kubwa ya kisasa ambayo itaweza kufanyiwa kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika tatizo la wafanyakazi katika Hospitali za vijijini na Wilayani ambapo tuliacha agizo la kupatiwa wafanyakazi. Nilikuwa Napata mashaka na wasi wasi, kwani nia yetu ni kuboresha huduma za afya. Unapotaka kufanya hilo ni lazima uwe na wafanyakazi na vitendea kazi. Utakapoleta mchele mtupu huwezi kula pilau ni lazima upate mchanganyiko.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Ajira na Utawala Bora, Wizara ya Afya iliomba wafanyakazi 816 wa kada tofauti, walipatiwa watu 14 tu kibali cha kuajiri. Hiyo inaonyesha dhahiri kwamba hata ukimwambia atende atashindwa kulifanya hilo. Lakini pia akapeleka kaombi ambayo yanahitaji watu 418 na hatimae akapewa watu 49 2011/2012. Hii inatuonyesha wazi kwamba hatuwezi kufikia yale malengo tuliyoyakusudia. Nadhani ipo haja sasa ya kuona wapi tumejikwaa ili tuweze kufikia malengo.

Wizara hiyo nimemaliza hilo, lakini nije tena kwenye maagizo ya Kamati nije kwenye Wizara ya Elimu. Hapa katika ujenzi wa Secondari 16 za Wilaya, Skuli nyengine nashukuru sana niseme nawapongeza sana walifanya vizuri wakandarasi wengine. Lakini kuna wakandarasi ambao hadi hii leo bado wanaendelea kudhalilisha Wizara ya Elimu na kutumia fedha zetu kinyume na utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Skuli ya Paje Mtule, Tunguu na Dimani kwa kweli wakandarasi hawa hawafai na sasa wizara serikali isimamie hili kuona inawasitisha tena bila ya gharama ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye Bodi ambayo zamani tukiita Bodi ya Upimaji na Tathmini ambayo saa tunaita Baraza la Mitihani. Maelezo ya Kamati hapa Majibu yake kwamba jengo la Ofisi hii ni bovu sana, ni mashaka hata kulipanda kwa mtu yoyote. Sisi tulivyokwenda pale tulikuwa tunawasi wasi kwamba wakati wowote linaweza likadondoka chini. Lakini tulitoa maagizo kwamba wafanyakazi wale watafutiwe Ofisi ili waweze kwenda.

Jibu lake anasema kwamba ni lazima wahame watu wa Shirika la Bima yaani wafanyakazi ndipo wapate wao Baraza la Mitihani wahamie. Kama wakiwa Bima hawakuhama ina maana hawa watabaki hapo hapo. Na lolote likitokea nani alaumiwe? Kwa sababu jingo hilo lina hali mbaya sana na ndio pale niliposema mwanzo kabisa serikali ni lazima sasa isingatie kuwa na Ofisi zake wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nije Kengeja kwenye Chuo cha Ufundi, niseme kwamba ni ukweli usiofichika kuwekeza katika elimu ni suala la msingi lakini vyuo vya ufundi ni muhimu sana kwa maendeleo la taifa hili . Pili ni kuona kwamba wanafunzi wetu wanapomaliza pale vijana wetu wanapata ajira na wanakuwa na uwezo wa kujiajiri wenyewe. Hivi sio vyuo vya kuvichezea ni vya kuongeza juhudi maarifa na kuingiziwa fedha na kukamilishia mahitaji yao kuona wanapotoka pale hawa ndio vijana wanaoweza kujiajiri wenyewe na hilo ndio tatizo la serikali. Kuna nini mpaka shule hiyo haina hada dahalia, dahalia yake imetengewa fedha milioni mia nne, itanunua vifaa vya umeme kidogo lakini imetaka uwajiri wa walimu wawili wa fani hiyo ya umeme, huu ni mwezi wa tisa bado walimu wawili hawajaajiriwa. Tukiulize kuna nini? Huo ndio utendaji, tutafikia malengo? Nadhani kuna masuali mengine ni ya kiutendaji. Ipo haja ya usimamizi mzuri wa shughuli zetu ili tuweze kufikia malengo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niondoke huko nije katika mchango wangu katika wizara hii hii ya ustawi. Kwa kweli nimepata mashaka makubwa kuona Wizara ya Utawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto ni wizara ambayo bajeti yake ni finyu mno, haikidhi h aja. Lakini bado serikali inaendelea kuwapa mzigo mkubwa wa kulipa fidia za wafanyakazi. Hii ni kuwaonea, hawamudu hilo na serikali inalifahamu hilo. Kwa sasa inalimbikizo la deni la milioni thamanini na nane, laki saba arubaini na tano mia saba na ishini na tatu. Deni hili hawawezi kulilipa, serikali ni lazima hili lirudi hazina, ofisi, Wizara ya Fedha na Mipango ya Maendeleo ilibebe deni hili kuwalipa wafanyakazi hao haki zao.

Hii naiyomba sana, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ya Maendeleo deni hili awaondoshee mzigo huu watu wa Wizara ya Ustawi, hawamudu kabisa, au mlimbikano utaendelea siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niseme kwamba kuna tatizo la ajira za watoto. Mheshimiwa hili ni lazima tulisimamie, watoto hawajafikia kimo lazima wapewe taaluma ili waweze kujiendeleza. Mhe. Mwenyekiti, kila nikiona wakati wangu unapotea haraka niiache hiyo wizara na nije kwenye Wizara ya Afya kwenye hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wamejitahidi kwa kiasi fulani lakini yale niliyoyatanguliza mwanzo ndio maneno. Utakapohitaji chakula kitamu na kizuri lazima upeleke vifaa. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri wa Fedha na Mipango ya Maendeleo, iko haja ya kuingizwa fedha hizi kwa utaratibu ili haya yaweze kutekelezeka. Mimi nadhani hii ni ndoto na kama kweli tunahitaji kulifanya hili basi hatuna budi lazima lazima waingiziwe fedha, kwa sasa hospitali hiyo ya rufaa haina sasa hivi *X-Ray* mashine zake tatu ni mbovu, *Ultra sound* haifanyi kazi, hali ya hospitali ya rufaa je tutafikia malengo.

Mhe. Mwenyekiti nije kwenye mradi wa ujenzi wa Kitengo cha Macho. Mheshimiwa hapa mradi huu uli-*cost* milioni 130 lakini mkandarasi amelipwa shilingi milioni 25 tu, jengo ni bovu limepasuka na haliwezi kulazwa wagonjwa kwa sasa. Tujiulize kuna nini mpaka imefikia hatua hii nadhani usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za umma ni suala la msingi, na ni tatizo kubwa kwa serikali yetu kuweza kufikia hatima katika matatizo kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na hilo nije hapa kwenye jengo la tiba asilia hawa kwa kweli ofisi yao ni finyu sana inahitaji kupatiwa eneo kwa sababu wanaishi kwa ufinyu na shughuli zao haziendi kiufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, nikifika sasa kwenye huduma za mama wajawazito kuwa bila ya malipo, hasa ndipo yalipo hasa masikitiko yangu ambayo nilikuwa nayakimbilia mno. Mhe. Mwenyekiti, Rais wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein aliondoa malipo ya wanawake wanaokwenda kujifungua hii ilikuwa ni maagizo ya Rais. Kwa masikitiko makubwa vituo vyote vya kujifungulia mama wajawazito ikiwemo na Mnazimmoja hospitali ya rufaa wananchi wanalipia. Hebu niulize swali kulikoni kuwa amri ya Rais au maagizo ya Rais kutotekelezeka tunakwenda wapi katika serikali hii hapa tulipofikia. Ikiwa la Rais halikusikilizwa litasikilizwa hili Baraza la Wawakilishi. Naomba sana kabisa kupitia Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuona tunazipata fedha hizi na haki yetu ya msingi wanawake ambayo Rais ametutakia msamaha huu iweze kutekelezeka. Vyenginevyo ni kuona kwamba ni mtihani.

Mimi nimeona agizo la meli tulipopata maafa maana mpaka yatokee maafa ndio tuweze kujihami, wakati alivyoagiza Rais tulikata mikato mbali mbali, hivyo basi Mhe. Mwenyekiti niiombe sana serikali turudi kwenye historia hatuwezi kufikia malengo kama hatukurudi kwenye historia tuliyotoka. Rais aliyeanza akaleta Mapinduzi matukufu 1964 amemudu mambo mengi kwa miaka 8 tu hadi alipouwawa. Sisi tunashindwa na nini tumekwazwa na kitu gani hebu tukae tujiulize tuna nini tuangalie tunakotoka, tulipo na wapi tunapahitajia kwenda kwa maslahi ya wananchi wa taifa hili. Vyenginevyo wananchi hawatatuelewa, wamechoka sana kuona serikali iko mbioni, mbio hizo haipatikani kila inaposhikwa basi inazidi kusogea tu mbio. Wamechoka kusikia kauli hizo na kinachotakiwa sasa ni utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti isifike pahala wananchi wakatusuta ni vitu visivyopendeza havijengi haiba na usataarabu wa Wazanzibari tulivyozoea kuongozana. Mheshimiwa katika msingi huu wa demokrasia tutawapa nafasi naomba sana serikali yetu ifikirie sana kabisa kuirejesha huduma ya wanawake wanaokwenda kujifungua katika vituo vyote kwa kupatiwa vifaa ambavyo Rais amesema ametoa msamaha.

Mhe. Mwenyekiti, niende tena Pemba, Mhe. hapa bwana kuna kukosekana kwa fedha za maendeleo kimekwaza nini kwenye Wizara mpaka pesa za maendeleo Pemba ya miradi huko zinakosekana, nini hasa kimekosekana mpaka pesa za maendeleo haziendi Pemba. Mhe. Waziri naomba utakapofika hapa utueleze utuelimishe tuweze kuelewa nini hasa kinakwaza mpaka fedha za maendeleo zinabaki hapa Unguja na hazifiki kule.

Mhe. Mwenyekiti nilikwenda haraka ili nilifikie lile la wanawake sasa nirudi kwenye Wizara ya Elimu nilifanya hilo kwa khofu kidogo kwamba muda wangu ungeweza ukaenda.

Mheshimiwa niseme basi kwamba kuhusu zile skuli zetu za sekondari Wizara ya Elimu. Sekondari 16 zimetumia fedha nyingi lakini sekondari hizo hazina dakhalia, hazina nyumba za walimu, na hao wanafunzi wanaotaka kupelekwa kule hatujui itakuwa kuwaje, je hizi fedha zilizopotea za walipa kodi na utaratibu gani Waziri aje kunieleza aliyoupanga wa kuwapata walimu, kujenga dakhalia hizo ambapo kuweza kufanya kazi kwa sababu sasa zimeshakamilika anieleze itakuwa kuwaje na nyumba za kuishi walimu anipatie tu niweze kuelewa utaratibu gani utatumika ili sekondari hizo ziweze kufanya kazi kwa maslahi ya watoto wetu kupata elimu iliyo bora na iliyo makini kabisa kwa uzuri kabisa ili kuweza na wao kuliendeleza taifa hili.

Baada ya kuyasema hayo Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana, naunga mkono hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati hii. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nami asubuhi kupata nafasi ndogo kutoa mawazo yangu machache juu ya ripoti hii tuliyonayo mezani petu ambayo inakusanya Wizara tatu. Kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara ya Afya na watendaji wake hasa Waziri wake, Naibu wake, Katibu Mkuu na wengineo. Sisi watu wa vijijini mtu yoyote ambaye anafanya kazi hospitali tunamuita dokta, kwa hivyo ninampongeza sana dokta Juma Duni. Hata *orderly* sisi watu vijijiji tunamwita dokta kwa sababu tu anatoa huduma hospitali kwa hivyo madaktari wote ninawapongeza kwa huduma wanazozitoa ingawaje kasoro za hapa na pale zipo za kibinaadamu lakini kwa kima fulani wanatoa huduma nzuri kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kusimama hapa kutoa haya maelezo machache. Mhe. Mwenyekiti hata maendeleo nayo yana matatizo yake. Kumuwezesha mtu ili akubali kufuata maendeleo kule kukubali kwakwe na kufuata masharti ya maendeleo nako kunaleta tatizo kwa sekta husika. Kwa mfano Wizara hii ya Afya inatuelimisha, inatuelekeza na inatufahamisha kwenda hospitali pale tunapoumwa, kinamama kwenda *clinic* kupima wanapokuwa wajawazito, kadhalika kwenda kucheki afya zetu. Pale tunapoelimika na tukafuata haya maagizo tatizo linajitokeza, mara nyengine watu wanakuwa ni wengi wakashindwa kuwahudumia. Kule kushindwa kuwahudumia kwao kwa ajili ya watu kuitikia wito ni tatizo la kimaendeleo. Kwa hivyo kwa kima fulani tatizo hili la kimaendeleo katika Wizara ya Afya lipo kutokana na watu kuitikia wito wa Wizara ya Afya. Na mara nyingi Mhe. Mwenyekiti huwa kuna mrundikano wa wagonjwa na baadhi ya wakati hasa katika sehemu za watoto kitanda kimoja kulazwa zaidi ya mtoto mmoja.

Mhe. Mwenyekiti mtoto mgonjwa tunapowalaza zaidi ya mmoja hii ina maana kitanda kile wanatumia watu wanne kwa sababu kila mtoto ana mama anayemuhudumia. Na kila mtoto pengine kenda na magonjwa yake tofauti, khofu yangu katoka kuja pale kutibiwa na kila mtu ana ugonjwa wake na kuna magonjwa mengine ya kuambukiza, sijui kuna utafiti gani wa kuwalaza wagonjwa kitanda kimoja je, tumefanya utafiti ugonjwa huyu na huyu unakubaliana? Hatoambukizana na kadhalika. Matatizo kama yapo hasa kule Abdalla Mzee hutokea sana matatizo ya aina hiyo.

Mhe. Mwenyekiti baadhi ya wafanyakazi wa hospitali hawakuhitimu vyema mafunzo ya *province night guide* baadhi yao wanapotoa huduma kwa wagonjwa lugha zao hazielekei kuwa lugha hii aelezwe mgonjwa. Ningeomba Wizara hii iendelee kuwaelimisha zaidi wale wanaotoa huduma kwa wajawazito wanapokwenda kujifungua lugha zao ziwe laini, ili wawape moyo

badala ya kuwapa maneno ambayo matokeo yake yanakasirisha. Mwanamke anapokuwa katika hali ile anahitaji kupembelezwa kwa sababu yuko katika hali mbaya, kwa mjamzito na kujifungua salama ni siri yake Mwenyezi Mungu tu lakini mzigo alionao na halafu ukamtwika na maneno mengine ambayo si mazuri kwa kweli ni tatizo.

Ningeomba kuwa wale ambao wana lugha ambazo si nzuri wajirekebishe kwa sababu ndio hasa kazi yao ni kutoa huduma kwa lugha laini. Ingawaje na sisi wagonjwa baadhi ya wakati tunakuwa na lugha mbovu lakini lugha zetu mbovu zisijibiwe katika ubovu wake kwa sababu sisi wengine hatujui chochote unakwenda pale pengine mgonjwa wangu hapati huduma nikaripuka, mhudumu yeye asiripuke kwa sababu yeye ana mafunzo maalum ya kazi aliyoifanya mimi sina mafunzo ya kiafya. Kwa hivyo dokta ningekuomba kwa wale ambao bado wana lugha hizi waelimishwe, wafahamishwe ili wawe na lugha nzuri kwa wagonjwa. Kwa sababu mgonjwa anahitaji kuhudumiwa vyema.

Waziri alipokuwa akisoma karatasi yake pale kwenye mgao wa dawa alisema sasa dawa zinagaiwa kwa mahitaji katika vituo vya afya. Kama nimefahamu ndivyo ina maana vile vituo vyetu vya afya vinapeleka mahitaji yao na matokeo yake wanapatiwa dawa kama walivyoomba ndio maana tukasema dawa zinagaiwa kwa mahitaji. Kama ni hivyo hivi karibuni nilipita katika kituo cha Kengeja ilikuwa mwanzo wa mwezi hata *panadol* ilikuwa hakuna na nikamuuliza kwa sababu nilikuwa nishasikia kuwa dawa zigaiwe kulingana na mahitaji. Sasa kama ni kweli wanafanya vizuri wanapeleka kulingana na mahitaji yao kwa nini dawa iwe hakuna na wamepeleka kutokana na mahitaji yao?

Mhe. Mwenyekiti nije katika sehemu ya kupambana na malaria. Malaria ni moja katika magonjwa ambayo yanaua watu kwa wingi na mapambano haya ya malaria yameanza kabla ya Mapinduzi haya yaliyopo. Ninafikiri miongoni mwa miaka ya 50 ilikuwa malaria yapo kwa wingi Zanzibar na WHO ilianza kutoa huduma hizi na wakaendelea kupambana na malaria mpaka kufikia kasoro ya 1% ya wagonjwa Zanzibar. Lakini baada ya kufika katika kiwango hicho na kutokea Mapinduzi kidogo yalisahauliwa malaria halafu yakaibuka tena upya kwa kasi mno, serikali ikaanza tena kupambana na malaria kwa kazi vile vile wakati huo kuna mabalozi wa nyumba kumi kumi, kila balozi alikuwa anapewa kopo la vidonge kwa wakati huo tulikuwa tunaviita vidonge vya balozi ninafikiri mna vidonge elfu moja.

Kila balozi anawapa watu wake vidonge 20 kwa lazima. Hali hiyo ikaendelea, malaria yakaanza kupungua tena tukaacha, yakaibuka upya. Sasa hivi tuna mchakato mwengine unaendelea kupambana na malaria na tumefika pahala baadhi ya wakati ukienda hospitali hivi sasa hapo kati kati kidogo hata kama una malaria unaambiwa si malaria, kwa sababu tulifika pahali tukasema malaria hakuna tena. Lakini bado walikuwa watu wachache wanaugua malaria. Sasa sijui kwa nini tukasema hakuna na bado wachache wapo na bado hii kasi ya kupanda malaria bado inaendelea. Ninaloiomba Wizara hii huu mradi wa kupambana na malaria uwe endelevu isifike pahala tukaona aa sasa tumefikia 0.5% au 0.2% tukaona basi hayapo tena tuendelee kupambana nayo hadi pale tuone kabisa hakuna. Kama serikali ilivyomudu kupambana na buba, wengi waliopo hapa hawajui hata mimi nikitaja huo ugonjwa wengi waliomo humu hawaujui, buba wewe hujui mtoto mdogo Mheshimiwa.

Sasa na malaria tupambane nayo mpaka tufikie kiwango kama vile tulivyoishinda buba. Mhe. Mwenyekiti hapa Mhe. Waziri alipokuwa akiwasilisha alitaja maombi ya ajira alikuwa na maombi 418 katika mwaka 2011/2012 lakini alipatiwa ajira ya vijana 49. Sijui ni asilimia gani hii ya maombi yake. Serikali isiidumaze hii Wizara kwa sababu wameomba kulingana na mahitaji lakini wapewe kasoro tena kasoro kweli kweli ya mahitaji yao, hapa ndio tunafanya nini? Sababu yetu ya msingi ni ipi kwa Wizara imeomba kiasi hicho lakini ikapewa kile kiasi kidogo walichopewa, sijui serikali ina sababu ipi ya msingi kuwakosesha watu wa afya maombi yao ya ajira kama vile walivyoomba. Lakini baadae alisema tarehe 1/10/2012 hadi tarehe 1/10/2013 walipata kibali cha kuajiri vijana 192, lakini hapa hakusema kama wote hawa waliajiriwa au la je nimuulize je hawa wote 192 waliajiriwa wote, na kama waliajiriwa je hawa ni miongoni mwa wale waliokosa mwanzo kule au ni wengine wapya?

Na kadhalika katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 waliomba ajira 816 na walizopata ni kumi nne kama ingelikuwa ni mtu aliyekuomba mtu wa kawaida nje huko kanambia Mhe. Mohammed Haji nigaie shilingi mia na ikawa ile shilingi moja au senti ziko kule mimi nikampa senti tano, kwa baadhi ya watu alirudisha mwenyewe kama huna kwa hii nakusamehe. Ni sawa na hii katika 816 kapewa 14, ingawaje kuwasamehe hawezi lakini nina hakika kuwa hakufurahia. Kwa hivyo hii ndio Wizara ya Afya ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa dakika zangu zilizobakia ni chache tena chache, nadhani huwezi ukaniongeza hata moja lakini ningeomba uniongeze kwa sababu haki yangu ya kusema ndio hivyo unavyoisikia.

Nije katika ukurasa wa 76 inayohusu Wizara ya Elimu, idadi ya Wilaya za Unguja ni nyingi yaani 6 ukilinganisha na Wilaya za Pemba ambazo ni 4. Hivyo idadi ya skuli za msingi na za sekondari za Unguja ni nyingi zaidi ukilinganisha na za Pemba. Kufuatana na ukweli huo Unguja kuna jumla ya walimu wa msingi na sekondari 7340 wanaume 2237 na wanawake 5103. Wakati Pemba kuna jumla ya walimu 2688 wanaume 1326 na wanawake 1362 takriban nusu ya idadi ya walimu walioko Unguja. Katika uteuzi wa walimu kusahihisha mitihani ya darasa la saba na kidato cha pili; walimu kutoka skuli za Unguja na wale kutoka skuli za Pemba huwa wanachaguliwa na kushiriki katika kusahihisha mitihani. Kwa vile Unguja ziko skuli nyingi na walimu wengi zaidi kuliko Pemba hivyo walimu wengi wanaosahihisha mitihani huchaguliwa kutoka Unguja. Ukichukulia kiasilimia walimu wa Pemba na Unguja wanapata nafasi sawa za kusahihisha mitihani.

Hapa ndio kwenye hoja yangu. Mhe. Mwenyekiti, sina takwimu ya kusasahihisha mitihani kwa mwaka 2000 lakini nimechukua ya ile ya 2011 ambayo jumla ya walimu waliosahihisha mitihani kwa *primary* walikuwa walimu 307 na *form 11* walikuwa 460 hawa ni kwa ujumla wao. Unguja *primary* walitoa walimu 300 na *form 11* ilitoa walimu 445 kwa jumla ni walimu 745 sawa na asilimia 97.12 ya walimu wote waliosahihisha mitihani. Sasa nikiambiwa kiasilimia ni sawa naomba kama hesabu yangu mimi si sawa nifahamishwe nione huo usawa kiasilimia hapa upo wapi? Nakubali kwamba Unguja ni kubwa, walimu ni wengi na Wilaya ni nyingi. Kwa ujumla walimu wote waliosahihisha kama tungechukulia hiyo iwe sawa ni 767 Wilaya zenyewe ni 10 kama tukiigawa kwa kumi kila Wilaya ingelipata *at least* walimu 77 hapa ingelikuwa huo usawa upo. Lakini hii lugha iliyotumika hapa kuwa ni sawa kwa mimi itabidi nipate maelezo mengine ili nikubali kweli ugawaji huu ni sawa kiasilimia, si kwa idadi ya watu.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Ufundi Kengeja. Kile Chuo kinafundisha mambo ya ufundi, lakini tokea kuasisiwa kwake mpaka hii leo kuna fani bado hazijafundishwa na nyengine zinafundishwa kinadharia. Hivyo ni kweli wale watoto tuliowapeleka pale wapate ufundi na hatimae wajitegemee au tumewapeleka watumie miaka yao 4 halafu waondoke waje wahangaike. Kama kweli Wizara imekusudia kweli kweli kukifanya Chuo kile au Sekondari ile iwe ni ya ufundi naomba waifanye kuwa ya ufundi, tena iwe ya ufundi kweli kweli. Iwe na sifa zote za ufundi.

Kwa hivyo naomba Chuo kile kiwe cha ufundi kweli kweli na wala kisiwe cha ufundi kijina tu. Kwa kuwa dakika mbili nilizopewa zinamalizika, nirudi kwenye Wizara ya Afya kidogo tu.

Kuna mara moja Waheshimiwa tulifanyiwa semina kuambiwa kwamba Vituo vya Afya sasa basi kwa sababu ule mpango kuwa mwananchi asiende zaidi ya kilomita tano umekamilika, na kama Wajumbe mkijenga hiyo itakuwa wizara haitambui na itakuwa haimo kama sikusahau. Lakini katika Wilaya yangu ya Mkoani kuna jimbo linajengwa kituo cha Afya, Jimbo la Mkanyageni je, hiki hakitohudumiwa na serikali?

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii na mimi nichangie mawili matatu katika Wizara zetu hisi tatu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa uwasilishaji wake mzuri ambao ameuwasilisha hapa katika Baraza letu hili. Na pia niwapongeze mawaziri wengine ambao wamewasilisha ripoti zao hizi za kamati katika Baraza letu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Makamo Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wake wote kwa kuwasilisha ripoti yao hapa na kuacha maagizo yakafanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze katika Wizara ya Elimu. Mimi nataka niungane na kamati kuhakikisha kwamba ujenzi wa Skuli za Paje, Mtule, Tunguu na Dimani zinafanywa na Kamapuni ya *Electrics International* ya Dar es Salaam kunakuwa viwango vilivyokusudiwa na unazingatiwa wakati kwa mujibu wa makubaliano ya sheria.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nasema niungane nao, kwa sababu ujenzi utakapojengwa ukawa mzuri naamini wanafunzi wetu watakuwa tayari wanasoma pahala pazuri na ambapo pa kutegemewa. Lakini vile vile ujuzi utakapokuwa ni ovyo wanafunzi wetu watakuwa katika matatizo ambayo hata sisi wazazi hatustahili kukubaliana nayo. Nikija katika wizara ya Mhe. Waziri aliyeagizwa maagizo kuwa anapenda kukiri kwamba baadhi ya maagizo hayo hayajapatiwa ufumbuzi kamili na yataendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo kutokutekekelezwa kwa maagizo hayo na kwa kuwa serikali baada ya kutekeleza maagizo hayo izingatie kwamba majengo yatakayojengwa yanapatiwa wakandarasi ambao wana kiwango cha kujenga majengo hayo na sio kutafuta wakandarasi ambao hawastahiki hata kujenga majengo na hatimaye majengo kama hayo hubomoka. Mfano mdogo Mhe. Mwenyekiti, juzi tu Dar es Salaam pameanguka jengo si dogo ambalo lina urefu wa

ghorofa 16, zimeporomoka na hatimaye kuathiri watu wetu. Kwa hivyo, naiomba wizara hii inapotafuta wakandarasi itafute wakandarasi waliokuwa watajenga majengo yetui yenye uhakika.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niingie katika kuanguka au kushuka kwa kiwango cha elimu Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, suala hili linatusikitisha sana kuanzia wazee mpaka watoto wetu, hebu tujiulize au tuiulize serikali ni kitu gani hasa kinachosababisha kuanguka kwa kiango cha elimu Zanzibar. Hili naomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nije katika Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ipo sehemu inayosema kwamba, wizara kuzingatia upatikanaji wa dawa muhimu kwa wagonjwa wa akili ili ziweze kusaidia matibabu kwa wagonjwa hao. Halafu mhe. Waziri akasema kwamba, wizara imeshaandaa mfumo *Frame Work Contract* kwa ajili ya kumpata msambazaji dawa kwa mwaka mzima.

Mhe. Mwenyekiti, hapa niiombe serikali, serikali ihakikishe kwamba huyoi msambazaji wa dawa awe ni mtu ambaye ana uaminifu na mwenye elimu ya kutafuta dawa hizo na kusambaza katika vituo. Kwa sababu isije ikawa mtu huyo anakwenda kutuokotea dawa ambazo hazina kiwango na kuzileta hapa katika hospitali zetu.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, niiombe wizara hii kufanya uchunguzi wa maradhi ya miguu, nyonga, pamoja na magoti ili iweze kuwapatia dawa wananchi. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, wananchi hivi sasa wengi wao wanaumwa na miguu, nyonga pamoja na magoti, sasa niiombe wizara hii ifanye utafiti zaidi ili kulitafutia ufumbuzi suala hili ili watu weti waweze kufanya kazi zao kwa umakini. Ukiangalia hivi sasa wananchi na wafanyakazi wengi wanashindwa hata kutembea. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili alifanyie utafiti ili tusiweze kupoteza nguvu kazi za watu wetu nikiwemo na mimi mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Wizara yetu hii ya Wanawake na Watoto. Kwanza niipongeze tena wizara kupitia taasisi zake imejitahidi kuvifanya vikundi kupiga hatua kwa kuviimarisha. Hili nimpongeze sana Mhe. Waziri. Lakini pia kiasi kwamba UN *Habitat* kuendelea kuvitambua vikundi hivyo ili viweze kupata misaada kutoka katika mashirika mengine.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe wizara isiishie hapo tu, yapo mashirika mengine ambayo yanaweza kusaidia vikundi vya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, juu ya vikundi hivi ni muhimu zaidi kutafutiwa elimu na pia nimuombe Mhe. Waziri asichoke kutoa taaluma kwa vikundoi hivi. Kwa sababu hivi sasa kuna vikundi ambavyo tayari vinaanza kufa na kusinzia kutoka na kukosa elimu ya ushirika. Vikundi vingi tu vipo ambavyo sasa hivi vinakosa elimu ya ushirika, nimuombe Mhe. Waziri hili suala alione, avipe elimu vikundi hivi ili navyo vipate mwelekeo kama vikundi vyengine ambavyo vina mwelekeo sasa hivi.

Pamoja na hili, bado viko vikundi vimeshindwa kupata usajili. Mhe. Mwenyekiti, karibuni hivi nilitembelea vikundi kiasi ya vinne bado havina usajili na wakati vikundi hivi tayari vimeshatoa pesa kwa maafisa wa ushirika, lakini kila wanapowauliza wanaambiwa subirini kidogo na hatimaye majibu mtayapata, lakini Mhe. Mwenyekiti mpaka hatima hii niliyoondoka bado vikundi hivyo havijapata usajili. Namuomba Mhe. Waziri afanye haraka kwa maafisa hawa kuwaelimisha kwamba, wanapochukua fedha za vikundi wafanye haraka kuwapatia usajili wao,

kwa sababu vikundi hivi vinashindwa hata kuweka pesa zao benki, wanashindwa hata kupata misaada kutoka kwa wafadhili.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimuombe Mhe. Waziri kwamba aangalie jumuiya ya Wanawake wajane pamoja na watoto mayatima. Jumuiya hii ipo katika Jimbo la Mtambile, katika Shehia ya Mjimbini na tayari imeshapata usajili na vile vile ina *account* number. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba ikiwa jumuiya hii bado hujapata kuiona nakuomba uitembelee jumuiya hii ili kwanza wamuone wiziri wao na pia uwease kuwasaidia hasa ha mayatima kwa sababu matatima utakapowasaidia kuna juhumu kuba kwa mwenyezi Mungu na utapata fadhila zake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niishie ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa leo kupata nafasi hii na kuweza kuzungumza kidogo tu baada ya muda wa siku nyingi kukaa kimya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nianze kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa muwasilishaji wa taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, Mhe. Hija Hassan Hija. Mhe. Mwenyekiti, kamati hii imefanya kazi za wizara tatu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa ikiwa ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mengi wamezungumzwa na kwa mujibuwa wa Kanuni ya kifungu cha 59.1 ukurasa wa 43 kwa hivyo nitajitahidi kama inavyowezekana kutumia muda mdogo kwa kuzungumza yale ambayo sikuyasikia kuzungumzwa na wengi wataalamu wetu waliotangulia kuchangia.

La kwanza Mhe. Mwenyekiti, nitaanza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, kama tukitizama taarifa hii ya utekelezaji kamati iliagiza wizara kutumia busara ili mikopo iliyotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambao waajiriwa katika Taasisi za Serikali hili liweze kurejeshwa deni la shilingi bilioni 8 walilokopa. Ni kubwa na linaathiri maendeleo ya bodi kwa ujumla. Sasa hapa kwanza Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya kamati ni kuwa deni linalodaiwa ni bilioi nane ikiwa ni sawa na shilingi elfu nane milioni. Lakini katika taarifa ya utekelezaji ni kuwa wizara imekubali kwamba, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 wizara ilishindwa kulipa Baraza la Mitihani la Taifa deni la watahiniwa wa kidato cha nne ambazo ni jumla ya Shilingi 434,490,000.

Mhe. Mwenyekiti, katika taarifa ya serikali ni kuwa, jumla ya deni wanalodaiwa wanafunzi ambao wameshamaliza masomo ya elimu ya juu baina ya mwaka 2006 na elfu mbili ni Shilingi 4,000,000,000. sasa kule kwenye kamati kumeaddikwa jumla ya shilingi bilioni nane, lakini hapa pameandikwa ni bilioni nne. Kwa hivyi nataka kujua sahihi ni shilingi bilioni nane kama ilivyoelekezwa na kamati ua ni shilingi bilioni nne kama ilivyo katika Ripoti ya Utekelezaji.

Jengine Mhe. Mwenyekiti ni kuwa hadi mwezi wa Machi, 2013 wanafunzi 1,564 waliopewa udhamini wa Bodi wamemaliza masomo yao. Lakini ukija katika kitabu cha ripoti ukurasa wa 74

wanafunzi hawa ni 1,230 sasa ni ipi sahihi, ni hii 1,564 au hii 1,230, na hapo nataka kupewa maelekezo.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kamati iliagiza wizara kutumia busara ili mikopo hii iweze kurejeshwa kama nilivyotangulia mwanzo, lakini Mhe. Waziri anasema wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora vile vile Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Idara ya Vitambulisho vya Zanzibar wameweza kuwatambua wafanyakazi waliopatiwa mikopo kupitia Bodi yao. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nilifikiria wakati wizara hii ndio inayotoa mikopo ilikuwa iwe na takwimu sahihi huyu tunampa mkopo kiasi kadhaa, mwaka kadhaa na kamaliza iweze kujua watu hao. Sasa ilikuwa kuna ulazima gani wa kushirikiana na wizara hizi mpaka Idara ya Vitambulisho kwa kuwatafuta watu ambao walipata mikopo. Hii ina maana kuwa, Wizara ya Elimu kwa upande huu wa mikopo haiweki kumbukumbu zake ipasavyo na kwa hili pia Mheshimiwa naomba nipate maelezo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ni kuwa kamati kifungu cha 3 ukurasa wa pili iliagiza wizara katika bajeti ya mwaka 2012/2013 kuhakikisha kuwa inaingiza ada ya shilingi 13 milioni ya watahiniwa wa Kidato cha Nne kwa lengo la kurahisishiwa ulipaji wa ada hizo kwa wakati. Katika utekelezaji wizara imekiri kuwa hilo ni kweli na kuwa hizo fedha kweli zinadaiwa. Lakini wizara ilisema kuwa ilipata jumla ya shilingi milioni moja na nusu katika mwaka wa fedha 2012/2013, na kwa sababu hiyo wakatumia walizotumia mpaka zikabakia shilingi 500 milioni ambazo walisema hizi zingeweza kulipwa lile deni la shilingi 433,490,000.

Sasa ukichukua hesabu sahihi zilivyo ni kuwa kama walikuwa na shilingi 500 milioni zimebakia na wakalipa deni hili hivyo wizara ilikuwa iwe na hakiba ya shilingi zisizopungua 65,000,510. Halafu kwa sababu watahiniwa hawa wataofanyiwa mtihani safari hii wanahitajika kulipwa shilingi 434,865,000 na wakati kule kuna hakiba ya shilingi 65,000,510 kama wangelilipa ingelikuwa sasa hivi kwa ujumla wizara hii ilikuwa idaiwe shilingi 369,355,000.

Lakini katika maelezo yake ni kuwa deni la mwaka jana la watahiniwa hawa na la mwaka huu itakuwa ni jumla ya shilingi 889,630,000 wakati ukifanya mahesabu yalivyo kwa kuzichukua zile shilingi 500 milioni ukalipa na kadhalika itakuwa haifikii. Kwa hivyo, sijui kwa kuwa sikuifahamu vizuri nataka nielezwe ilikuwaje mpaka deni liwe shilingi 789,630 na senti kidogo wakati tayari walikwishakuwa na *balance* ya shilingi 500 milioni.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, humu yametokea malalamiko au maelekezo kuhusu mambo yanayohusiana na usahihishaji wa mitihani kwa darasa la saba na vile vile kwa darasa la kumi kwa watahiniwa wa Zanzibar. Ilivyoonekana ni kuwa siku zote walimu wanaoishi katika Kisiwa cha Unguja huwa ni wengi kupita kiasi kuliko wale walimu wanaoishi katika Kisiwa cha Pemba ambao huchaguliwa kwa kusainisha mitihani hiyo. Sasa pamoja na kuwa ripoti imeeleza kuwa safari hii walimu watachukuliwa sawa mimi hilo kidogo nisingelikubali iwe hivyo. Kwa sababu najua kwa vyovyote Pemba skuli ni kidogo Unguja ni nyingi, walimu Pemba ni kidogo Unguja ni wengi. Mimi ushauri wangu tungelifuata uhalisia.

Mhe. Mwenyekiti, unajua katika Zanzibar tuna Mikoa mitano, Mikoa mitatu Iko Unguja na Mikoa miwili iko Pemba hiyo *ratio* ya mbili kwa tatu. Vile vile tuna Wilaya 10, sita ziko Unguja

na nne ziko Pemba ni sawa sawa na *ratio* ya *2 as 2/3*. Kwa hivyo, na hawa walimu angalau wangelichukuliwa katika *ratio* hiyo wasingelichukuliwa kama majimbo, majimbo tuliyonayo ni 50 lakini hayakwenda *ratio* 20 kwa 30 yanakwenda 18 kwa 32. Sasa ili kuondoa *confusion* tungelitizama mgao wetu wa asili na tukenda hivyo kwa kupunguza matatizo.

Halafu siku hizi kwa kuwatayarisha wanafunzi wetu waweze kusoma vizuri kuanzia daraza la kwanza kumeenea skuli nyingi za chekechea. Lakini walimu wanaofundisha chekechea kwa ninavyofahamu mimi kama sivyo naomba kupata maelekezo vyenginevyo ni kuwa baada ya skuli ya chekechea kujengwa tunachukua watoto au walimu waliokuwa tayari wameshasoma ambao hawakuajiriwa tunawapa ajira wanasomesha watoto. Sasa usomeshaji una mbinu zake na hasa watoto wadogo. Je, Mhe. Mwenyekiti, kama ushauri wangu utakuwa sawa serikali haioni kuwa umefika wakati hivi sasa wa kuwa na vyuo ambavyo vitatoa mafunzo si kwa walimu tu wa kusomesha skuli za serikali kuanzia *Form One* na kuendelea, lakini *specially* kwa kusomesha hawa watoto wetu wa chekechea ili waweze kutoka vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakisha dakika tano.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Dakika tano Mhe. Mwenyekiti, haya kwa sababu ni wa mwanzo katika siku zote naomba angalau saba. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya kwa katika ripoti ina uhaba mkubwa sana wa wafanyakazi na ilikuwa ina uhaba wa wafanyakazi 418, na walipeleka vibali kuomba ajira ya wafanyakazi ili kuondoa tatizo hili katika wizara inayohusika. Kutokana na taarifa zao kwanza walipata ajira ya wafanyakazi 49 halafu ikatokezea tena 192 na mwisho katika watu 816 katika kada kadhaa wakapata kuajiri watu 14 ambao hawa wote tukitizama ni wafanyakazi 255 katika pengo lao kuna upungufu wa wafanyakazi 163 hivi sasa hawako katika kada mbali mbali.

Mimi kwa sababu ya umuhimu wa wafanyakazi katika Wizara ya Afya wanaohudumia watu ambao hali yao ni wagonjwa kwa njia moja au nyengine, ningeliomba wizara husika ifanye kama inavyowezekana ili hawa wafanyakazi 163 ambao ni wapungufu na huku wengine wanachukua likizo huenda wakazidi waweze kuajiriwa ili huduma ya afya iweze kupatikana kwa ufanisi zaidi.

La mwisho kwa sababu ya wakati Mhe. Mwenyekiti, naingia Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Katika ripoti yake wizara hii ambayo naipenda sana kwa huduma zake ni kuwa kwanza iliagiziwa kuwa isimamie katika kuvihimiza vikundi vya ushirika hasa vile ambavyo vimo katika mchakato wa kufikia masharti ya kufaidika na msaada wa wahisani kama vile msaada wa Mfuko wa UN *Habitat* Pemba kuwa na maeneo rasmi ya kufanyia kazi zao ili kuweza kutambulika kiurahisi na washirika wa maendeleo.

Katika utekelezaji imeonesha kuwa hii kazi imefanywa na kwa wizara imesaidia mbinu na utaalamu na utaratibu mzuri wa kuomba na kupata mikopo mbalimbali ikiwemo ya UN *Habitat* na hasa Kisiwani Pemba. Mimi nilitaka nijue kwa nini iwe hasa Kisiwani Pemba isiwe Unguja na Pemba sawa sawa.

Halafu kwa mikopo ya UN *Habitat* kwa waliofanikiwa kupata msaada ni vikundi sita, vinne kutoka Pemba na viwili kutoka Unguja ni kwa sababu Unguja wameshapata misaada sana au vipi mpaka Pemba wawe wengi naomba maelezo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa kamati imebaini tatizo la kukosa ofisi maalum za kuendesha shughuli za vikundi vingi vya ushirika Pemba vikiwemo vikundi vya *Youth Center* Mbuzini na Selem *Women* Wete. Lakini katika maelezo ya wizara ilivyojitahidi kutafuta ni kuwa wizara imechukua hatua ya kuishajihisha na kuvisaidia vikundi vya *Youth Center* Mbuzini, Chake Chake na Selem *Women* Wete na Kikundi hicho cha Selem tayari wamepata jengo na wameshahamia katika jengo hilo na shuguli katika vikundi vyengine zinaendelea kuwa za kudumu.

Sasa nauliza hili jengo ni lao wenyewe wamelijenga, wamelinunua, wameazimwa kwa muda gani au kama wamekodi ni kwa kiasi gani kwa mwaka na pesa za kulipia zinatoka wapi.

La mwisho kwa sababu ya wakati na mengine nitayaacha Mhe. Mwenyekiti. Ukiangalia Wizara hii ya Ustawi wa Jamii katika taarifa ya ukurasa wa tatu hii wizara inahusika sana na naipongeza kwa kuwasaidia watu wetu katika vikundi, kuwaelimisha, kuwakusanya pamoja na kutoa misaada kwa vikundi mbali mbali vya ushirika na kadhalika, au na vikundi vyengine vinavyohusiana na hayo.

Lakini tuna Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika hii nayo kazi yake kubwa ni shughuli hiyo hiyo ya vikundi inayofanywa na Wizara hii ya Ustawi wa Jamii. Sasa wakati mimi nilikuwa ni mjumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari; mara zote tulikuwa tunakagua vikundi ambavyo vinashughulikiwa na Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na hatukuwahi kukagua kikundi kwa niaba ya wizara nyengine kama nilivyoeleza. Mimi hapa swali langu nataka kuelewa vikundi ni vile vile na vyote kweli vinahitaji msaada na wakati kuna wizara hii inafanya na wizara hii inafanya kwa vikundi vile vile. Je, hatuoni kuwa ipo haja ya wizara husika hasa baada ya wenyewe kukubaliana wakawa ndio wanao-*play role* ya kushughulikia vikundi hivi ili kuondoa huo utatanishi wa kuwa wizara hii inatoa na hii inatoa.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, na kwa sababu ya wakati nataka nishukuru naomba kupumzika.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia machache katika ripoti hizi za kamati. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati na kuwapongeza Mawaziri wote ambao walituwasilishia ripoti zao kwa uwasilishaji mzuri kabisa.

Lakini pia nimshukuru Mwenyekiti ambaye naye amewasilisha ripoti yake vizuri, ninamshukuru na ninampongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wenzangu wengi ambao wamesimama wameweza kuchangia vizuri lakini na mimi nikasema angalau niweze kutoa mchango wangu japo mdogo.

Kwanza kabisa ninataka nianze na mchango wangu katika Wizara hii ya Elimu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninataka kuchangia kuhusu hili deni ambalo limekopeshwa wanafunzi. Nilitaka kujua tu jee serikali inafuatilia vipi deni hili kwa umakini ili kuweza wanafunzi hawa kulipa na hatimaye fedha hizi kwa kuwa tunajua wapo wanafunzi wengi ambao wanapenda kujiendeleza katika elimu hii ya juu ili fedha hizi ziweze kuwasaidia wengine. Nilitaka kujua hilo kwa sababu bila ya wizara wenyewe kufuatilia kwa umakini wadau wengine huwa wanajitia pambani ya kuweza kulipa madeni yao.

Mhe. Mwenyekiti, pia niendelee kwa Wizara hii ya Elimu, kwa kweli imo katika taratibu za uajiri wa walimu lakini mimi tu nilitaka niwasisitize kwa sababu kuna wanafunzi ambao wameshasoma kwa muda mrefu tangu 2007, wapo hawa na bado wizara naona haijawazingatia katika uajiri wao ili wakaweza kuwaajiri hawa ambao wapo katika muda mrefu wanaweza wakapoteza zile sifa kwa sababu watakuwa wameshakaa sana na hata kile ambacho walichokisoma wanaweza wakakisahau. Ningeomba serikali iweze kuwazingatia walimu hawa ambao kwa muda mrefu na bado hawajapata uajiri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije kwenye suala zima kwanza niipongeze serikali kwa ujenzi wa skuli zile za sekondari ambazo ni za kisasa na ni nzuri zenye mvuto kabisa lakini niseme kwamba skuli zile tunaweza tukapoteza ule mvuto kama hatukuziwekea uzio, kwa sababu hivi sasa inaonekana wachungaji wa mifugo mbali mbali wanavamia skuli zetu zile na kukosa kuzithamini kama vile ambavyo tumetakiwa tuzithamini ili zibaki katika mfumo ule ule wa kuwa nzuri kama zinavyoonekana. Mhe. Mwenyekiti, niombe sana serikali kuzijengea skuli hizi uzio basi zitaendelea kuonekana katika hali nzuri. Kwa hivyo tuzingatie hilo.

Jengine nilitaka kuzungumzia kuhusu maslahi ya walimu, wizara pia ijitahidi pamoja na jitihada zinazofanya kwa sababu jitihada zipo na zinaonekana lakini pia kuwajali walimu kimaslahi, kwa sababu kazi wanazofanya ni ngumu kidogo. Kwa hivyo pia waongezewe na marupurupu yao na waweze kulipwa kwa wakati ili isichukue muda mrefu waweze kujikimu kimahitaji.
Lakini kuna suala zima ambalo wamelizungumza wenzangu wengi ambao wamesimama ni kuhusu hati miliki ambazo majengo yetu ya serikali ukiacha za Wizara ya Elimu lakini majengo mengi ya serikali hayana hati miliki. Hili litakuwa linarejesha nyuma na tutakuwa tunafanya uzembe ambao haulingani kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niseme sote tumeshuhudia wimbi kubwa la kufeli kwa watoto wetu ambalo jambo hili lilituhuzunisha sana wazazi pia na kuwakatisha tamaa watoto wetu. Pia niulize serikali juu ya jambo hili imejipanga vipi ili kuweza kuona basi tunaondokana na matatizo haya ambayo yanafanya kuwakatisha tamaa watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka katika wizara hiyo niende katika Wizara ya Afya. Pia kabisa nichukue kabisa kumpongeza Mhe.Waziri na watendaji kwa jitihada zao kubwa ambazo wanazichukua. Ninaipongeza wizara kwanza kwa kuboresha zile huduma za vijijini katika hospitali zetu za wilaya. Kufanya hivi serikali ambapo itajikita katika kuboresha hospitali hizi basi ile dhana ambazo tunahitajia kwamba tunaipate kuwa hospitali kuu ya Mnazi Mmoja iwe ni ya Hospitali ya Rufaa basi inaweza ikapatikana, kwa sababu wananchi wengi wa vijijini wataweza kupata huduma zile pale pale walipo na tena huduma za kuridhisha. Kwa hivyo bado iendelee na juhudi zake hizi za kuhakikisha inaboresha zile huduma za vijijini.

Nitoe pongezi hizi kwa kupitia hospitali yangu ya Wilaya ya Kaskazini A yaani Kivunge kwa vifaa mbali mbali ambavyo vimepatikana pale vinaweza kidogo kukidhi haja kwa matatizo yakitokea hapa na pale basi tunaweza kujikimu na kuacha kukimbilia hospitali ya Mnazi Mmoja.

Lakini pia niwapongeze madaktari mahiri pale ambao wanatuhudumia vizuri tu na wao, nichukue fursa hii kuwapongeza kwa kazi zao nzuri. Lakini Mhe. Waziri bado tuna tatizo hili la posho hizi za call bado kuna madaktari wengine hawajapata kabisa, inafika hata miezi saba hawajaweza kupata hii call allowance. Kwa hivyo nikuombe Mhe. Waziri uweze unapotoa huduma hii basi waweze kupata madaktari wetu wote.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nije katika Wizara hii hii ya Afya lakini kuna siku niliwahi kutembelea Pemba kwenye Hospitali ya Chake-Chake na nilileta swali langu siku moja hapa baada ya kuzikuta zile huduma pale hazipo vizuri. Nilikwenda katika huduma ya kujifungulia mama waja wazito na nikakuta vitanda haviridhishi ni vibovu ambavyo vinaweza vikahatarisha mama anayajifungua na mtoto wake.

Nililileta swali langu hapa nikajua kwa kulileta hapa serikalini basi serikali inaweza ikafanya mipango mizuri ya kuboresha huduma ile. Nikiuliza Mhe. Waziri baada tangu pale tulipozungumza suala hili ni hatua gani ambayo imechukuliwa kuweza kupatiwa huduma bora akinamama pale katika kujifungua. Pia kulikuwa na tatizo la incubator ambayo ya kuhifadhia wale watoto ambao wanaozaliwa chini ya umri wa miezi tisa, kwa sababu watoto wale huwa wanahitaji uangalifu mzuri. Tukakuta huduma ile hapana, jee na huduma hii ikoje mpaka hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende haraka haraka kwa sababu sipendi kumega muda mwingi ili na wenzangu waweze kupata fursa ya kuchangia, niende katika Wizara ya Wanawake na Watoto ambayo hii ndio wizara yetu tunaitegemea sana wanawake na watoto kwa mambo yetu.

Kwanza nikija katika wizara hii, nianze kuzungumzia jinsi ya udhalilishaji wa watoto kijinsia. Mhe. Mwenyekiti, hili wimbi ni kubwa sana na linatukatisha tamaa na kututia unyonge hasa wazazi. Kwa sababu kuna kesi ambazo zinaambiwa zina utata labda hazikupatiwa ushahidi unaokamilika lakini kuna kesi nyengine huwa zinaonekana zina ushahidi wa kutosha lakini sijui ni kwa nini haziwezi kuchukuliwa hatua ili ikaonesha mfano wa kuwa wale waliofanya tendo hili wamechukuliwa hatua kali na wale ambao hawajalitenda wakajizujia kulitenda ili tukanusurika katika hali hii mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika mafunzo. Kweli wizara inajitahidi kutupa mafunzo mbali mbali ya vikundi vya ushirika. Hili nalo niipongeze sana wizara kwa kazi zao na juhudi zao ambazo wanazochukua, lakini mimi nilitaka kujua tu katika mafunzo haya ambayo tunapata, kuna tathmini gani ambayo imefanywa ili tukaweza kujua ni hatua gani ya maendeleo ambayo tumeweza kuipiga kupitia mafunzo haya au ni changamoto gani zipo baada ya kupata mafunzo haya tukaweza kuzijua ili tukajua tujikwamue wapi pale ambapo tumekosea.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuvipongeza sana sana vikundi vya ushirika vyote ambavyo vinajitahidi katika kujikwamua na kujiletea mafanikio katika familia zao. Mhe.

Mwenyekiti, nikipongeze kikundi kimoja kipo Tunguu ambacho hiki kinajishirikisha sana na ukulima wa mboga mboga na matunda yale tunayofanyia juice. Kikundi hiki kusema kweli kinatoa mfano na mwanga mzuri. Kwa hivyo ninakipongeza sana na wizara bado niombe iendelee kutokiachia mkono kwa hatua waliokwisha kufika, ina maana wanakwenda vizuri basi wasije wakapoteza mwelekeo.

Lakini pia kwa wivu wa maendeleo niweze kumuomba Mhe. Waziri kuwapatia wana vikundi wangu wa Mkoa wa Kaskazini elimu hii ya upandaji wa haya matunda ya juice ili na wao waweze kuzalisha, hatimaye tuweze kuwa na mashamba haya mengi tunaweza tukapata Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko akaweza kututia masoko ili tukaweza na sisi kuwa na bidhaa za kwenda kuuza nje au pia tunaweza tukashawishika tukaona tayari bidhaa yetu imeshakuwa nyingi basi na sisi tukaweza kuanzisha viwanda hapa hapa vya juice na nini tukaweza kuzalisha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika 5 za kumalizia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Aah! mimi ninasema sichukui muda kumbe. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo nilitaka pia kujua kuna ufunguzi ule wa soko la *Sunday Market* ambalo, kwa kweli mimi nilitaka kujua tangu kufunguliwa soko lile ni hatua gani ambayo tumeweza kuifikia au tunafaidika vipi ili basi tuweze kuwa na mvuto wa kufanya biashara zetu vizuri na tuweze kufaidika akinamama.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninawapongeza sana mawaziri wetu basi waendelee tu na juhudi hizi ipo siku Mwenyezi Mungu atatufikisha katika mafanikio yaliyokuwa makubwa, hakuna lisilowezekana.

Baada ya hayo ninashukuru na ninaunga mkono ripoti za kamati kwa asilimia mia. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nishukuru kupata fursa hii kuweza kuchangia asubuhi hii taarifa za Kamati za Ustawi wa Jamii pamoja na Wizara ya Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijachangia chochote kwanza naomba nichukue muda wako mchache kama sekunde moja mbili tatu hivi nitoe pongezi za shukurani kwa mchezaji mwenzetu kapteni wa timu ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Gavu kupitia vyombo vya habari niliona jana kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia jengo la Dar Young African na Mhe. Ridhwani Kikwete. Mhe. Mwenyekiti, tunamshukuru Mhe. Ridhwani Kikwete kwa kumuona mwakilishi wa Jimbo la Chwaka kumpa fursa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi zangu hizo niende katika Wizara ya Elimu, niishukuru serikali, nimshukuru waziri kwa jitihada walizozionesha katika kusaidia kwa namna moja au nyengine kuboresha wizara yetu hii ya elimu. Na zaidi naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa wizara hii ni katika masuala mazima ya ujenzi wa skuli za sekondari.

Mhe. Mwenyekiti, kilio kilikuwa kikubwa, wanafunzi walikuwa wakihangaika nafasi zilikuwa ni finyu na hatimaye serikali imeona kilio kupitia wafadhili wetu na kuweza kujenga skuli za

sekondari zenye ubora na zilizokuwa makini na tunatarajia kwamba baada ya muda mfupi kadhia ya watoto kwenda masafa marefu itaweza kuondoka mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Wizara ya Elimu pia naomba nitoe mchango wangu katika eneo zima la Skuli ya Kisiwandui. Mhe. Mwenyekiti, ile skuli ina watoto wenye akili tahira au inatolewa mafunzo ya elimu mjumuisho. Na kama miongoni mwetu kama mjumbe atapata fursa ya kwenda kuangalia ile skuli na kuwaona wale wanafunzi zile hali zao, basi tusingefikia mpaka hadi hii leo Mhe. Mwenyekiti, ikawa tunapiga kelele namna ya kuimaliza ile skuli kuweza kuwaweka katika mazingira mazuri na bora.

Mhe. Mwenyekiti, skuli ile ina watoto wa aina mbali mbali. Skuli ile muna vipofu, walemavu wa miguu ambao hawawezi kutembea kwa miguu, viziwi, akili zao zilizokuwa zina matatizo. Sasa mazingira yake kwa kweli hayaridhishi. Ahadi mbali mbali zimeshatolewa katika skuli ile na bado hayajatekelezeka.

Mazingira yanakuwa magumu zaidi hususan wakati wa mvua. Sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Elimu apite akaangalie ile kadhia ili aweze kuwasaidia wale watoto wenye ulemavu wa skuli ile, ili na wao basi wajihisi kama ni sehemu ya viumbe ambao wanastahiki kupata haki zao za msingi katika kutafuta elimu.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika skuli hiyo namuombe Mhe. Waziri basi atakapokwenda basi atupie jicho la huruma kwa wale walimu ambao wanawasomesha wale watoto. Kwa kweli sio kama wanawasomesha wanawalea kabisa, kwa sababu kukaa na mtoto mwenye akili tahira ukaweza kumchunga na kukaa naye kwa muda wote na kuweza kumpa elimu na akafahamu, basi imani yangu kwamba mwalimu huyo anafanya kazi mara mbili; anafanya kazi katika kutoa elimu lakini wakati huo huo anafanya kazi ya ulezi kwa ile hali ya watoto wetu waliyokuwa nayo.
Lakini pia niombe watoto wale wanakabiliwa na vitendea kazi katika kupata elimu yao, kwa sababu mtu ambaye aliyekuwa haoni basi anakuwa na karatasi zake maalum za kuweza kupata mafunzo yale na ni ufinyu wa vitu ambavyo walivyokuwa navyo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa nitoe wito wangu kwa Mhe. Waziri kwa kweli kuna haja ya kuiangalia skuli ile na nyenginezo ambazo zina watoto wenye akili mjumuisho ili kuweza kuwasaidia watoto wetu na wao kuweza kupata elimu ya kuweza kuwasaidia hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la Wizara ya Elimu pia katika document hii ya taarifa ya kamati, nimejitahidi kuangalia lakini kuna vitu vinanipa mashaka. Hapa katika suala la bodi ya mkopo wa elimu ya juu. Mhe. Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa bodi yetu ya mkopo kwamba safari hii kilio sio kikubwa, wamejitahidi na hakuna ambaye kwa kweli ameweza kulalamika kwa namna moja au nyengine katika utoaji wa mikopo katika bodi yetu pamoja na ufinyu wa fedha ya bajeti ambayo inaikabili, ni imani yangu kwamba wizara safari hii Wizara ya Fedha itajitahidi kuweza kuboresha hii taasisi ili vijana wetu kupata nafasi.

Kitu ambacho kinachonipa mashaka na sijakiona ni suala zima la wanafunzi ambao wanapata mikopo, wale ambao wanaosoma nje ya nchi na baadae wanatoa maamuzi ya kutokurejea nchini wana-disappear katika kutafuta maisha yao katika hali nyengine. Sasa sijapata kuona taarifa ya marejesho kwa wale wadhamini kwa zile hatua ambazo zimechukuliwa, ni kuweza kujua ni

wanafunzi wangapi wame-disappear na wale wadhamini wao wamechukuliwa hatua gani ili kuona yale marejesho tunatarajia kuweza kupata wenziwao basi yanaweza kupata ufanisi na wenziwao wanafaidika.

Sasa Mhe. Waziri atakapokuja kutoa taarifa zake hapa ninafikiri atanisaidia kunipa maelekezo kwamba kuna wanafunzi idadi gani na njia gani wamezitumia kwa kupitia wadhamini wao, kuweza kuchukua hatua za kisheria ili kuweza kulipa mikopo ile.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika Wizara ya Elimu basi pana tatizo ambalo limejitokeza linaleta usumbufu katika maeneo mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri safari hii niliweza kushiriki katika shughuli zetu za sherehe za mapinduzi katika uzinduzi na uwekaji wa majiwe ya msingi kwenye maeneo mbali mbali.

Kwa bahati nilifika Moga kwenye Jimbo la Chaani na pale niliweka jiwe la msingi. Wizara iliahidi kulijenga jengo lile katika hatua iliyobakia kwa haraka, na walikuwa na sababu za msingi kusema hivyo. Kwa sababu watoto wa pale hivi sasa wanasoma katika jengo la chama na kwa kweli hilo jengo lenyewe mazingira yake pia hayaridhishi. Sasa hiyo ni sehemu moja tu.
Sasa niseme tu kwamba haya majengo yapo mengi ambayo yanahitaji kumalizwa kwa haraka katika zile hatua ambazo Wawakilishi na Wabunge wamejitahidi. Sasa niiombe wizara basi ifanye jitihada ya kuweza kuyamaliza haya majengo ili kuwaondoshea usumbufu watoto wetu katika maeneo mbali mbali.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninaondoka kwenye Wizara ya Elimu na ninakwenda katika Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada nzuri ambazo zinaonekana katika Wizara ya Afya, kwa kweli panapo mazuri na mapungufu hayakosi.

Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Jussa alipokuwa akichangia hapa alimsifu sana Mhe. Juma Duni kwa wakati alipokuwa katika chama chake kama Naibu Katibu Mkuu, alivyokuwa na umahiri katika suala zima la kusimamia chama chake lakini alikuwa anashangazwa na namna hali halisi ya usimamizi wa shughuli zake katika Wizara ya Afya.

Na yeye zaidi aliegemea katika kutoa mashaka yake kwamba watendaji wanamuangusha. Mimi niseme kwamba bado lawama tutamtupia Mhe. Waziri kwa sababu yeye ndiye tunayemkabili ndani ya Baraza letu. Kama kuna watendaji wenye matatizo basi inaonekana bado yeye usimamizi wake haujawa imara.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mifano mingi ya wenzetu mawaziri Tanzania Bara jinsi wanavyochukua hatua kwa kurugenzi zao pale ambapo wanafanya matokeo yaliyokuwa hayastahiki au hayaridhishi katika hizi taasisi. Kwa hivyo bado wizara kama itakuwa na mapungufu ya hapa na pale, bado Mhe. Waziri yeye ndiye ndiye msimamizi mkuu, ndio mtu ambaye tunamtegemea asimamia shughuli zake katika wizara ile, ni mtu ambaye sisi kama wawakilishi basi tunakuja kumsaidia katika changamoto mbali mbali katika kuisimamia serikali katika hiyo taasisi.

Sasa katika hiyo hiyo Wizara ya Afya Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia kwenye bajeti yangu mwaka jana na hili sijaliona katika kitabu chao, kamati katika kuelezea nilikuwa nikizungumzia suala zima watu ambao wanaokwenda kutizama wagonjwa Hospitali Kuu ya

Mnazi Mmoja, na nikatoa kilio kikubwa hususan kwa mama zetu ambao wanakwenda pale kwa suala zima la kupeleka wajawazito.

Unakuwa huna hata sehemu ya kupita katika lile eneo, watu wanalala mpaka kwenye ngazi, jua watu wanakaa kwenye miti, watu wanateseka kusubiri muda wa kwenda kutizama wagonjwa au kuangalia ile hali halisi ya wagonjwa wao ndani. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu unajua suala la wazazi wewe ni mwanamke hakuna mtu ambaye akili yake inatulia kama hajamuona mwanawe au mzazi wake ameshajifungua salama usalimin.

Nimepewa taarifa kwamba kuna mipango ya kujenga banda kwenye bustani yetu ya Victoria Garden. Sasa nilitaka kujua ule utaratibu umefikia wapi na nini kinachoendelea katika suala zima la hiyo hali. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapa hapa tu katika Wizara ya Afya basi niseme hilo kwamba hilo litakuja baadae lakini kuna haja ya kuitaka serikali yetu, ninasema tutaendelea kuwapa lawama watendaji, madaktari na sekta mbali mbali za kijamii kama Wizara ya Fedha haijaamua kwa makusudi kuangalia bajeti za taasisi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaamini serikali hii inapoamua inaweza pamoja na kwamba tunaamua mpaka tukumbane na matatizo mbali mbali. Tuliamua kutafuta namna ya kuweza kupata fedha ya kuondosha kero za meli. Tumeondosha mambo mengi, tumepunguza mambo mengi katika taasisi zetu. Ni imani yangu kwamba kama kulipunguza kule basi na mwaka huu kupitia bajeti yetu ninafikiri kuna haja ya kima kile ambacho tulichokusanya mwaka uliopita basi tukisukume katika taasisi zetu hizi za Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya ili kuweza kuondosha manung'uniko na kuweza kukidhi zile bajeti zinavyohitajika. Ni kweli hali hairidhishi, hali sio nzuri na hatutoweza kupata ufanisi pale mtu anapoomba bajeti ya asilimia 100 akapewa asilimia 20.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya kujali muda wako ningeomba nimalizie katika Wizara ya Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, mimi bado ninapata mashaka na wizara hii na kigugumizi namna ya utekelezaji wa shughuli zao za kila siku katika maeneo mawili. Bado nasisitiza kwamba hii wizara kuna haja ya kuangaliwa kwa makini.

Sijui sababu ya ubinafsi au sababu nyengine yoyote katika maeneo hasa ya utoaji wa mikopo kwa akinamama na vijana. Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba ninukuu kidogo, kwenye ukurasa wa 100, "Wizara imewahamasisha wanawake 168 kujiunga na vikundi vya uzalishaji ambapo kati ya hao 38 ya Shehia ya Bumbwini Msufini, 43 ya Shehia ya Zingwezingwe Wilaya ya Kaskazini B. Wilaya ya Mjini ni Mwembeshauri Shehia 24 na Mchangani Shehia 32".

Mhe. Mwenyekiti, kama utaangalia kama huu ni uhalisia wenyewe kwa Wilaya ya Mjini nzima kuzichukua Shehia mbili bado ninahisi hakujawa na uwiano katika masuala mazima ya kusaidia vikundi vya akinamama. Mhe. Mwenyekiti, katika Wilaya yetu tuna Shehia nyingi lakini Shehia zilizoainishwa hapa ni 2 na Shehia hizi ni idadi waliosaidiwa ni kubwa 32 kwa 24, lakini hakuna Shehia nyengine yoyote ambayo imeweza kusaidiwa.

Sasa lipo wapi tatizo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hebu tusaidie tatizo watu hawahamasiki au maafisa wao wanakuwa na matatizo ya kuchagua zile Shehia ambazo wanahisi zinakuwa zina-benefit na wao. Lakini hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, kuna kifungu kinasema, wizara imefanya

ufuatiliaji katika vikundi 14 kwenye Wilaya ya Kaskazini A, Mjini, Kusini na Kati. Aidha vikundi 7 vya Wilaya ya Kati vimefuatiliwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika vikundi 7 vya Wilaya ya 7 ukiangalia, kuna 3 Ukongoroni na 4 vya Charawe. Hili ni jimbo moja na hapa imezungumzwa ni Wilaya ya Kati. Sasa inabaki kujiuliza haya majimbo ya Makunduchi, Muyuni, wao hawastahiki kufuatiliwa kupata hizi haki za msingi ambazo wizara yetu imeamua kutusaidia.

Sasa mimi Mhe. Waziri atakapokuja hapa anisaidie namna ambavyo maafisa wake wanafanya hii kazi ya kuratibu katika kuvisaidia vikundi vyetu kwenye maeneo mbali mbali.

Lakini kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, pia ninapata hofu yangu katika suala zima la vijana wetu katika kupewa mikopo. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 98, katika kipindi cha Oktoba/Disemba hakuna mkopo mpya uliotolewa tangu kuanza kwa mpango wa mkopo kwa vijana. Jumla ya shilingi mia moja tisini na sita milioni laki tano na hamsini elfu zimetolewa kwa vikundi 78 Unguja na Pemba. Hali ya marejesho ya mkopo ni nzuri kidogo ambapo karibu asilimia 95 ya vijana waliokopa wanarejesha mikopo kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ninataka Mhe. Waziri anisaidie aje anitosheleze, hizi mia moja na tisini na sita laki tano na hamsini kwa vikundi 58 aje kunisaidia, ni vikundi vya maeneo gani. Kwa sababu ninasema bado ninapata mashaka na taasisi kwamba wanatoa fedha au wanatoa mikopo kwa kuangalia vile ambavyo wao wanaona lakini sio kwa kujitosheleza au kwa kuangalia jiografia ya nchi yetu au uwiano wa kimajimbo katika kuwasaidia vijana wetu. Hii italeta mashaka kuja kuona baadae kama Wilaya fulani zina upendeleo, Wilaya fulani hazipati upendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye eneo hili la vijana, fedha hizi Mhe. Waziri atakapokuja basi aje kunisaidia maeneo yale ambayo wamefanya ugavi na hali halisi vile ambavyo wamefanya.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyozungumza mwanzo kwamba ninajali muda zaidi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani ninaunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa bahati mbaya sana au kwa masikitiko makubwa leo inatubidi tumalize wizara zetu hizi tatu. Kwa hivyo sasa hapa tukiongeza zaidi muda tutakuta kwamba tutashindwa kumaliza.

Mchangiaji wa mwisho ambaye atachangia atakuwa ni Mhe. Rufai. Ningewaomba sana wale wajumbe wote ambao wameleta majina yao wangefanya kwa maandishi ili wakafikisha wanaohusika.

Naomba sana tukubaliane hili ili tumalize leo mchana na jioni tuanze na wizara nyengine. Ninawashukuru.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kuipata hii nafasi nikawa ni mtu wa mwisho kutoa maoni yangu katika Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuwa mzima asubuhi hii na mimi nikapata nafasi ya kutoa maoni yangu machache. Kwanza niipongeze Kamati kwa uoni wao waliouona katika wizara zetu hizi tatu na wakaweza kutufikishia mbele yako Mhe. Mwenyekiti, na sisi tukaweza kupata uwezo wa kutoa maoni yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda moja kwa moja kwenye Wizara ya Afya, katika programu ya kupambana na malaria. Mhe. Mwenyekiti, hatuna budi hapa kuipongeza serikali kwa utafiti wake wa kuweza kupambana na suala zima la malaria, kwa kiasi fulani imefanya jukumu kubwa na juhudi kubwa kwa kupambana na tatizo sugu la malaria, ambalo linasumbua sana wakaazi wa visiwa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, juu ya hivyo bado mapambano haya yanaendelea na baadhi ya wananchi wetu bado wanaathirika na maradhi makubwa haya ya malaria. Ni kweli kwamba jitihada serikali imechukua na imefanya uchunguzi wa dawa mbali mbali, na watu kupitia sekta mbali mbali wameangaliwa na baadhi yao ikaonekana kuwa kuna asilimia 0.2 ya watu hao waliofanyiwa uchunguzi wa malaria. Lakini bado tunaamini kwamba malaria nchini yapo na bado tunaiomba serikali iendelee kuyatafuta yale makaazi kabisa ya mbu huyu, ambaye anasababisha matatizo ya homa mbali mbali kwa wananchi wetu, ili kuhakikisha maradhi haya yametokomezwa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, bado niseme kuna huduma za afya vijijini ambazo bado hazijakaa sawa, kuna baadhi ya vituo vyetu havina ubora, havina madaktari na linakuwa ni tatizo sugu wananchi wetu kufika pale na wakakuta kwamba hakuna utibabu wowote unaopatikana katika vituo hivyo.

Kwa mfano, tunavyo vituo mbali mbali hufika karibu wiki hapana daktari na vituo vingine havina muhudumu pia hapatikani pengine kapangiwa semina au shughuli nyengine zozote zile za kiutendaji. Kwa hivyo, tunaiomba sana Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, suala la kuajiriwa madaktari lifanyiwe haraka ili huduma za wagonjwa wetu waweze kuzipata katika vile vituo ambavyo viko karibu na wao. Limekuwa ni tatizo sugu vituo vyetu vingi vya afya havina madaktari.

Pia Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima la tatizo la madeni ya umeme katika vituo vyetu vya afya. Jitihada za Kamati suala hili waliligundua. Ni kweli kabisa vituo vingi vya afya vina tatizo zima la ulipaji wa umeme hasa vituo vya kule nyumbani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, vituo hivi kwanza walikuwa wanakwenda na mita hizi za kawaida, ikawa Wizara inajilimbikizia madeni ya umeme na huku ikawa wizara ina mpango wa kulipa kwa mwezi tu shilingi 80,000, lakini kutokana na madeni ya nyuma mpaka kuwekewa mita hizi za TUKUZA ikabidi vituo vingi vikose huduma hii ya umeme. Kwa hivyo, kuna baadhi ya vituo vilifikia madeni ya shilingi 500,000 na vituo vyengine mpaka zaidi ya milioni moja. Kwa hivyo, ikawa kuviendeleza vile vituo ikawa ni tatizo sugu kwa kipindi hicho. Lakini tunashukuru Wizara ilichukua jitihada baadhi ya vituo kuendeleza kulipa, lakini bado hili tatizo lipo.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sana Wajumbe wenzetu tutakapoingia kwenye bajeti ya mara hii ili tatizo tulione kwamba lipo na itabidi wizara hii tuipe kipaumbele ili iweze kutoa huduma ya umeme, ili vituo vyetu viweze kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile tuna tatizo la madaktari wanaoajiriwa kwenda Pemba. Mhe. Mwenyekiti, tumeshaona kwamba vijana wetu wanaopata taaluma na ikawa baadhi yao wanatoka hapa Unguja kwenda Pemba, basi kule Pemba hawaishi wanarudi, na wizara imeshawapangia kazi Pemba. Sasa kurudi kwa vijana wetu hawa bado ni tatizo la wagonjwa kutopata matibabu. Imeshaonekana wanaporudi hakuna vikwazo vya aina yoyote, wanarudi na wakirudi wanafanya ajira katika maeneo mengine ya vituo hivi hivi vya serikali. Kwa nini serikali ikawa hawaweki mkakati kwa vijana hawa waliowaajiri kutoka Unguja kwenda Pemba, ili wakaweza kufanya kazi kule Pemba, inafikia madaktari hawa kurudi huku Unguja na wakaendelea kufanya kazi huku Unguja.

Kwa hivyo, bado tunaitaka wizara kwamba yule inayemuajiri kwa afya Pemba, basi wahakikishe kwamba wamepata eneo ambalo ni zuri, na anapata nyumba ya kuishi, japokuwa tutashirikiana na sisi Wawakilishi tuliopo katika maeneo yale ili kuhakikisha daktari wetu huyu amepata pahala pazuri pa kuishi na kuweza kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo yale. Lakini limekuwa ni tatizo vijana wanaajiriwa Pemba, lakini hatima yake wanarejea tena hapa Unguja. Kwa hivyo, tunaiomba sana wizara ihakikishe kwamba waajiri wao wanapokwenda kule Pemba basi wanafikia maeneo ambayo wanaweza kuishi.

Mhe. Mwenyekiti, pia kwa kipindi kirefu tuna ukosefu wa madawa, hospitali nyingi za vijijini mgao huu wa madawa umekuwa na matatizo. Kuna taarifa mbali mbali ambazo sina uhakika nazo, lakini tunaambiwa kuna matatizo ya haya madawa, kulitokea hitilafu fulani, zilikuwa zinaletwa dawa, lakini baadhi ya dawa ni maboksi matupu hakuna dawa. Kwa hivyo, utaratibu wa kuletwa dawa ukawa unatiliwa mashaka. Kwa hivyo, wizara ikawa ina mipango mingine. Lakini kwa kweli imekuwa ni tatizo sugu kwa wananchi wetu kutopata matibabu kwa kipindi kirefu, dawa hazichukui hata wiki ni katikati ya mwezi. Kwa hivyo, unakuta kituo hicho hakitoi tena matibabu kwa wananchi. Kwa hivyo, tunaiomba wizara itueleze tatizo hili limekuwaje na limefikia vipi mpaka hatima yake wananchi wetu wakakosa matibabu ya kila mwezi katika maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kujali muda wako naomba sasa niingie Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 75, kuna maagizo matatu ya Kamati waliyoyaona katika wizara hii ya elimu.

Kwanza Kamati iliiagiza wizara katika bajeti ya mwaka 2012/2013 wahakikishe kwamba waainishe ada ya shilingi milioni 300 za watahiniwa wa kidato cha nne kwa lengo la kurahisisha ulipaji wa ada hizo kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, hapa pana deni kubwa wizara ya elimu ambayo inadaiwa. Hivi sasa tumo katika maandalizi ya vijana wetu wengine wa *form four* na hivi sasa tumo katika maandalizi ya vijana wetu wengine wa *form four* ambao wanatarajiwa kufanya mtihani. Kwa hivyo, agizo hili ningeomba sana Wizara hichi kitabu kukidurusu, wakayaona haya matatizo ambayo yapo kuyafanyia kazi ili mitihani itakapofika, kusijekuwa na sababu kwa baadhi ya wanafunzi wetu wakajakosa kufanya mitihani kwa sababu wizara inadaiwa. Tunaiomba sana Wizara ilisimamie hili na wahakikishe tatizo hili wamelitekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, Tunatarajia kwamba bajeti ya mwaka huu wizara italeta maagizo yake mazuri ili na sisi Wajumbe tuweze kuyatilia nguvu ili kuhakikisha kwamba vijana wetu hawa wanawezeshwa kuweza kufanya mitihani yao. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kuna agizo kwa jengo la maendeleo la kutumiwa na ofisi ya bodi ya upimaji na tathmini, inayotolewa taarifa ya Mamlaka ya Mji Mkongwe kwamba haifai kwa ajili ya matumizi ya ofisi kutokana na hali mbaya ya ubovu wa zaidi ya miaka 10.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatari kwamba Mji Mkongwe umeshatoa taarifa karibu miaka 10, jengo hili wanaloishi watu hawa wa tathmini ya mitihani kwamba jengo hili halifai kuishi watu, miaka 10 imeshapita bado watu hawa wamo kwenye jengo hilo. Litakalokuja kutokea tutakuja kumlaumu nani. Kwa hivyo, ni vyema wizara kuliona hili na kulisimamia, na yale madai yao waliyoyapeleka katika Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kuhakikisha limesimamiwa ili kuwanusuru watendaji wetu hawa, kutoka katika jengo hilo na kuhamia katika jengo hilo lililokuwa la Bima ya zamani. Hilo ni agizo la pili, naiomba sana Wizara kulisimamia hili.

Agizo la tatu Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufuatilia kwa karibu matatizo yanayoikabili Skuli ya Sekondari ya Ufundi ya Kengeja, yakiwemo, hali ya mfumo wa maji machafu, upungufu wa walimu wa ufundi katika idara ya umeme, uhaba wa mabweni pamoja na huduma za afya.

Mhe. Mwenyekiti, maagizo haya ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Rufai Said, naomba ujumuishe umalize.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante. Mhe. Mwenyekiti, hii skuli ni ya serikali, sasa ikiwa skuli ni ya serikali wanafunzi wanaokwenda pale ni watoto wetu, lakini hali mbaya ya maji machafu, hakuna asiyefahamu maji machafu madhara yake, maambukizi mengi ya maradhi ya tumbo la kuharisha, maambukizi ya homa za malaria na mambo mengine, maji machafu ni jumla yanayochangia. Ikiwa pale tunawafundisha watoto wetu ili wawe wataalamu, lakini mazingira yao hayaridhishi, tatizo likitokea tutamlaumu nani.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi nashukuru dakika tano nitazitumia vyema wala sitokukera.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote waliowasilisha utekelezaji wa ripoti. Vile vile nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wake mzuri. Lakini niende moja kwa moja katika mchango wangu mfupi kama nilivyoomba.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niende katika Wizara ya Afya ambayo ni wizara nyeti kabisa kwa wananchi na maisha yao. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Afya, babu Duni kwa jitihada anazozichukua ili wizara hii iende vizuri na huduma zake. Lakini pamoja na jitihada zote anazochukua bado kuna utata wa kutosha katika huduma hizi za afya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mfupi tu. Kuna vituo vyengine hasa vya vijijini havina huduma za kutosha wala havina huduma nzuri. Mfano ulio hai ni ndani ya Jimbo langu la Kojani na ndani ya kisiwa cha Kojani. Kwa kweli tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya Umoja wa Kitaifa, kwa kujenga kituo kizuri cha afya katika Kisiwa cha Kojani. Lakini hivi sasa kituo hicho kimebakia kuwa ni jengo tu, huduma hazipatikani. Ukiangalia mazingira ya Kojani ni kisiwa kinachoishi watu wengi kati ya visiwa vidogo vidogo vya Zanzibar, lakini bado kuna utata wa afya. Sasa niseme.

Mhe. Mwenyekiti, inasemekana katika kituo kile karibu miezi sita hakuna dawa yoyote, hata *panadol* hakuna. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni tatizo kubwa sana katika mambo ya afya na mazingira ya kisiwa kilivyo. Kama hakuna huduma kama hizo zinazopatikana ni lazima tukimbilie hospitali ya Wete au Chake Chake na ni mahali pa kivuko. Mgonjwa akitokewa na tatizo hata ukipata huo usafiri basi masaa mawili yameshapotea. Kama mtu yuko hali mbaya basi anaweza kupoteza maisha yake ndani ya mtumbwi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hiyo haitoshi. Katika kituo hicho cha afya kuna uzalishaji wa kinamama pale, lakini jambo la kusikitisha na la kuhuzunisha kabisa, hata maji hakuna katika kituo hicho. Mhe. Mwenyekiti, na hilo ni tatizo kubwa na sumu, tuwaangalie sana watu wa visiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba katika mazingira hayo ni ya hatari. Tunashukuru Naibu Waziri wa Afya alituondolea tatizo moja, nampongeza sana la kutuletea madaktari, lakini madaktari na jengo tupu bila ya huduma basi hatujafanya chochote, maana daktari anakwenda pale lakini hana nyenzo afanye nini, hilo ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Hili limezungumzwa sana na kila mtu, lakini sio kwamba tunasema kwa utashi tu, ila tunasema kwamba vitendo vya kuwadhalilisha wanawake na watoto vinakithiri sana siku hadi siku. Sijui ni kwa sababu hayana usimamizi mzuri au vipi. Namuomba

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, dakika tano zako umeshazimaliza.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Haya, namalizia kidogo. Lakini tunaomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri husika anafuatilia na azidi kufuatilia. Ni hapa juzi tu mtoto wa miaka mitatu kabakwa na baba yake, anayesadikiwa ni baba yake wa kambo na alimjeruhi vibaya sana, mpaka mtoto akalazwa Al Rahma anasikilizwa pumzi. Hivi ni vitendo vya kudhalilisha na vya uadui. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba wizara husika zisaidiane, ili kukomesha vitendo hivi ni vya aibu na vya ujasiri kabisa ambavyo ni vibaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante, ujumbe umefika.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia uhai na uzima uliotufanya kufika hapa, na kutupa fursa ya kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kwanza natoa shukrani zangu maalum kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Hija Hassan Hija Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake mbele ya Baraza lako tukufu, kuhusu Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea Kamati imetupongeza kwa heshima na taadhima, tunazipokea shukrani hizo kwa wizara pamoja na watendaji wake. Lakini nataka nirudie tena maelezo yangu, kwamba mafanikio ya utekelezaji tuliyoyapata yamechangiwa sana na Wajumbe wa Kamati katika ziara zao za kukagua shughuli za utekelezaji unaotendwa na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru wale wote waliochangia na michango yao itatusaidia sana katika kufanya kazi zetu vizuri zaidi. Mhe. Mwenyekiti, nimechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 9, nawashukuru sana na ninatoa ahsante kwao. Kwa hivyo, nianze kuwataja mmoja mmoja. Wa kwanza aliyechangia ni;

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Asha Bakari Makame
3. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
4. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
5. Mhe. Ashura Sharif Ali
6. Mhe. Saleh Nassor Juma
7. Mhe. Panya Ali Abdalla
8. Mhe. Salim Abdalla Hamad
9. Mhe. Hassan Hamad Omar

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme katika michango yote ya Wajumbe, suala la udhalilishaji limechukua nafasi ya kwanza. Udhalilishaji na ubakaji wa watoto na wanawake. Sasa naomba kutoa maelezo ya ufafanuzi kwa Wajumbe mbali mbali waliochangia suala hili la udhalilishaji, kwanza naomba nianze hapo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza suala hili alilianza Mhe. Asha Bakari Makame, lakini nataka niseme najibu kwa wote waliochangia juu ya udhalilishaji na ubakaji. Mwakilishi huyu wa viti vya wanawake, alielezea juu ya huzuni zake kwa watoto wanaotendewa vitendo vya udhalilishaji, ambavyo hivi sasa vimekithiri miongoni mwa wanajamii. Nataka niungane naye katika kuwasihi na kuwaomba wananchi, tushirikiane katika kupambana na vitendo hivi viovu vinavyoidhalilisha nchi yetu na utu wetu, tunawaomba wananchi waache tabia hii mbaya ambayo inadhoofisha taifa letu, tuwaacheni tena watoto udhalilishaji sasa basi!

Pia alizungumzia juu ya majengo ya wizara, nadhani suala hili hakulichangia Mhe. Asha Bakari tu, lakini wamechangia wengi. Nataka nikubaliane na wale wote waliochangia juu ya jambo hili. Ndio maana Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na wizara nyengine mbili, suala la kujenga ofisi Pemba, tumelipa uzito mkubwa sana, kwa kuelewa umuhimu wake. Tunaamini juhudi zetu za pamoja za kujenga majengo ya ofisi hapo Gombani Pemba yataendelea kama tulivyokusudia mara tu tutakapopata mshiko, yaani fedha za kufanyia kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Saleh Nassor Juma na yeye alizungumzia tatizo la omba omba, tatizo hili linaonekana kukua katika jamii zetu, hasa katika miji. Ni kweli hali hii ya omba omba imeanza kujitokeza na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, tayari tumeanza kulifanyia utafiti. Kwa taarifa za awali imeonekana asilimia 86 ni omba omba, wenye umri kati ya miaka 40 na 60 ambapo asilimia 65 ni wanawake na asilimia 35 ni wanaume. Hii ni aibu kubwa jamani.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuziangalia sababu zinazosababisha kukua kwa omba omba, tumeona kwamba sababu kubwa ni hali ngumu ya maisha inayowakuta wale ambao hawafanyi kazi na wanashindwa kujituma ili kujitafutia riziki zao kama wanavyofanya watu wengine. Lakini wengine wamegeuza omba omba kuwa ni tabia yao na ni njia ya mkato ya kujitafutia maisha.

Jengine ambalo tumeliona ni kwamba watu wengi hivi sasa ambao wana jukumu la kuwahudumia wazee wao na kuwapatia maisha, wengi wao wanakwepa jukumu hilo na wanawaacha wakiwa barabarani wanaombaomba. Jukumu ambao ni wajibu kwa kila kijana kulea na kumuhudumia mzee wake. Kwa hivyo, ni suala la kuporomoka kwa maadili katika jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, itaendelea kuwahamasisha na kuwaelimisha wana jamii juu ya umuhimu wa kutunza familia zao. Aidha, juhudi kubwa tutachukua katika kuwasaidia na kuzishawishi familia zenye hali ngumu kuanzisha miradi midogo midogo ili iwasaidie kukimu maisha yao na kuondokana na omba omba.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Saleh Nassor pia alizungumzia na kupongeza sana suala la kuwapatia vijana eneo la kufanyia kazi kutokana na kazi nzuri aliyoiona kwa vijana wa Tunguu, wanaolima kilimo cha maua ya harozela na mboga mboga. Nataka nilifahamishe Baraza lako tukufu kwamba wizara ina mkakati maalum wa kuwaendeleza vijana katika suala la kilimo, ili kuwawezesha kupata mapato makubwa yatakayoweza kuwasaidia kujiendesha wenyewe na kusaidia familia zao.

Kwa kweli niseme mbele yenu Waheshimiwa Wajumbe, kwamba walioko Tunguu, nawapongeza kwa bidii na juhudi zao na kwa namna wanavyojituma. Wengine sifichi wamekimbia kwa sababu ni kazi nzito. Katika mwaka wa fedha ujao tumekusudia kuongeza mashamba, vijana pamoja na kuwapatia utaalamu wa kilimo cha mboga mboga, kwa kutumia *green house* ili kuongeza mapato yao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie kidogo kuhusu maelezo ya Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, maarufu anaitwa BHAA. Mhe. Mwenyekiti, alizungumzia Mhe. Mjumbe kuwa kesi za udhalilishaji ni nyingi bado hazijapatiwa ufumbuzi wa kufaa na kutiwa hatiani wale waliotenda makosa, ili kukomesha vitendo hivyo vya udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba kesi ni nyingi na bado hazijakomeshwa, maana wale wanaofanya vitendo vile bado hawajapata adabu. Lakini *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia jambo hili tutalishughulikia na tutalisimamia kidete, ili angalau watu wawili watatu wapate adabu kidogo. *(Makofi)*

Kwa kweli tunalo tatizo kubwa katika uendeshaji wa kesi kwa masuala ya udhalilishaji wa watoto na wanawake. Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa pamoja tumeandaa mkakati wa kulishughulikia suala hili la kesi za udhalilishaji.

Kikao maalum kilichokuwa chini ya Mwenyekiti Abubakar Khamis Bakary (Waziri wa Katiba na Sheria) kiliitishwa na kuwashirikisha watendaji na viongozi kutoka Jeshi la Polisi, Waendesha Mashtaka (*DPP*), Mahakimu, Madaktari, Wanasheria pamoja na wadau wengine wa *NGO's* wanaoshughulikia masuala ya udhalilishaji walikutana na kulizungumza kwa kina pamoja na mimi mwenyewe, suala hili la kesi za udhalilishaji na kuliwekea mkakati wa pamoja na kulishughulikia haraka na kuhakikisha kwamba kesi zote za udhalilishaji zinapata ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani wale wote waliokuwa wakiniuliza kwa nini kesi hazihukumiwi naamini nimejaribu kuwajibu. *(Makofi)*

Vile vile wahusika wanaobainika kutenda makosa kupewa adhabu kali, ili iwe funzo kwa wengine wote katika jamii. Mhe. Mwenyekiti, waswahili wanasema *mla kuku wa mwenziwe miguu humuelekea*. Sasa wewe unamfanyia vitendo vibaya mtoto wa mwenzio je, ukijakufanyiwa wewe utaona vizuri. Kwa kweli mimi siwaelewi watu, lakini kama ningekuwa nawaelewa wale wanaowafanyia watoto wa wenzao ubakaji, basi ningewambia hebu jitahidini kidogo kumsogelea, ili apate adabu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna suala la watoto wenye mazingira magumu ambalo lilizungumziwa hapa. Kwa hivyo, naomba kujibu kwamba jambo hili ni miongoni mwa kazi ambazo tunazozishughulikia, na hivi sasa Wizara inaandaa sera itakayoelezea jinsi ya kuweza kuwasaidia wazee, wakulima, watoto na wale wote ambao wanahitaji msaada wa kijamii katika masuala ya afya na usafiri. Kwa kweli sera hii ikikamilika itaweza kuleta uwiano mzuri wa kukidhi maisha na kuweka hali za wananchi kuwa sawa.

Suala jengine ni kuhusu Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwamba Mwanasheria Maalum awekwe kwa ajili ya kushughulikia kesi za watoto. Mhe. Mwenyekiti, nataka nieleze kidogo juu ya suala hili kwamba suala la kushughulikia kesi sio la wizara yangu tu, bali ni la Mkurugenzi Idara ya Mashtaka (*DPP*).

Lakini kwa umuhimu wa jambo hili wizara inao wanasheria na pia tumeunda Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto (*Child Protection Unity*), ili kufuatilia masuala yote ya haki za mtoto ikiwemo kesi za udhalilishaji na ubakaji. Pia tunayo mashirikiano mazuri na Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*), na kwa mkakati tulioweka nao hivi sasa wa kushughulikia kesi za udhalilishaji wa watoto, basi tunaamini kwamba tutapata mafanikio tunayoyakusudia na Mwenyezi Mungu atujaalie *Inshaallah*. *(Makofi)*

Nikiendelea Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe jibu kidogo kwa Mhe. Saleh Nassor Juma, kwa sababu alikuwa ananiuliza kwamba kesi nyingi kuwa hazihukumiwi na hilo tayari nimeshajibu za kubakwa kesi hizi zinakwenda vipi. Mhe. Mwenyekiti, haya mambo ya kesi yana utaalamu wake kidogo haya, lakini kwa ufupi kesi zinashughulikiwa kikamilifu.

Sasa naomba niende kwa Mhe. Ashura Sharif Ali yeye alizungumzia kuhusu *DNA* bado ni tatizo. Mhe. Mwenyekiti, kweli nakubaliana naye kwamba *DNA* bado ni tatizo.

Vile vile alizungumzia kwamba tufanye utaratibu maalum wa kushughulikia Vijana, Wanawake na Watoto, ili kesi zishughulikiwe pamoja na jengo la ofisi Pemba, nadhani kuhusu jengo la ofisi Pemba tayari nimeshajibu kwamba jengo hili tunalishughulikia kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mhe. Mjumbe, pia alisema kwamba watu huwa wanakataa kutoa ushahidi. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hilo ni tatizo kwamba anasema mimi ni jirani yangu aliyefanya hivi au huyu ni ndugu yangu, sasa nikienda kusimama kutoa ushahidi itakuwa tatizo kidogo kwangu, hivyo wanakataa kutoa ushahidi. Mhe. Mwenyekiti, naomba niwaambie kwamba watu kwa mambo maovu wasikatae kutoa ushahidi jamani. *(Makofi)*

Mhe. Mwakilishi alieleza kwamba pamoja na mambo mengi tuliyonayo, lakini bajeti yetu ni ndogo. Kwa hivyo, mimi namshukuru Mhe. Mjumbe na serikali imeshalisikia suala hilo. *(Makofi)*

Halafu kwa sababu tunayo dhamana kubwa ya kuwalipa wale jamaa wanaoumia kazini. Kwa kweli suala hili nataka nieleze kwamba tumeshalikalia kitako mimi na Waziri wa Fedha, ili tuone tutafanya namna gani, kwa ajili ya wale wote walioumia kazini walipwe fedha zao na baadaye mambo haya tena yarudi kwa kila wizara inayohusika, ili wale waliopata ajali kazini wajisikie kidogo.

Nikiondoka hapo sasa niende kwa Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi. Kwanza ameipongeza Kamati na mimi nakubaliana naye, alisema tuvitambue vikundi na tutafute misaada mingine, tuvipe elimu vikundi vya ushirika, vikundi vipate usajili. Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana naye kwa hili na tukishirikiana na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, ambaye yeye ndiye anayehusika na mambo ya usajili, basi nitamuhimiza ili kila kikundi tuhakikishe kwamba kimepata usajili.

Vile vile alisema kuna Kikundi cha Wanawake Wajane ambao tayari wameshapata usajili, kwa hiyo alinitaka Mhe. Mjumbe kwamba kama siwajui hao wanawake basi niwatafute mpaka niwaone, ili tuweze kuwasaidia na kuwapa moyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Salim Abdalla Hamad ametaka kujua Kikundi cha SELEMU *Women Group* au wamehamika katika jengo hilo au wamekodi. Kwa hivyo, nataka nimueleze Mhe. Mjumbe kwamba jengo hili ni lao wenyewe, ambapo wamejenga wenyewe wakisaidiwa na watu wengine wanaowajua wao wenyewe na wala hakuna kukodi hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwakilishi, alieleza kwamba kuna vikundi 6 ambavyo vimepewa msaada. Lakini kabla ya hapo alisema katika maelezo yetu kule ameona kwamba tumesema mambo ya utaalamu kwa nini wakapewa Pemba tu na isiwe Unguja na Pemba. Mhe. Mwenyekiti, tumesema hivyo kwa sababu Pemba wale viongozi wa vile vikundi utaalamu wao ni mdogo au niseme hawana utaalamu.

Kwa hivyo, tumetoa nafasi maalum kwa ajili yao tunatoa mafunzo, ili wapate na wao kujua na kwa sababu kule hakuna mambo ya mitandao pamoja na mambo mengine, kwa hiyo lazima kwa vyovyote wizara inabidi tuwasaidie. Kutokana na hali hiyo, ndio maana tukajilazimisha kutoa utaalamu kwa wenzetu hawa wa Pemba.

Mhe. Panya Ali Abdalla naye kwanza ametupongeza na ninashukuru sana, alisema kwamba Wizara imefanya utafiti wa vikundi mbalimbali na kujua aina ya mafunzo wanayohitaji hao wenzetu. Mhe. Mwenyekiti, nataka nieleze kwamba tumefanya utafiti wa kujua wanawake wanahitaji nini na tuwasaidie nini, kwa sababu na wewe unapendelea kwamba *ZASOZE* katika wilaya au mkoa wako iweko, basi Mhe. Mwenyekiti napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba hilo linawezekana na ninachokuomba ajitayarishe na fedha maana kuna kazi pale. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji alizungumzia kuhusu suala la upatikanaji wa mikopo kwa vikundi. Mhe. Mwenyekiti, tunasema suala hili halizingatii mgawanyo wa kimajimbo au wilaya, isipokuwa kikundi kinaomba kwa mujibu wa mahitaji, Wizara inafanya tathmini ya maombi haya na uwezo wa kurejesha mkopo huo unaombwa na Kamati ya Kitaalamu inayofuatilia mikopo hiyo ikiridhika, basi kikundi kinapatiwa mikopo. Orodha ya vikundi vilivyopatiwa mikopo ya vijana itawasilishwa kwa maandishi Mhe. Mwakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naona nimejitahidi na kama kutakuwa na Mjumbe yeyote ambaye anaona kwamba sikumjibu kama alivyotaka yeye mwenyewe basi naomba radhi sana. *(Makofi)*

Vile vile nasema kwamba mimi niko tayari kufanya kazi na nyinyi wakati wowote na ninawakaribisha katika Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, ili tushirikiane kwa sababu Wizara hii si ya ustawi wa jamii tu peke yake, lakini nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi mumo, kwa maana ya rika zote zipo. Kwa mfano, kuna wazee akina sisi, vijana, wanawake na hapa hapana watoto tu, lakini nyinyi wenyewe munao watoto. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba sana tushirikiane katika mambo haya na tuone kwamba janga hili la udhalilishaji tunalisimamia ipasavyo, tukiwa kwenye majimbo yetu, sehemu zetu za kazi, almuradi tuwe sauti moja kupiga vita janga hili la udhalilishaji na ubakaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Waziri ameua kunitaja tu kwamba mimi nimechangia, lakini lile suala ambalo nimelieleza hakunipa jibu. Kwa hivyo, naomba sana kwa unyenyekevu na nilisema hivi wakati wa bajeti ulituahidi kwamba utatuletea Hati ya Jengo la Watoto Yatima, niliomba sana na nilitegemea kwamba utanijibu na kuniambia kuwa hati sasa iko tayari, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ahsante sana kwa kunikumbusha hili kuhusu hati ya watoto.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kwanza ulikuwa upate ruhusa yangu kujibu hilo swali. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri sasa nakuruhusu.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa ridhaa yako naomba sana kumjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kama hivi ifuatavyo. Kuhusu hati Mhe. Mjumbe nakuomba uje katika Ofisi ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto nikuoneshe hasa uisome wewe mwenyewe. *(Makofi)*

Lakini kuna suala moja ambao nilisahau kidogo kukujibu, kwamba ulinipongeza mimi kwa namna ninavyosimamia wale vijana wa *Scout*. Kwa hivyo, nakushukuru na ninasema ahsante sana. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Sasa ni zamu ya Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ahsante lakini dakika 10 hazinitoshi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, sawa tutaongeza na uwasilishaji wa majumuisho ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Waheshimiwa Wajumbe kutokana na hali tuliyofikia itabidi tuendelee na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Mwenyekiti wa Kamati muda wa jioni.

Lakini naomba Waheshimiwa Wajumbe, munisikilize hivyo nitamuomba Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutuwekea kando Kanuni, ili tuweze kumaliza na Wizara ya Afya.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwa maombi ya Baraza la Wawakilishi naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liongezewe muda kuweka kando Kanuni na ikishindwa isionekane imeshindwa serikali. Baraza la Wawakilishi limeomba kwa kupitia kiti chako, basi naomba kutoa hoja kuweka Kanuni kando ya muda, ili tuongeze muda mpaka hapo shughuli za asubuhi zitakapomalizika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa wengi wamekataa na kwa kuwa Baraza letu linafuata demokrasia, basi nachukua fursa hii adhimu kuakhirisha kikao mpaka saa 11:00 jioni.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kukataliwa)

(Saa 6:44 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nishukuru kiti chako kwamba asubuhi ilipoonekana muda ni mchache mkaniruhusu nianze jioni. Kwa hivyo ninakushukuru wewe na ninawashukuru wajumbe wote kwa kunistahmilia.

Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati wewe na pamoja na wajumbe wote na naomba niwapongeze na kuwashukuru kwa michango iliyotolewa katika kujadili ripoti ya kamati na taarifa nilizotoa Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitangulize kwamba pale mnapotukosoa na hasa napotukosoa kwa hamasa mimi mwenzenu huwa ninapata faraja kwamba mna nia ya kutusaidia. Mnapoyaona maovu mnatueleza na mazuri mnatupongeza, kwa hivyo kwa yote hayo ninashukuru. Na wachangiaji waliochangia Wizara ya Afya ni 17 na nawaomba niwataje:

1. Mhe. Hija Hassan Hija:
2. Mhe. Makame Mshimba
3. Mhe. Asha Bakari
4. Mhe. Nassor Salim
5. Mhe. Ismail Jussa
6. Mhe. Hussein Ibrahim
7. Mhe. Saleh Nassor
8. Mhe. Ashura Sharif
9. Mhe. Mohammed Haji Khalid
10. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
11. Mhe. Salim Abdalla
12. Mhe. Panya Ali Abdalla
13. Mhe. Ali Salum Haji
14. Mhe. Rufai Said Rufai
15. Mhe. Hassan Hamad

Na Waheshimiwa wawili walileta kwa maandishi Mhe. Marina na Mhe. Salma Bilali wote hao wametoa michango mikubwa tu na itakayonisaidia hasa kwa sababu tunakwenda na kwenye bajeti kujiandaa vizuri zaidi.

Mheshimiwa mjadala ulikuwa wa mambo mengi lakini mengi yalikuwa yakirudia. Mhe. Mshimba akitaja jengo la macho hospitali mwengine anataja jengo la macho, kwa hivyo ninapojibu naomba ionekane kwamba nimewajibu wote kwa hoja zile kuliko kwamba kila mtu nieleze moja moja.

Sasa la kwanza lililozungumzwa kwa urefu sana ni suala la *DNA machine*, *DNA machine* ni kweli kuna wakati hapa tulisema ipo na kweli ipo tuliipata kwa msaada lakini sisi si wataalamu, tulipokwenda tufanya uchunguzi juu ya utaalamu na vipi tunaweza kuitumia tukagundua kwamba kumbe vile kile ni kama kitonyo kwenye maji ya bahari. Ile ni mashine inayoweza

kuibagua ile *DNA* kutoka damu, maana *DNA* lina urefu wake kitaalamu si vizuri kulitaja maana mimi si *bilologist*. Kwenye damu ndio unatoa *DNA* lakini ukishapata ile *DNA* sasa uende kwenye hivyo vinavyoitwa vinasaba unapata *DNA* kwanza halafu tena utafute vinasaba. Kwa hivyo ile tuliyokuwa nayo inaweza kufikisha hapo tu. Sasa ili kufika mpaka huko samahani useme huyu mtoto wa Juma Duni kuna mamashine makubwa sana ambayo hivyo vidudu vinabidi vipitishwe. Mashine ile haina uwezo wa kufanya hivyo.

Lakini suala la kutoa maarifa kidogo kwamba hata huko Tanzania Bara ambako liko moja nchi nzima na matumizi yake ni matumizi maalum na kwa sababu maalum na mara nyingi huwa inatumika pale ambapo kunatokea utata wa maamuzi hasa ya mahkama au ya kesi za mauaji. Maandalizi yake yanakuwa si ya kuwa kila kitu kifanywe. Sasa sisi tunafikiria kwamba kila anapotokezea mtoto kubakwa twende kwenye *DNA* sio rahisi kiasi hicho. Kwa hivyo naomba nikubali kwamba ile mashine ina upungufu na kuinunua kwa bei tulizoambiwa inahitaji mafedha mengi sana si chini ya milioni mia nane. Hatusemi kwamba hatutonunua lakini hali ya uchumi wetu hivi sasa hatuwezi kusema tutanunua leo au kesho. Kama tutapata wahisani watatusaidia itakuwa jambo la maana na hasa kwa sababu huko tunakokwenda tunategemea hospitali yetu ya Mnazi Mmoja iwe ni hospitali ya rufaa ya kuweza kuhitaji maamuzi makubwa kama hayo. Kwa hivyo tunakubali kwamba kuna upungufu huo na mashine ile ipo lakini haiwezi kufika *stage* tuliyonayo.

La pili lililozungumzwa kwa sauti kubwa ni suala la *incinerator*; mashine ya kuchomea taka hasa pale Mnazi Mmoja na wengi waliokuwa wakisema walikuwa wanarudia hakuna mashine ya kuchomea taka, hatari, madudu yanakwenda baharini. Mashine tunayo isipokuwa ya zamani na haiwezi kuchoma wingi wa taka zilizokuwepo ile inayotumia kuni. Na ikichoma inatoa moshi mnajua mambo ya miili ya binaadamu na viwiliviwili yakichomwa harufu yake nzuri.

Kwa hivyo mara nyingi si kitu ambacho kinachopendelewa kutumiwa sana. Tunachoma kwa sababu hatuna budi. Lakini naomba niseme kwamba kwenye bajeti yetu ya mwaka jana tuliweka kwamba tununue na tulitenga si chini ya shilingi milioni mia tatu kwa azma hiyo. Bahati mbaya tu kwamba kutokana na ufinyu wa fedha hadi sasa hatujaweza kupata fedha za serikali kuinunua. Isipokuwa naomba niwahakikishie Wajumbe kwamba tumepata fedha za msaada za kulipia madeni kuna fedha zinaitwa fedha za kusamehewa madeni kwa lugha ya kigeni inaitwa MDRI. Tumeshakubaliana Wizara kwamba kwa vyovyote vile moja katika priority mwaka huu ya fedha zile tununue hiyo *incinerator*. Kwa hivyo nategemea pengine hadi tutakapokuja kwenye bajeti tutakuwa tuna jibu sahihi tumefika wapi katika kutoa tenda au kuiagiza.

Mhe. Mwenyekiti suala la tatu ni suala la dawa, kule kwetu kuna kitu kikiwa kimedumu kwa muda mrefu tunaita donda ndugu, aa suala hili tena limekuwa donda ndugu. Kumbe zamani tulikuwa hatujui donda ndugu maana yake kensa. Sasa dawa imekuwa ni hoja inayosemwa sana kwenye Baraza kama vile donda ndugu, dawa hakuna, dawa hakuna lakini nawaomba wenzangu vile vile munisaidie kukumbuka kwamba tumetoka mbali tangu kuingia katika awamu hii tulikuta sisi zinatumika milioni 300 tu kwa dawa. Tumeendelea kupigiwa kelele na Baraza, tumeendelea kueleza serikalini, hivi sasa serikali imefika daraja ya kutupa bilioni tatu. Tangu milioni 300 mpaka bilioni tatu zilitengwa bilioni moja na nusu kutoka serikalini, na bilioni moja na nusu kutoka serikalini na bilioni moja na nusu kutoka msaada wa *DANIDA*. Tumeweza

kuagiza vile tulivyoweza kuagiza lakini suala hilo halijapata ufumbuzi wa kutegemea la kudumu kwa sababu ya mfumo wenyewe wa kuagiza.

Sasa tulipokuwa tunaeleza mfumo wa kuagiza na mfumo wa kusambaza kidogo watu walichanganya. Mfumo wa kuagiza ni ule wa tenda na sisi dawa takriban zote kwa sababu ya misaada ya Shirika la *DANIDA* tunanunua kutoka ghala kuu ya dawa Dar es Salaam linaitwa MSD. Tunapeleka pesa huko hasa zile za *DANIDA* pamoja na zile za kwetu tunaletewa dawa, na tukiletewa dawa zile nyengine tunaletewa kwenye viboksi moja kwa moja kinatiwa alama hasa hiki kinakwenda kituo cha Kitongoji, hichi kinakwenda Msuka moja kwa moja kutoka huku. Sasa yanapotokea matatizo mara nyengine na mshawahi kusikia lile dudu kule ilifika *stage* mpaka Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya akasimama kulikuwa na matatizo. Kwa hivyo akipata matatizo kule tulikuwa na sisi tunapata matatizo hapa, lakini baada ya marekebisho hali hiyo sasa nzuri. Sasa dawa hivi sasa haiko hali mbaya kama tulivyoanza mwezi wa Julai, dawa tumepata zinaendelea kusambazwa na mbali ya zile tunazopitisha kwenye tenda ya Wizara.

Sasa kumesemwa dawa za wagonjwa wa akili zamani dawa hizi nazo zilikuwa zinafanywa mbali, sasa tunazinunua pamoja ili kurahisisha upungufu huo. Lakini ni vizuri tuelewe hakuna ghali kama dawa za kuwatibu wagonjwa wa akili na dawa ya kutibu mgonjwa wa akili si kama ile *dose* ya malaria, kwamba unaambiwa ule hizi baada ya wiki umepona, ni kitu cha maisha mpaka yule mtu uhakikishe amepona. Na mnaijua jamii yetu ukishaugua maradhi hayo hata uwe mzima utaambiwa aa huyu jamani alipita huko upande huo. Kwa hivyo inakuwa ni suala la muda mrefu. Sasa kila wagonjwa wakiongezeka haina maana kwamba matumizi ya dawa yanapungua, kwa sababu wale wa zamani inabidi uwape na hawa wapya uwape. Suala hilo hivi sasa haijambo tunaendelea nazo dawa zinapatikana ingawa si za kutosheleza kama tulivyotegemea.

Lakini tumeamua katika kutatua tatizo la dawa ni kwamba kuna dawa ambazo haziwezi kukosekana popote pale na kuna dawa ambazo zinahitajika kwenye *referral* tunafanya uchambuzi tunashirikiana na wataalam ili tutayarishe mfumo wa tenda utakaokuwa unafuata masharti ya benki ya dunia na yoyote sasa yule anaweza aka-*tender* pamoja na hiyo *MSD* nayo ikishakubali masharti yale ya benki ya dunia kutoa tenda atakaepata ndie tunatiliana mkataba kwa ajili ya kuleta muda wote ndio hiyo mkaikuta tumeiandika *frame work contract*, hivi sasa hatujafika huko lakini Mungu anatusogeza huko.

La pili Usambazaji. Usambazaji kuna njia mbili tulikuwa zamani tunakuletea kilichokuwepo kama unakitaka, kama hukitaki haya, tunabadilisha utaratibu sasa tutakuletea utakachokihitaji ndio maana wanaita *pull and push*. *Pull* maana yake unavuta, *Push* maana yake unasukuma. Sasa *Push* ilikuwa tunaleta sisi, *pull* wewe unatwambia nipe hiki mfumo huo umeanza kwa baadhi ya vituo na uko kwenye *trial* na unakwenda vizuri na pale mwengine mulimokuwa hamjanini unafuata utaratibu vile vile wa zamani. Hatuwezi kukosa matatizo katika kuanza utaratibu mpya, sasa nakumbuka Mhe. Jussa akasema dawa ziko Ghala Kuu Maruhubi lakini Mnazi Mmoja hakuna hayo ni matatizo ya kuwasiliana tu lakini utaratibu wa kukusanya mahitaji ya dawa Mnazi Mmoja unajulikana, mfamasia mkubwa wa hospitali anapita kila Idara anaeleza mahitaji ya kila Idara anaifikisha Maruhubi dawa zilizokuwepo zinaletwa hospitali zinapelekwa tena. Na huko mbele tunakokwenda kila kitengo au Idara ya Mnazi Mmoja itakuwa ni Idara kamili inayojitegemea kutwambia inahitaji kiasi gani ya dawa na mahitaji gani ya bajeti na tukishaitengea bajeti hana sababu tena kuja kutwambia hana dawa. Kwa sababu makisio atakuwa

amefanya yeye kwa matumizi kama vile kinavyofanya kituo kilioko Msuka au Makunduchi au Jambiani.

Katika mfumo huo tutakuwa sasa suala la kumimina bila ya kujua dawa zinakwenda wapi itakuwa tunaweza kuhoji kwa nini dawa hazikutosha na wewe ulishasema unahitaji hicho. Tunatarajia kuweka mfumo unaitwa *PBF* (*Performance Based Fund)* kwamba wewe unafanya, kile unachofanya ukitekeleza sisi ndio tutakupa.

Suala jengine kubwa lililozungumzwa ni suala la wajawazito. Waheshimiwa mimi pamoja na nyinyi sote ni matokeo ya akina mama na siku moja hapa nilisema kwa jeuri, kwa kejeli na kwa ukweli kwamba hivyo anaweza akatokea mtu hapa akatwambia yeye kazaliwa na mwanamme mkanicheka. Ni kwamba jeuri yetu sote hapa sisi kama si kinamama tusingekuwepo. Kwa hivyo watu wanapozungumza tatizo la mama mjamzito si kwamba naliona tu kwa sababu nawajibu lakini najiona kwamba kusingekuwa na mama nisingekuwepo.

Sasa lilipozungumzwa kwamba Rais ameamua kuwaacha kinamama bila ya kulipa na kwamba sasa wanaendelea kulipa ati kwa sababu tumedharau agizo la Rais la hasha! Bado agizo la Rais lipo na tunaendelea kulitekeleza. Ninavyosema hapo katikati matatizo ya dawa yalipotokea yalitokea kwa bahati mbaya, lakini mfumo huo unaendelea kuwepo na hakutakiwi watu kuchangishwa pesa kama hapana budi hatuwezi kumwacha mama akafa au mtoto akafa lakini tunatakiwa huduma hiyo ipatikane bila ya malipo. Hata hivyo kuna watu wengine hawapendi kufuata utaratibu huu kwa sababu ulikuwa na maslahi nao. Juhudi tunafanya suala hili tuliweke sawa ili likae kama vile lilivyoagizwa na Rais.

Na ni vizuri kuelewa vile vile Mhe. Mwenyekiti kwamba huko duniani huwezi kuzungumza chochote hivi sasa katika misingi ya huduma za afya kama hujazungumza mama na mtoto. *Meternal health and child surviver, Meternal health, Meternal mortality, infant mortality* kila utakapokwenda mikutano yote unayosikia afya tunakwenda watu wanajaribu kutaka kuona kwamba mama hawafi na vitoto vichanga havifi. Kwa hivyo ni suala linalohitaji kupewa kipaumbele sana. Juzi kama wiki mbili tatu nilikuwa Rwanda ilikuwa hoja ni hiyo hiyo. Mkutano niliokwenda Nigeria hoja ilikuwa hoja ni hiyo hiyo, na kule Nigeria *UNFPA* wakaamua kwamba kuna dawa kama 13 muhimu za ku-*save* maisha ya mama na mtoto wanahitaji ziwe zinapatikana muda wote na wako tayari kusaidia katika kutekeleza shughuli hiyo.

Waheshimiwa ili nisichukue muda zaidi suala lililozungumzwa na wengi madeni ya umeme na Mhe. Jussa akafika hadi kusema ee basi hata umeme wa vijijini wa kwenye vituo 20,000 sijui 80,000 nataka niwaeleze kwamba deni la umeme si la Wizara ya Afya tu ni la serikali nzima, ni dudu lilokaa miaka mingi watu walikuwa na tabia ya kutumia umeme bila ya kulipa, madeni yamekusanyika sitaki kusema hapa kama na Wizara zenu zote zina madeni sina hakika, na hata Ofisi hii ya Baraza la Wawakilishi. Umekuja waraka Baraza la Mapinduzi Shirika la *ZECO* limeeleza tatizo lake na madeni ni makubwa, wengine wanafika milioni 500, wengine milioni 200, sisi kwa sababu ni suala la huduma hatuchumi ndio linatokezea.

Serikali inakusudia kukubaliana jinsi ya kulipwa Shirika la *ZECO* ili lijiendeshe kibiashara. Uamuzi huo umeshafanyika serikalini na kuna mazungumzo baina ya *ZECO* na Wizara ya Fedha jinsi ya kulipa. Sisi tutaambiwa litalipaje kama litatiwa kwenye bajeti tulipe kidogo kidogo ni

sawa, lakini si suala la kulaumiwa tu ni suala la kitaifa. Kama hapo Mnazi Mmoja; hospitali kubwa na madeni makubwa sana. Kwa sababu fedha wanazopata huwa wanaangalia huduma zaidi kuliko kulipia Shirika la Umeme. Kwa hivyo hili nilikuwa nataka nilijibu hivyo lisionekane kama ni sisi tu watu wa Wizara ya Afya.

Lakini nataka nitoe maelezo kwamba sisi tuna vituo visivyopungua 134 mbali ya serikali za Wilaya 3, *quotage* hospital 4, na hospitali ya Muembeladu ile ya wagonjwa wa akili na Mnazi Mmoja. Sasa hapa asubuhi kila mmoja analalamika kituo kipya cha upande gani kimejengwa na wananchi hakijamalizwa itakuwaje, watu hawafikiri haya kwamba ukishakijenga kituo kile kinahitaji wafanyakazi, kinahitaji umeme, kinahitaji maji, kinahitaji huduma, umuhimu wa Mwakilishi anaona aweke jengo tu mengine anayasahau. Tunapofanya hivyo na haya mengine tuwe tunayaona kwamba yanatuwajibikia. Ninachoomba tu Waheshimiwa badala ya kuongeza kujenga vituo, vituo tunavyo vya kutosha.

Mheshimiwa mmoja hapa asubuhi alisema kwamba tuna vituo havina madaktari na kwamba tulipewa semina tukaenda pale kwenye *Sea View* nadhani akaja mtaalam wetu akaiweka *map* ya Unguja na Pemba halafu akafanya *circle* ya kilomita tano akazungusha akakuta vyote vimo. Akaja kwenye kilomita tano akagundua 3 *kilometres* bado vituo vipo, yaani ukienda upande huu kilomita 3 utakikuta. Alipokuja ipanua ile *map* tukaulizana pamebaki wapi hakuna vituo baharini watu wakacheka pale. Tuna vituo vya kutosha vya kuhudumia wananchi. Tusifike *stage* ikawa sasa kila mwanachi ana kituo chake itakuwa ni miujiza ya dunia, tunahitaji tusaidie kujenga nyumba za wafanyakazi tusaidie dawa, tusaidie vifaa, tusaidie kuwalipia umeme na tusaidie huduma nyengine katika kituo badala ya kufikiria kujenga vituo zaidi na zaidi.

Mheshimiwa likaja suala la pesa za maendeleo hazipelekwi Pemba sikufurahi kidogo kwamba hii imeonekana kama ni agenda mradi huko Unguja Pemba hakuna. Mradi wa maendeleo ni mradi wa maendeleo hauko Unguja na Pemba ni mradi tu wa maendeleo wa Zanzibar. Inawezekana katika kuendesha mradi huo utafanyika Pemba au utafanyika Unguja. Kuna mambo mengine yanahitajika yawepo Unguja yawepo na Pemba, lakini kwa kawaida miradi yote ya maendeleo huwa bado inaendeshwa kutoka Makao Makuu, kwa hivyo si suala kwamba zinabaguliwa au nini lakini baadae nitakuonesheni hali ya bajeti ilivyo sio kwamba pesa hazipelekwi Pemba za maendeleo. Fedha za kawaida wale wenzetu wa Pemba wana *sub-vote* yao wenyewe moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha zinapelekwa huko Pemba. Na kule Pemba kuna Ofisi yao hivyo hivyo. Kwa hivyo fedha za huduma za kazi za kawaida hazipiti Makao Makuu ya Wizara zinakwenda moja kwa moja. Lakini fedha za mradi ukishakuwa mradi wa malaria maana yake ni mradi wa malaria, ukishakuwa mradi wa kichocho maana yake ni mradi wa kichocho, bila ya kujali kwamba huu ukafanywe Pemba, kama ni lazima ufanywe Pemba kwa sababu ndio kwenye vibwawa na vidimbwi vya maji, lakini si kwa sababu ya kubagua. Naomba hili tuliepuke isionekane kwamba labda kuna miradi ya pande mbili.

Mhe. Nassor Salim alizungumza suala la wananchi wawili nadhani jimbo lake kufariki, hata mimi nahuzunika sana kwa sababu hakuna bei ya uhai. Siku zote nikizungumza mimi sijasikia mtu akatiwa bei na siku mtu atakayotiwa bei itakuwa mtu sasa si mtu tena isipokuwa ni sawa sawa na bidhaa. Kwa hivyo hakuna bei ya uhai, akifa mtu hata kama utazaa mwengine atakuwa si yeye. Tunasikitika sana kwa yale yaliyotokea na tunahuzunika, nadhani ulikutana na watendaji wangu Wizarani wakakushauri uandike barua ili tulifuatilie. Tumewaambia watu wetu wa Tiba

Asili watizame katika orodha yao na kwamba ikilazimika watu wale wachukuliwe hatua, aidha za kisheria au hata kama itastahiki kutokana na ushahidi utakaokuwepo wafutwe katika daftari la tiba asili.

Lakini ni vizuri hoja hii imetokea kwa kupitia hapa nawambia wananchi mnaotizama na kunisikiliza si kila daktari wa tiba asili ana uwezo wa kutibu. Nyinyi mnapokwenda tahadharini na siku hizi inasikitisha Mhe. Mwenyekiti kila mtu kawa mganga, kila mtu kawa tiba asili, kila mmoja ukifungua radio anajitangaza ni balaa! Naomba radhi wananchi nitatumia maneno mengine si mazuri, ukienda msikitini siku za Ijumaa kila mtu anauza dawa ya nguvu za kiume. Sasa mimi kama Waziri natoka msikitini unasikia ee mzee nuri, chukua hii, mambo yatakuwa mazuri, nasema hee dawa za kiume jamani ndio zinazouzwa dawa za kike hakuna? Ni tatizo huyu anakwambia hii ya msuaki meno yako yatasafika. Mmoja katika jamaa zangu akanunua dawa ya msuaki siku ya pili domo likabambuka akatoka vidonda ni hatari kweli kweli. Lakini yote hii ni kwa sababu tulikuwa hatujawa na sheria ya kudhibiti. Mungu amejaalia tumepitisha sheria ya *public health* hapa kama miezi 6 iliyopita na wengine waliuliza suala kwa nini haitumiki.

Kamati tumeshaunda, kanuni zinatayarishwa, masuala yenyewe yalikuwa hayapo hatuwezi kuvamia tu kwa sababu tuna sheria tunahitaji kujipanga, lakini ni vita. Siku nilozindua Baraza jipya la Tiba Asili nikayasema yale kwamba jama mnatumaliza kila siku tunapata wagonjwa wa vibovu vya mkojo, kila mmoja kongosho bovu kumbe madudu wanayovamia mitaani ni madudu ya kuyamaliza. Wakaja juu wenyewe sijui sasa Waziri tutapambana nae, utapambana na mimi, mimi nimeshakufa tayari unapambana na mimi unaua kizazi kijacho ni hatari Mheshimiwa. Kwa hivyo tunaomba wananchi tahadharini tabia ya kusikia daktari kila mmoja akaona kwenda na nyinyi mna haki zenu kama utakuta umetibiwa na ukapata athari una haki ya kushtaki. Kule Marekani serikali zimeshawahi kushtakiwa kwa sababu ya matatizo ya kumtibu sivyo au kumfanyia sivyo kuliko vile utaratibu wa matibabu unavyotaka.

Suala jengine Mhe.Spika lililoulizwa ni benki ya damu ikaambiwa labda Pemba hakuna nyumba ya benki ya damu. Pemba tuna stoo ya damu, tuna huduma hospitali ya Wete, hatujapata tatizo la watu wanapohitaji damu kuikosa isipokuwa kikubwa inakuwa nadhani ni masafa kwamba labda mtu yupo Mkoani kuifuata masafa ya Wete. Lakini kuna kila taratibu ya kupata damu huko Pemba. Wengine walisema tujenge nyumba ya benki ya damu kule si vibaya. Lakini hebu tuone kile kilichojengwa hapa kwenye nyumba za wazee hapa kile tumesaidiwa na fedha za wafadhili, tutaomba kama inalazimu na itahitajiika tujenge kule Pemba Ofisi. Lakini kwa sasa huduma hizo zinakwenda vizuri na wala hatuwezi tukalalamika kwamba huduma hizo lazima ziwe kwenye jengo.

Mhe. Mwenyekiti naomba unistahmilie kwa sababu masuala mengine tuliyoulizwa jumba bovu la hospitali ya macho. Kila alosimama hapa jumba bovu, lina nyufa, linakufa wee, watu sijui kapewa milioni ishirini na tano nyengine hakupewa. Tumeulizana nimelitafuta imekwendaje mkataba ule. Mkataba ulifuata taratibu, ulikuwa na mkataba wa ujenzi, kulikuwa na Kampuni moja inayoitwa *KOI* hapa nimefungua kidudu changu kwa sababu baada ya kupata anuani yake nimemwambia anitumie *document* zinazohusu mkataba wa ujenzi ule. Kwa mujibu wa *data* zilizokuwepo hapa mkataba umekwenda kama ulivyotakiwa, yeye anasema anavyojua ana *certificate* mpaka *certificate* ya mwisho amelipwa mjenzi milioni 105. Sasa mnaposema kalipwa

milioni 25 hii imetoka kichochoro gani. Muda nilikuwa sina ilikuwa nizichape hizi *document* nisambaze na ikiwezekana kesho nitazisambaza ionekane.

Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa mjenzi halipwi mpaka yule mshauri a-*certify* kwamba sasa anaweza kulipwa na *certificate* zote humu zimo yule bwana lazieleza na ya mwisho anaijua kanambia, anajua mpaka shilingi 105 zimelipwa. Sasa kama huyo mjenzi alikuwa anadai pesa zaidi anasema labda kama *certificate* moja ya mwisho inaweza kuwa hajalipwa, lakini anachojua yeye kwamba kila kitu kilikwenda sana na *certified accordingly.*

Mimi siamini kwamba yule mjenzi ambaye ni mama mmoja ninamjua kuwa kalipwa shilingi 25 milioni nyengine hakulipwa, *document* zipo. Sasa uvumi huu umetoka wapi itakuwa labda kuna taarifa mbili zinazogongana na huu mkataba ulikuwa mwaka 2007 ukamalizika baada ya miaka miwili.

Jengo lile tuliangalie kama jengo la Mji Mkongwe tusilitizame kwa kuwa liko hospitali mkafikiri nalo linapata dawa lipone, nalo ni bovu kama yale majengo mengine ya Mji Mkongwe linahitaji kutunzwa, tangu kutengenezwa sasa ni miaka mingapi, mwaka 2007 mpaka sasa kama miaka sita lihoi la zamani hata babu zetu wengine walikuwa hawajazaliwa mana tangu elfu moja mia tisa na zero ni majengo ya kwanza yaliyojengwa hospitali ile. Hivi sasa linahitaji matengenezo zaidi.

Lakini kwa jumla kama huyo mjenzi anaamini kwamba ana deni anadai basi alete *document* kupitia kwa yule mshauri, suala hilo liangaliwa kwa hali hiyo. Lakini si vizuri kujaza uvumi ambao una ushahidi wa maandishi, inawezekana mimi niko *wrong* lakini huyo ndio Bwana tena yeye ni Mchungaji, anaitwa Mchungaji Justice mnaweza mkaona ni mtu wa kiasi gani wa kuamini hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, tuna tatizo la kijamii kwa vitu vyote na tabia. Wazanzibari tuna tabia ya kujenga kipya na kutengeneza kibovu, hatuna tabia ya kutunza kinapokuwa kipya kisiwe kibovu. Hiyo moja inaitwa *preventive maintenance* hatuna na matokeo yake vitu vingi tunavyonunua hatuna mikataba kwamba bwana unatuuzia hizi ndudu tunazozisemea hapa lakini kila baada ya miezi sita uje uzi-*service*, sina hakika hapa kwamba upo mkataba huo kwa sababu si kawaida yetu. Unanunua mashine hizo *X-Ray*, ma-*scanner,* madudu gani sijui yaliyokuweko kule, ukishanunua ushanunua ilikuwa tutie mkataba kwamba kila baada ya muda fulani uje ufanye maintenance tunangoja mpaka lisha *collapse* aa, tunaanza kumtafuta ee bwana wee basi njoo haraka anakuja kwanza hajui, lazima tubadili tabia. Tabia yaku-*preventive maintenance* hatuna. Mhe. Mwenyekiti, mikataba yetu mingi ya ujenzi, ya vitu kununua haiku hivyo.

Kulisemwa suala nadhani Mhe. Ismail Jussa la kwamba Ubalozi wa India wa Tanzania tunapopeleka wagonjwa tunakuwa hatushirikiani nao. Inawezekana, mimi bado sina taarifa hiyo ingawa nasikia kuna barua zinakuja, lakini tumelichukua suala hilo na tutalishughulikia ipasavyo kwa kushirikiana. Sisi tunachofanya tuna utaratibu wa kupeleka wagonjwa baada ya kutiliana *memorandum of understanding* na zile hospitali na tukishampa barua mgonjwa na wafuasi wake tunampa na barua anakwenda kwenye hospitali, akifika kule uwanja wa Ndege anapokelewa na hospitali moja kwa moja anakwenda hospitali.

Ni kweli inapotokea matatizo kwa mgonjwa yule hasa wale wanaokwenda wenyewe anakuwa hana pa kushika, inakuwa ni hospitali na yeye mwenyewe. Na tumeshapata kesi wanakufa watu wetu wa Zanzibar wamekwenda wenyewe hospitali inatwambia kuna maiti yenu hapa tufanye nini, wakati huo tena wenye maiti ndio wanaanza kuijua wizara. Kwa hivyo, ina maana katika hali ile ndio mara nyengine tunaushirikisha Ubalozi, si vizuri tulikuwa tushirikishe Ubalozi tangu mwanzo. Hilo tumelichukua na tutalishughulikia.

Lakini pia kulisemwa suala la Hospitali ya *MIOT* na Mhe. Ismail Jussa kwamba labda wagonjwa wetu hawashughulikiwi. Bado hatujapata malalamiko hayo na kama yako malalamiko hayo basi tunaomba tuletewe *officially*. Lakini kwa kawaida Hospitali ya *MIOT* ni moja katika hospitali zilizokuwa tunahudumiana wagonjwa muda mrefu sana. Kwa taarifa yenu hata baadhi ya wale viongozi waliomo Wizara ya Afya wanakuwa na ndugu zao na wagonjwa na wao huenda huko huko, kwa hivyo wasingekwenda huko ila kwa kujua kwamba ile hospitali ina huduma nzuri. Inawezekana kwamba imetokea kesi moja au mbili, lakini tunaomba tuarifiwe ikiwezekana tuzifuatilie.

Mhe. Mwenyekiti, kulizungumzwa suala la *Call allowance*, kuna *call allowance* na *risk allowance. Call allowance* inapata madaktari wa zamu wanaoitwa kwa kutokea kesi za dharura haipewi kila mtu. *Nurse* hapewi *allowance* ya *call*, *nurse* wanakuwa kwenye *shift*, wanakaa *shift* ya masaa manane wanakuja wenzake na kila baada ya wiki huwa wanapata *off* nadhani siku moja au mbili, ni sehemu ya kupata yeye kupumzika ili aingie *shift* nyengine.

Risk allowance ni *allowance* kwa sababu unafanya kazi kwenye mazingira magumu, hilo ni suala tulilokuwa tunalishughulikia sasa mwaka huu na tumeshafikisha taarifa kwa Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora hatujapata jibu. Kuna na *allowance* nyengine vile vile lakini nadhani ni suala la uchambuzi baina ya sisi na utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, kulitajwa wizi wa ma-*gril*, kweli jamaa mmoja alijiona mwamba akenda akakata *grill* zilioko kwenye jengo la Mkemia Mkuu pale Maruhubi, sikwamba iko nje imewekwa aa, kenda kuikata iko kwenye dirisha kwa msumeno na mashine. Sisi tukashtaki tukawapelekea habari polisi, kesi iko polisi hatujaitwa Mahakamani kutoa ushahidi. Sasa kama tutaitwa tutaeleza Mkurugenzi wetu wa *Chief Chemist* hapa atakwenda kueleza kwamba hapa pamekatwa, lakini vyenginevyo hatuwezi kusema kwamba kesi ile ya wizi tusimame vipi, kesi iko polisi na nadhani na polisi ndio itakayoweza kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, karibu namaliza kwa sababu nilitaka kufanya hivi kusudi ili nisiweze kujibu suala moja moja kwa sababu ni mengi. Pia kulitajwa habari ya Nyumba ya Lishe Pemba, nyumba ya lishe Pemba iko katika Hospitali ya Wete, Hospitali ya Wete hivi sasa inafanyiwa matengenezo kutokana na mkopo wa ADB na kile kidudu kimo mule nacho kitashughulikiwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alizungumza sana kuhusu chombo cha kufanyia uchunguzi wa *cancer*. Ni kweli kuna chombo fulani kilikuja kwa matumaini ya hivyo kikakaa kwa muda kukakosekana kitu kimoja ambacho ndio hicho alichosema kimeambiwa kimesagika. Kilipokosekana hicho kimefuatiliwa na mtaalamu yule alikuwa bado yuko masomoni, kimefuatiliwa hatujakipata mpaka sasa. Kuna njia mbili, kuacha ile tukanunua mashine mpya, lakini nayo mashine yenyewe vile vile sio rahisi.

Lakini suala la kufurahisha ni kwamba pale Dar es Salaam mpaka sasa katika kituo cha *censor* kiliopo pale *Ocean Road* hatujapata matatizo ya mashirikiano, ni kweli kuwa mbali, lakini utaalamu wa pale na madudu ya pale ni madudu ambayo yanahitaji fedha nyingi sana na wagonjwa wa pale wanahudumiwa bila ya matatizo kama vile wanavyohudumiwa wa pande nyengine. Tukipata nafasi tutaweza kununua chombo hicho katika huko tunakokwenda kwa kuifanya hospitali yetu iwe ya rufaa ya Zanzibar.

Pia yalitajwa ma-*ambulance*. *Ambulance* la Wete lipo likapelekwa na jengine Makunduchi tumepata mawili tumeomba na mengine kutoka *UNFPA* tutakapopata tutapeleka mule mwengine.

Mhe. Saleh Nassor Juma alizungumza habari ya usalama wa wafanyakazi wanaoingia *shift* ya usiku pale Mnazi Mmoja. Ni kweli, ukitoka pale Manazi Mmoja ukifika hata Darajani giza pana miti mingi kweli kwa kijana mtanashati anayetoka saa tatu na keshavua sare za *nurse* vijana wa mjini wanaweza wakamshughulikia. Ni suala linalosikitisha wala hatulifurahii. Na wakati fulani nilikuwa nimeshapata ufumbuzi lakini ukanishinda kwa sababu ya fedha.

Ilikuwa tununue basi ili wafanyakazi wote wa Mnazi Mmoja wawe wanachangia senti fulani liwe linawachukua sio lazima usiku tu, hata wale wanaokuja asubuhi, tunafanya *route* kama ni Jang'ombe, Kidongo chekundu, wapi mpaka Bububu linawaleta na saa saba linawachukuwa linawarejesha ukiwa unakaa kichochoroni utakaa *main road*, sikufanikiwa. Sasa kama kuna tajiri hapa anaweza kutusaidia hilo hadi sasa mpango huo ninao na nilizungumza na uongozi wa Mnazi Mmoja ukakubali kuweza kushirikiana na sisi kwa hilo. Ni kweli si vizuri wafanyakazi wale saa tatu ya usiku kukimbilia Darajani mara nyengine daladala ya Jang'ombe na mgurunyembe huko hakuna tena inakuwa kidogo ni tabu sana. Tunashukuru Mhe. Saleh kwa kutupatia ushauri huo.

Kulitajwa dawa ya UKIMWI kwamba ni haba. Zilikuwa ni haba wakati ule ambapo dawa zilikuwa hakuna, lakini sasa zipo na zinakuja kwa wagojwa wanaohusika, si dawa kama vile dawa nyengine kwamba kila mtu apate.

Mhe. Mwenyekiti, ilitajwa Ofisi ya Tiba Asili hawana ofisi, wana ofisi nzuri kuliko mtoto bikra, mana lile jengo la madawa pale kulikuwa na ofisi ya Mfamasia Mkuu pale chini walikuwa na wale watu wa Bohari Kuu wanakaa pale, wamehama wamepata jimbo lao Maruhubi wale watu wa tiba asili wako pale. Hivi sasa watu wa tiba asili wana ofisi nzuri kuliko maafisa wetu, kama hilo mlielezwa labda wakati huo walikuwa hawajahamia.

Maombi ya ajira, wengi walisema vipi. Kwa jumla tumepata nafasi 809 kati ya mwaka 2011/2012 na 2012/2013 kuajiri, tumeruhusiwa wakiwemo wale wanafunzi wanaotoka Vyuo vya Mbweni.

Uchunguzi wa maradhi alisema Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi. Kazi hii inafanywa tangu mwaka 2008, wanakuja Waspain pale wanapasua mifupa, wanapasua magoti, wanapasua mpaka vichwa, inaendelea bwana na umeshafanywa uchunguzi huo tangu hapo na inajulikana aina gani ya maradhi, kama unalo tatizo hilo onana na Naibu Waziri wangu akushauri na akuongoze.

Mhe. Ali Salum Haji alisikitika sana na suala la watu wanaoingia kutizama wagonjwa wao. Naomba niseme na mimi hili linanisikitisha na hata juzi kwenye bangokitita nimelizungumza na Rais, tumefika *stage* sasa hata yale masharti na utaratibu wa hospitali tunashindwa kuuheshimu. Hivi sasa tunapata tabu na wafanyakazi wetu wanapata tabu, inalia kengele ndio kwanza bibi kaweka 4 juu ya kitanda cha mgonjwa hana habari kwamba wakati umekwisha, tunalazimisha mpaka tutumie nguvu ambapo hatutaki, lakini tunafanya utaratibu kuweza kuondoa hali hiyo.

Tuliomba tujenge kituo cha kuegezea au kungojea wagonjwa nje kwenye bustani pale, lakini watu wa Baraza la Mji kwa kutunza mazingira yao na Mhe. Waziri atanisaidia labda walikataa tusijenge banda pale, lakini dhamiri tujenge pale banda ili wagonjwa wale watizamaji wakitoka pale wana-*cross* kuingia huku hospitali wana na vile vijipande viwili kama zamani na ikifika saa 11 au saa moja ya asubuhi ikilia kengele ni rahisi kuwaambia watu toka. Hivi sasa kweli tuna tatizo hilo. Ukienda pale kwenye Idara ya Wazazi wanapozaa kinamama utafikiri uko kwenye soko la samaki, humjui nani mgonjwa, humjui nani kaja kutizama, humjui nani kaja kuza ilimradi ni balaa tu. Kwa kweli linasikitisha sana na halifurahishi katika jamii ya kiungwana kama ya Kizanzibari. Tunavishughulikia.

Naomba Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa mambo mawili, wale wengine masuala madogo madogo niliokuwa sijamaliza wataniwia radhi na ikiwezekana basi waniulize pembeni.

Mhe. Jussa alizungumza kwa hamasa sana kuhusu bajeti kwamba ndogo inakuwaje. Katika ile *document* naomba nisahihishe jambo moja walichokosea, walichukua hesabu za kipindi kimoja wakakifanya cha miezi sita. Waliandika kwa kipindi cha miezi sita Julai/Disemba fedha ni hizi, kumbe zilikuwa ilikuwa za *quarter* moja, lakini kwa kweli ilikuwa itizamwe kuanzia Julai mpaka Disemba ile walichukua ilikuwa ni Oktoba mpaka Disemba. Sasa ukweli ukoje kuhusu bajeti? Ukweli ni kwamba Julai/ Septemba tulipata pesa shilingi bilioni nne na ushei, Oktoba/Disemba tulipata shilingi bilioni tatu na milioni mia tisa, jumla shilingi bilioni nane na ushei, total ya bajeti yetu ilikuwa ni shilingi bilioni 18. Kwa hivyo, Julai/Disemba sio ile 13 aliyoisema Mhe. Jussa ila ni asilimia 47 kwa miezi sita.

Lakini hadi mwezi wa Machi bajeti yetu ya kawaida tumepata asilimia 56. Hizo bajeti za kawaida. Bajeti ya maendeleo haijaonesha sura nzuri tumepata asilimia 15.6 tu. Kwa hivyo, miradi mingi haijafanya vizuri. Na bajeti ya wafadhili tumepata asilimia 58. Hiyo ndio hali halisi, nilitaka niseme tu kwamba hivi ndivyo tulivyoweza kupata hizo pesa. Ni kweli ni finyu na yale tulioweza kufanya tumeweza kfuanya. Juzi tumewasilisha ripoti yetu mbele ya Rais na ameona yote haya na huo ndio uwezo tulioweza kupata, tungepata zaidi tungefanya zaidi. Kwa hivyo, mara nyengine tunapolaumiwa tulaumiwe na hali hiyo halisi tuliyonayo, ndio hali ya nchi ilivyo na ndio hali ya uwezo.

Sasa Mhe. Jussa alisema kitu kimoja pale kwamba huyui Babu Juma alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa *CUF* na tunajua utendaji wake. Sidhani kwamba nahitaji kulijadili lakini mwalimu hupimwa na wanafunzi, wanafunzi ndio wanaoweza kusema huyu mwalimu mzuri, tofauti ya Juma Duni wa sasa na wa *CUF* ni kwamba kule nilikuwa mimi ndiye mtendaji hivi sasa mimi ni msimamizi na mambo mengine yako nje ya uwezo wangu, kama nimepewa nitafanya mengine yako ndani ya uwezo wangu. Nakubali lawama zote, nakubali upungufu wangu wote

uliokuwepo, lakini najitahidi pamoja na wenzangu na naomba kuthibitisha kwamba hakuna anayenikandamiza au kuni-*sabotage.* Tunajitahidi kufanya na kwa kweli nina wataalamu wazuri sana tena wenye uwezo ambao wanashirikiana na mimi kwa kila hali. Lakini sasa yale yanayokuwa nje ya uwezo wangu ndio yako nje ya uwezo wangu.

Bahati nzuri Mhe. Mwenyekiti, nipate kuondoka nimefanya kidogo mambo ya *economics* ingawa si *professional* kama kina Mhe. Omar Yussuf na wengine. Kwenye uchumi tunasema kuna vitu viwili, *ability to pay and willingness to pay*, uwezo wa kulipa na hiari ya kulipa, mengine sina hiari nayo. Ahsanteni.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kufafanua mawili matatu ambayo yaligusiwa katika wizara yetu. Mhe. Mwenyekiti, jambo moja kubwa ambalo lilijitokeza hapa na kuzungumziwa na Waheshimiwa wengi akiwemo Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Salum Abdalla Hamad na Wawakilishi wengi ni suala la deni ambalo tunadaiwa na Baraza la Mitihani.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Wawakilishi walisema kwamba deni hili ni kubwa na mimi nataka nikiri kuwa ni kweli lakini linatokana na hali halisi ya bajeti ambayo tunayoipata. Kwa mfano, katika mwaka 2011/2012 Baraza la Mitihani la Zanzibar lilitengewa jumla ya shilingi 1,382,000,000 kwa ajili ya shughuli zote za mitihani ya taifa ya SMZ, mitihani ambayo inahusu *Form* II na Darasa la Saba. Pesa hizo hizo ni kwa ajili ya mitihani yetu ya *Form* IV.

Mhe. Mwenyekiti, katika pesa hizo matumizi yake ambayo tulitumia ni kama hivi ifuatavo:-

Mitihani ya Darasa la Saba na ya *Form* II tulitumia jumla ya shilingi 1,310,409,173. Tukalipa deni la mitihani ya *Form* IV ya mwaka 1998, jumla ya shilingi 70,000,000,572, tukalipa tena deni la mitihani ya *Form* IV la mwaka 2010 hizi ni zile ambazo zinabakia baada ya malipo ni shilingi 159 milioni laki 5 na shilingi milioni 590, jumla ya matumizi yote ni shilingi 100,255,551,176; fedha ambazo zilibakia katika pesa ambazo tulitiliwa na bahati nzuri tulipewa kwa asilimia mia ni shilini milioni laki moja na ishirini na sita, mia nne na arobaini na sita, mia nane na kumi na tano, hizi zikabakia Mhe. Mwenyekiti, kwa matumizi ya ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, kati ya shilingi milioni mia moja na laki tano kwa mwaka 2012/2013 shilingi milioni sabini na tisa, mia saba na ishirini na nne, laki tano na arobaini na sita zililipwa kupunguza deni la mitihani ya *Form* IV ya mwaka 2011, ambapo jumla ya deni hilo ni shilingi milioni mia nne na thalathini na nne, mia tisa na tisini. Dini lililobaki la mwaka 2011 ni jumla ya shilingi milioni mia tatu sitina na tatu, laki nane na kumi na nane.

Mhe. Mwenyekiti, deni la mitihani la *Form* IV la mwaka 2012 ni shilingi milioni mia nne thalathini na nne, laki nane na sitini na tano. Katika fedha za mwaka 2012/2013 zimebakia shilingi milioni mia nne na sabiini na mbili tu, kama tutazipata fedha hizi tunaweza kulipa shilingi milioni mia nne na hamsini tu, ili kukamilisha deni la mwaka 2011 na kuanza kulipa deni la mwaka 2012.

Mhe. Mwenyekiti, imebidi nizungumze hivi ili wenzetu wa Baraza la Wawakilishi waone ni hali gani ambayo tunayo ya fedha. Tuna hali ngumu Mhe. Mwenyekiti, na kama binadamu basi

hatupendi tuwe na madeni kama haya, lakini inatubidi tuwe nayo kutokana na hali ya bajeti nzima ambayo tunayo. Na hili nataka niliunganishe na lile suala ambalo lilichukuwa nafasi kubwa ya kuzungumzwa na Waheshimiwa wa Baraza lako hili tukufu linalozungumza juu ya usahihishaji wa mitihani.

Hiki Mhe. Mwenyekiti, ambacho nilikieleza shilingi bilioni moja, milioni mia tatu na thalathini na mbili ndio pesa hizi hizi ambazo tunatumia kwa ajili ya matumizi ya mitihani yetu ya darasa la Saba na la Kumi. Na ndio maana Mhe. Mwenyekiti, huwa tunajaribu kupunguza matumizi, suala la usahihishaji wa mitihani hautegemei uwiano wa walimu kutoka Pemba au Unguja, kutoka Kusini au Kaskazini au Mjini. Ukitizama hasa utaona walimu wengi ambao tunawatumia katika kazi hizi ni walimu karibu asilimia arobaini wanaotoka Mjini Magharibi. Kwa sababu hawa huwa hatuwagharamii zaidi ya ile posho ya usahihishaji, lakini ukichukua mwalimu kutoka Pemba au Kusini mzigo unakuwa ni mara mbili kwa sababu inabidi uwalaze na uwape chakula, mbali na nauli yao ya kwenda na kurudi ambayo inatumika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kupitia Baraza lako kuwaomba Wawakilishi hii isiwe *issue,* kwa sababu mwisho itakuja kuonekana kama Wizara ya Elimu labda inabagua Wapemba. Kwa sababu suala hili nilijibu katika swali mama Nam. 79 kipindi kilichopita, nikajibu tena swali hilo hilo Nam. 120; tukalijibu tena swali hili na waulizaji ni hawa hawa ukimuacha Mhe. Ismail Jussa yeye kaliuliza jana na alitaka ufafanuzi kwa sababu aliliona katika kitabu, tukalijibu kwa upeo mkubwa na tukaahidi kama kadri ya fedha zitakavyoingia basi tutajaribu kuongeza na kwa mwaka huu tumeongeza kutoka asilimia ambayo tumechukua mwaka juzi na tuliyochukua mwaka huu ni tofauti, tutaongeza kila hali itakavyoturuhusu katika bajeti. Wenzetu watuone kwamba tuna mzigo mkubwa katika hili na hatuna nia ya kubagua.

Mimi mwenyewe Mhe. Mwenyekiti, ni Mpemba kindakindaki nisingekubali kuona kama kuna ub aguzi ndani ya wizara yangu kubaguliwa Wapemba wakati mimi mwenyewe ni Mpemba, hili ningelisimamia Mhe. Mwenyekiti.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumze kwa haraka haraka ni lile suala la kusikitisha ambaloo kila Mzanzibari limemgusa la kufeli watoto wetu. Waheshimiwa wengi walichangia suala hili na kama tunavyojua kumeundwa kamati, lakini mbali ya kusubiri kamati maelezo ambayo watatuletea lakini kama alivyojibu Waziri wangu hapa juzi kuwa wizara tumekusudia kufanya mdahalo wa Wazanzibari wadau wa elimu ambao utawahusisha wadau wengi, tujue ni wapi ambapo tumejikwaa bila ya shaka mtu mwenyewe hawezi kujiona alivyo, anaweza kuona kama anafanya kitu kizuri lakini kukawa kuna mapungufu ya hapa na pale.

Kwa hivyo, hili kama Mhe. Ismail Jussa alivyosema kuwa tulifanyia haraka naahidi tutajitahidi kulifanyia haraka nia ya watoto wetu na sisi wazazi ni kuwa wasome.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho ambalo nataka nichangie ili kuokoa muda wako ni lile suala ambalo lilizungumzwa kuhusu skuli zetu hizi nane ambazo tayari tumezifungua tunaziita za *World Bank*. Mhe. Asha Bakari alisema kwamba skuli hizi zimejengwa mbali na maeneo ambayo wanakaa watu, hatukuzingatia ni sehemu gani ambazo tunajenga skluli hizi.

Mhe. Mwenyekiti, kwana si Wizara ya Elimu peke yake ambayo ilikaa na kuamua skuli hizi zijengwe wapi, lakini

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tujitahidi kumsikiliza Naibu Waziri ili tuweze kusikia namna hoja zetu zinavyojibiwa na tumpe nafasi ili amalizie vizuri.

.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Tulikusudia skuli hizi ziwe ni skuli za wilaya na mwanzo hasa tulikusudia ziwe na dakhalia na nyumba za walimu. Lakini kutokana na ujengaji ule na makisio yetu kuchelewa ikabidi makisio ya ujenzi yakawa makubwa, kwa hivyo zile dakhalia hatukuwahi kujenga.

Lakini tunafikiria na tupo katika matayarisho na tumeanza kuwaandikia wenzetu wa *World Bank* juu ya skuli hizi kujengwa dakhalia. Nia ya skuli hizi Mhe. Mwenyekiti, ziwe ni skuli za wilaya na matarajia yetu ni zile cream ambazo zitatoka katika maskuli yetu mbali mbali ya mawilaya yetu, basi waingie pale wasome uzuri na kwa nafasi.
Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kumalizia kujibu au kusawazisha michango iliyotolewa na Wajumbe wa Baraza hili tukufu.

Naomba nianzie na mimi kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai uzima leo tukafika kwa pamoja tukatekeleza hii kazi ambayo tumepewa na wananchi wetu waliotuchagua.
Mhe. Mwenyekiti, shukurani za pekee zimwendee Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kipindi kifupi kidogo tulim-*miss* kutokana na hali yake. Na mutakumbuka kipindi kimoja nilikuja hapa nikatoa tamko la kumuombea dua mwenzetu kutokana na maradhi yaliyomsibu. Leo sote tunafurahi kumuona leo tunaye na kama kawaida yake michango yake ni ya kina na tumeifahamu.

Kwa kweli sina haja ya kurejea tena kwa yale maeneo aliyochangia kwa sababu amechangia vizuri, amekwenda katika zile *details* zinazohitajika, mimi nitakwenda katika michango mengine.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu ilipata hoja tano au maagizo matano ya kuyafanyia kazi. Lakini nathubutu kusema kwa umuhimu wa wizara hii waliochangia ni watu wengi. Ni watu 13 na 3 wamechangia kwa maandishi.
Nashukuru sana kwa michango yote iliyochangiwa hapa na nataka niwaahidi kwamba ule ushauri wote uliotolewa nimeupokea na sitaki niukalie, hapana nitaufanyia kazi na matokeo yake tutayaona. Naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka niwataje wale ambao kama kuwatambua waliochangia.

1. Mhe. Hija Hassan Hija

2. Mhe. Asha Bakari Makame

3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu

4. Mhe. Saleh Nassor Juma
5. Mhe. Ashura Sharif Ali
6. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
7. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
8. Mhe. Salum Abdalla Hamad
9. Mhe. Panya Ali Abdalla
10. Mhe. Ali Salum Haji
11. Mhe. Rufai Said Rufai
12. Mhe. Nassor Salim Ali

Waheshimiwa waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Ussi Jecha Simai wa Jimbo la Chaani na yeye amenihimiza tu nimsaidie katika kukamilisha zile skuli ambazo wananchi wake wamezijenga. Nampongeza sana ana skuli tano, nyengine ni banda moja moja na nyengine banda mawili na nazijua zote. Wakati ukifika hivi sasa kidogo hali ya bajeti si nzuri na bado kuna skuli nyingi kubwa, lakini nataka nimuhakikishie kwamba nitalitekeleza suala lake kwa nguvu zangu zote.

2. Mhe. Marina Joel Thomas nataka nikuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba nimeupokea, ni mzuri sana na nitahakikisha kwamba nitauweka na kuutekeleza.

3. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, huyu amechangia uzuri sana na mchango wake nimeupokea kwa mikono miwili.

Baada ya utangulizi huo sasa nataka nikuhakikishie Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mchango alioutoa Mhe. Naibu Waziri nitakuwa na machache sana ya kuyazungumza.

Kwanza nitazungumza yale ya jumla ambayo ni muhimu sana na ikisha nitawajibu wale wachache ambao Mhe. Naibu Waziri hakuwajibu au hajawatolea michango yao au hajayatolea ufafanuzi wa michango yao.

La kwanza ni suala kufeli kwa watoto wetu wa *form four* katika mtihani wao wa mwaka huu. Mhe. Mwenyekiti, naungana na wenzangu wote kwa masikitiko yaliyotukumba Zanzibar hii, lakini naweza kusema hata Tanzania kwa jumla ya watoto wetu wengi sana kufeli. Asilimia ya waliyopasi *grade one, two and three* hawafiki hata asilimia 40.

Ni ajabu lakini ni kweli. Mhe. Mwenyekiti, bado Zanzibar tunahusika kwa sababu *NECTA* ni shughuli ya muungano. Inawajibika au tunawajibika kulibeba suala hili na kulitafutia ufumbuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe ali-*pause question* akasema kwa nini tunaubeba huu mzigo wa *NECTA* kwa nini hatujitoi. Mimi namuunga mkono katika hili kwa ile kauli aliyoizungumza Mwenyezi Mungu *Subhana Wataalla* akasema, "*walaa taziru waaziratun wizra ukhra".* Hatobeba mbebaji mzigo wa mwenzake na mimi katika hili linaniwia gumu sana kulibeba lakini twende nalo pole pole, *in shaa Allah* wakati utafika.

Nimeeleza wakati najibu maswali mbali mbali, matatizo tunayopata na *NECTA* ya kubadilisha viwango vya wanafunzi wetu kufanya mitihani, kubadilisha tarehe ya kufanya mitihani, hata kubadilisha zile *passing marks* za matabaka mawili, ile *writing examination* na ile ya mwaka mzima uliofanyia, kama ni *homework*, *test*, nini, zamani ilikuwa ni *fifty percent* hii na *fifty percent* hii.

Ghafla bila ya kushauriana na bila kukubaliana wamesema mwaka huu *passing marks* kwenye *writing* itakuwa ni *seventy percent* na zile za mwaka mzima zitakuwa *thirty percent*. Kwa kweli wanafunzi wetu walibabaika sana. Maana kwa muda wote wa zaidi ya miaka minne, mitano sita walikuwa wanajiandaa kwa *ratio* ya *thirty to seventy*. Ratio imebadilishwa ghafla.

Kwa hivyo ni kweli kabisa mizigo tunayotwishwa ni mikubwa na si yetu, lakini ni yetu kwa sababu hili ni suala la muungano. Sasa nimeona lizungumze hili kwa urefu kidogo. Waziri mwenzangu amekuja mara mbili na mimi nimekwenda mara moja wizarani kwake kuyaondosha matatizo madogo madogo kama haya.

Mara ile nilipokwenda mimi Dar es Salaam niliona aibu, wizara anauliza watendaji wake hili nyinyi munalijua la kubadilisha tarehe za kufanya mitihani na kubadilisha viwango vya watoto wanaopasi wanaoruhusiwa kufanya mtihani wa *form six.*

Mhe. Mwenyekiti, hakuna aliyekuwa anajua katika wale wakubwa waliokuwepo pale; alikuwepo Naibu Katibu Mkuu na alikuwepo Kamishna. Mhe. Mwenyekiti, tulilimaliza suala lile kwa kujibu masuala matatu, unataka tufanye nini. Kwanza nataka wanafunzi wetu wote wanaofanya mtihani wa *form six* wasamehewe kutokana na kiwango kile kile cha tokea mwanzo. Kwa sababu kumchukua mwanafunzi aliyeingia *form four*, akatoka *form four* sasa akapasi akaingia *form five* kwa *passing* zile zile akaingia *form six*, sasa yupo tayari kufanya mtihani unambadilishia viwango, haiwezekani. Tukakubaliana, tukaja la pili tukasema naomba kuanzia leo tunapotaka kubadilisha mambo mazito tukutane kwa pamoja na tuamue kwa pamoja, la tatu nikasema hata mitihani ya mwakani, mwaka huu *form six* si wameshafanya basi mwakani wafanye kwa viwango vile vile tunavyovitambua tokeo mwanzo wasibadilishe. (*Makofi*).

Kilichofanikiwa ni watoto wetu kufanya mtihani mwaka huu na bila shaka mwakani watafanya mtihani, lakini wenzangu wanakimbia kukutana pamoja ili kuzungumza. Mhe. Waziri Kawambwa namshukuru sana na nampongeza sana ni mwepesi sana kukutana na mimi na wafanyakazi wangu na Wakurugenzi wangu, ni mwepesi kujadili mambo yetu kwa utaratibu na mwepesi kukubaliana na ushauri wetu.

Lakini nasikitika sana wengine hawapo hivyo, wanaburura, wanatulazimisha na kibaya zaidi wanaamua, badala ya kutuandikia sisi wizara wanawaandikia Walimu Wakuu wetu. Hizo ni *protocol* ambazo ni za kienyeji kabisa na wala hatuzielewi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, niliona nilizungumze hili kwa urefu kidogo ili libakie katika *hansard* lakini vile vile wenzangu walioko huko walisikie. Tuna upenda muungano, tunautaka sana muungano lakini tunataka *fair contribution* ya mambo yetu na sio mambo ya kulazimishwa na kuburuzwa buruzwa na wakati ukifika wenzetu tutawaeleza. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine nalotaka kulizungumza ni lile ambalo Mhe. Asha Bakari Makame alilizungumza. Bahati nzuri Naibu Waziri ameligusia. Nataka niliongozee kidogo. Skuli hizi zote ni 19 tulizowahi kuzimaliza na kuzifungua ni 8 Unguja na Pemba.

Tulikaa tukaamua tujenge Matemwe, tujenge wapi kwa lengo la kwanza *population* ya pale tunapojenga lina watu na sio kama alivyozungumza mheshimiwa. Lakini la pili kama alivyozungumza Mhe. Naibu Waziri hizi skuli ni za wilaya. Wilaya popote tutakapojenga kwa sababu ni wilaya, wanafunzi watafaidika kuzitumia.

Lakini la pili, ili kwamba tumeshindwa kujenga hizi nyumba au nyumba za kulala wanafunzi kwa sababu ya bajeti yetu. Tumelazimika kupunguza bajeti, kufanya yale yaliyokuwa ni muhimu na makubwa ili tukizifungua skuli tuwe tumezifungua skuli zilizokamilika.

Nataka niliarifu Baraza lako hili tukufu Mhe. Mwenyekiti, skuli zetu zimekamilika, zina walimu wazuri na tumeweza kujenga nyumba tatu katika kila skuli ya kuwaweka walimu wetu. Bado tuna deni la kujenga nyumba saba katika kila skuli na tuna deni la kujenga nyumba za kulala wanafunzi wetu.

Kama alivyosema Naibu Waziri tumeshazungumza na *World Bank* wafadhili wetu waliotukopesha pesa sio kidogo dola nyingi sana tukaweza kuzitumia kujenga skuli zetu hizi.

Mhe. Mwenyekiti,katika ufunguzi wa skuli hizi tulialika watu mbali mbali, tulialika waheshimiwa mbali mbali kutoka Bara na kila aliyekuja alisema hapa mumeukata Wazanzibari, kwa skuli hivyo walivyoziona, nyumba walivyoziona za walimu na tumekwenda Matemwe Kilimani kufungua skuli ile tulimualika mwenyewe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Alipata bumbuwazi zile sifa alizotumiminia wengine tulishindwa kuzibeba na hususan alisifu sana ujenzi wa nyumba za walimu, hata akathubutu kuchukua ramani ili na wao wakipata fursa kama hii waitumie.

Kwa hivyo nasema tushukuru na tupongezane kwa juhudi tuliyoichukua ya kufika pahala pa kuzifungua skuli 8 hizi muhimu na sasa hivi zina wanafunzi tayari wanasoma. Maabara zipo 3, biolojia, physikia, chemistry, kuna maabara ya kompyuta na kuna kila skuli ina maabara au ina chumba cha vitabu, chumba kizuri sana na vitabu vipo vingi. Na *Inshaallah* panapo uhai na uzima mradi wetu tutaumaliza siku chache zijazo kabla ya mwaka 2015 tutakuwa tumeshamaliza ujenzi wa mradi wetu huu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nassor Jazira Mhe. Naibu Waziri ameshajibu lakini nataka nigusie kwamba wakati nazungumza hivi sasa mabati 30 yameshapelekwa pale skuli kwa kuziba ziba yale mapengo yanayovuja ile skuli, lakini inshaallah penye uzima mwakani tutaongeza mahitaji ya bajeti yetu ili kuzimaliza hizi skuli zilizojengwa na wananchi.

Nikimjibu Mhe. Nassor pia nimemjibu Mhe. Mwakilishi maarufu anayeitwa Bhaa, Mhe. Ibrahim Makungu na yeye tutakuwa tumemjibu katika suala lake hilo hilo la skuli zenye matatizo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameshajibisa na Mhe. Naibu Waziri na sina haja ya kuongezea zaidi kuliko alivyomjibu Mhe. Naibu Waziri, lakini lile alililozungumza kuhusu mzigo aliohusia kwamba tumetwikwa na *NECTA* pia nimeuelezea na *Inshaallah* tutautua.

Mhe. Mkereketwa rafiki yangu Sheikh Saleh Nassor Juma, huyu namwita mkeretwa tuna *history* baina ya mimi na yeye katika chama chetu cha zamani cha Afro Shirazi. Bahati mbaya hayupo hapa kama angelikuwepo angelitikisa kichwa ku-*approve* hii *statement* yangu, yeye amekuwa mara nyingi akiliuliza swali hili la wale walimu waliopata mafunzo ya *education* ya sayansi na *mathematics* wakaajiriwa sasa hivi baada ya masomo yao, bado hatujawalipa mpaka leo. Asubuhi nilipokuwa najibu suala hili nililijibu vizuri sana na nikaweka wazi kwamba suala sio kama hatujawatengenezea malipo hapana, suala hatujaruhusiwa kuzitumia hizi pesa kuwalipa malipo yao lakini tumeshapeleka mahesabu yetu Tume ya Utumishi, tukipata kibali leo, kesho tunawalipa na iliahidi hapa nitalifuatilia tena hili suala, Katibu Mkuu wangu atalifuatila kwa Katibu Mkuu mwenzake na mimi nitalifuatilia kwa Mhe. Waziri mwenzangu. Na itakapoandikwa barua ya pili ya kulihimiza nitampelekea nakala kwa Mhe. Nassor na nitapeleka nakala kwa Baraza ili Wajumbe wote walijue, tuhakikishe kwamba hili suala tunalimaliza.

Kwa kweli linaumiza sana. Hawa wanafunzi wetu wamejitolea kujifunza zaidi, wanatusaidia kufundisha yale masomo ya sayansi ambayo tuna upungufu wa walimu. Sasa huyu amejitolea kusoma na akapasi, ukamuajiri kufundisha masomo ya sayansi lakini bado unasita *physical* kumlipa yale malipo yake yanayostahiki. Naomba sana na ninaahidi hili litalifuatilia na kulimaliza, hili sio tatizo kwa bahati mbaya ni kwamba limekaa kwa muda mrefu lakini sio tatizo la kuzungumza kila wakati.

Mhe. Saleh alizungumza suala la kamati zetu skuli jinsi zinavyorejesha nyuma maendeleo ya wanafunzi wetu. Hili tumelizungumza hata katika mkutano wa majumuisho na kamati hii ya Baraza la Wawakilishi. Nikapata agizo ambalo mimi nilikuwa tayari nimeshalifanyia kazi. Kasoro mbili ziliopo katika skuli yetu ya Haile Selassie, kasoro ya gereji bandia na kasoro ya jaa. Hili tumekuwa tumeshalifanyia kazi na ninamuahidi mheshimiwa hili suala si siku itabakia kwamba ni historia.

Tumeshaamua ile kamati iliyodumu kwa zaidi ya miaka 20 kamati ya skuli, kiasi ambacho wajumbe wengine wanatamba wanasema hakuna hata waziri mmoja anayeweza kuiondosha hii kamati. Kaja Waziri Mapuri hii kamati kaikuta hapa hapa, kaja Waziri Haroun kaitizama kaacha hapa hapa, kaja Waziri Abdalla Shaaban kaikuta na kaja Waziri Shamuna hivi sasa ataiacha uporo, hatutoiondosha kwamba basi, tutaiondosha kwa sheria na tutaichagua nyengine kwa sheria. Tunataka kamati zetu zitusaidie kama zilivyotusaidia kamati nyengine za skuli.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ashura ninafikiri jibu lake limejibiwa na Mhe. Naibu Waziri. Amelizungumzia suala la dakhalia limeshalijibu, amelizungumza suala la kuwapata walimu wawili wa umeme kuwapeleka ile skuli ya Kengeja. Nataka nimuarifu Mhe. Mwakilishi kwamba

si walimu wawili, ni walimu wanne, tumeshawachagua, tumeshawapata, tumeshapata kibali cha kuwaajiri na tunawapeleka Kengeja hivi sasa haraka iwezekanavyo.

Ni kweli kabisa Skuli ya Kengeja ina kasoro lakini wakati tunajibu masuala tulieleza nini tumefanya na kasoro nyingi sana tumeziondosha, iliyobakia ni ile kasoro ya kuwa na vitu vya umeme na hivi vitu pesa tumeshazipata tunazo na karibu tumeshatoa tenda, tukipata muuzaji mzuri mwenye bei nzuri, bei ya ushindani tutanunua vitu hivi haraka iwezekanavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mohamed Ali alizungumzia suala la uteuzi wa walimu wa kusimamia mitihani kutoka Pemba na Unguja. Suala hili Mhe. Naibu Waziri amelitoa ufafanuzi mzuri sana na sina haja ya kuongezea.

Mhe. Mwanajuma Mdachi ninakushukuru sana kwa mchango wako. Ulikuwa unatuhimiza kuhusu Skuli ya Paje Mtule, Tunguu na Fumba. Nilipokuwa najibu suala la msingi jana na hata leo, nilieleza zile hatua ambazo tulizozichukua tutakazozichukua. Nilieleza ile *penalty* tunayomkata huyu mkandarasi na labda leo niongeze kusema kwamba mkandarasi huyu aliingia katika tenda yetu ya ushindani. Huyu ni mama engineer, tena ni engineer mzuri. Huyu ni mwenyekiti wa Wakandarasi wa Tanzania Bara, ile jumuiya ya wakandatasi kule Tanzania Bara, yeye ndiye mwenyekiti wao.

Inasikitisha sana kwamba yeye ndiye aliyeshindwa na ameshindwa kweli kweli. Katika skuli hizi nimeshazitembelea mara nne na mara ya mwisho nilizitembelea wakati kamati siku ya pili yake inakwenda kutembelea lile eneo.

Nasikitika sana na nawaomba radhi Waheshimiwa wa kitaifa kwa ahadi waliyopewa na mama huyu, *engineer* huyu. Rais kenda katembelea katoa ahadi yule *engineer* atamaliza lini lakini hakumaliza, Makamu wa Pili kenda, katoa ahadi atamaliza lini lakini hakumaliza na hivi karibuni alikwenda Makamu wa Kwanza wa Rais, akasema tarehe 28 mwezi wa Februari atakabidhi skuli, mpaka leo.

Mhe. Mwenyekiti, nilikwenda kuzitembelea tena hivi karibuni hizi skuli. Skuli mbili mpaka wale ma-*contractor* wameshahama hawapo, Skuli ya Tunguu na Skuli ya Fumba hawapo. Paje Mtule kuna kazi ndogo ndogo za kugusagusa na kuna kazi ya kuchimba kisima cha maji. *Otherwise*, kwa jumla wanasema wamemaliza kwa asilimia 80 ya kazi, lakini kazi zilizobakia hiyo asilimia 20 ni kazi muhimu na ni kazi za ndani.

Natoa ahadi kwamba bado tutaendelea kusimamia na ile hatua niliyoizungumza juzi kwamba ikifika wakati tutavunja mkataba. Lakini kabla ya kuvunja mkataba nimeshaweka miadi na Mwanasheria Mkuu, amenitaka nimtengenezee *detail* zote, tunazitengeneza, tukiwa tayari tutakwenda kuzungumza na Mwanasheria Mkuu kutupa maoni yake. Tukivunja mkataba tufanye nini, twende vipi, kwa sababu tuna- *deal* na mtu, sitaki nimpe zile sifa za matusi, lakini ni mtu mkakamavu, ni mtu mjuaji.

Kwa hivyo, tusipokuwa *careful* anaweza, kwa mfano akaweka *court injunction* tukashindwa sisi kujenga hata kama tutamtafuta *contractor* mwengine tukashindwa kufanya hiyo kazi, badala ya skuli kumalizika, skuli zikabakia *white elephant* zimekaa tu pale. Kwa hivyo, tunataka tuwe *very*

careful kupita katika nyanja zote na tumeshakwenda *World Bank*, tumeshawaandikia matatizo na *World Bank* ndio tuliokubaliana ile *penalty* ya kumkata huyu mama pesa zake tuitumie, na ya ku-*terminate* mkataba tuitumie. Sasa sisi tunaiandikia *World Bank* ku-*extend* mkopo ili ukifika mwezi wa Julai, ambapo itakuwa ni muda mrefu sasa ule mkopo wetu uendelee ili tuweze kuwa na fedha za kuajiri *contractor* mwengine kumaliza shughuli zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema nieleze hayo vile vile kwa urefu kwa sababu masuala haya yameshakuja mara kwa mara kuhusu Mtule, lakini hizo ndio hatua tulizofikia. Naamini na nakubali Waheshimiwa Wawakilishi watanivumilia, wataniunga mkono na watanisaidia ili tuhakikishe skuli zetu zote 19 tulizokusudia kuzijenga zimalizike.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, pamoja na majibu mazuri, jitahidi kuzingatia muda.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Salim Abdalla Hamad, nafikiri umeridhika na jibu alilotoa Mhe. Naibu Waziri, alilitoa kwa urefu kidogo na kuhusu haya madeni kati ya wale wadaiwa wa bilioni 4 na wale wa bilioni 8 mbona kuna tofauti, tupe taarifa Mhe. Naibu Waziri amelieleza kwa ukamilifu.

Mhe. Panya nilikuelewa mchango wako, umeunga mkono na tumefurahi sana ni yale yale yaliyozungumzwa na wengine na mengi yao tumeshayatolea taarifa pamoja na yale yako.

Mhe. Ali Salum wa Jimbo la Kwahani suala lako ni zuri sana, hii skuli naijua na nimeshaitembelea mara mbili, ni kweli kabisa ni skuli yenye walemavu. Pale ndipo tulipoanzisha ile *project* ya TZ 21, kwa ajili ya kuanzisha mradi ule wa kompyuta kwa skuli zote za *primary*. Lakini *project* hii tulianza pale Skuli ya pale Kisiwandui na Darajani. Tulianza Kisiwandui kwa sababu ya kuwapa fursa wanafunzi wetu walemavu. Tunawasaidia sana na tunashirikiana nao sana. Hili sitaki nilizungumze nikaja nika- *commit* taarifa iliyokuwa sio sahihi, lakini nadhani yule mlemavu aliyeingia Chuo Kikuu, chimbuko lake ilikuwa ni ile Skuli ya Kisiwandui. Mhe. Ali Salum ana *note* kukubali kuwa ninayosema ni sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, huu ni mfano mzuri na tunamtumia sana huyu mwanafunzi kuwaelezea waathirika wengine kwamba wasikate tamaa huu ulemavu sio tatizo la kumalizika maisha yako, hapana. Tunashirikiana nao vizuri na tunawasaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mikopo ya elimu ya juu Mhe. Naibu Waziri amelizungumza vizuri. Ni kweli ina matatizo na matatizo yake ni ya muda mrefu. Lakini nina furaha kama nilivyoeleza juzi kwamba kutoka milioni 4 tulizozikusanya mwaka mmoja uliopita, nilizozitolea taarifa katika bajeti yangu hapa, sasa hivi tuko kwenye milioni 75 tumeshazikusanya. Hizi pesa sio kidogo, hatua tunazozichukua ni kushirikiana na wenzetu.

Tunashirikiana na hii taasisi ya watu binafsi, tunashirikiana na Tume ya vitambulisho vya Mzanzibari na kadhalika, ili kuhakikisha kwamba sio wafanyakazi wa serikali peke yake tunaowabana na kuwadai na kutulipa, lakini hata wafanyakazi wa taasisi binafsi. Tumepata orodha ndefu tunaifanyia kazi, tunawadai wengine wanatukubalia na wengine wajanja, wanatuambia kwamba hebu tuoneshe unayo *document* yoyote ya kuthibitisha kwamba unatudai.

Hawa tumewaonesha mkataba tuliofunga nao, mkataba wa wadhamini wao na *copy* ya *voucher* tuliyowapa pesa, wengine wanasalimu amri wanatulipa, wengine bado ni wagumu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tatizo zaidi la mkopo huu ni wale ambao tunazungumza nao sana ambao wamekopa, wamesoma na wamemaliza, wanakimbia hawarudi. Hawa tunajaribu kuwafuatilia kutokana na Balozi za nchi zao, lakini sitaki nithibitishe kwamba tunaweza kupata chochote. Lakini bado juhudi tunazichukua na *Inshaallah* tutafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kama niwezavyo kuyatolea ufafanuzi maelezo haya yaliyoelezwa. Sasa kwa wale ambao sikuwagusia sana nawaomba radhi sana, sijakusudia kwamba sikuwa na jibu la kuwapa, lakini mambo ni mengi na mengi tumeshayajibu, muda bado tunao wa kuulizana, kushauriana na wa kusemeshana. Ninaloliomba ni kwamba wizara yangu ni sikivu, tunasikiliza kila shauri tunalopokea na kujaribu kama iwezekanavyo kulitekeleza. Pale tuliposhindwa tunatoa jawabu, tutaendelea kufuata utaratibu huu huu. Suala la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni kubwa, ni nyeti na ni zito.

Mhe. Mwenyekiti, jukumu hili nikikaa nalo mwenyewe kulikumbatia tu, litanishinda. Lakini nikijua kwamba jukumu hili sio langu peke yangu, ni langu na wenzangu wote walioko katika Baraza hili, na kwa hivyo tutaendelea kushirikiana kulimaliza na kulitekeleza. Kazi yangu itaendelea kuwa rahisi, kuwa nzuri na kuwa naipenda.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kumshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu. Nina hakika Makamu Mwenyekiti, siku zote alikuwa yuko tayari kuhakikisha wizara hii inafanya vizuri. Siku zote Makamu Mwenyekiti katika mikutano yetu, mkutano wa ufunguzi na mkutano wa majumuisho, alikuwa akisema; tusiposhirikiana na Waziri, tusipomsaidia Waziri, waziri ana matatizo mengi na mengi ya msingi ni bajeti, waziri wetu ana majukumu makubwa, lakini bajeti yake haipati kwa ukamilifu. Anasisitiza sana msaada wa kunipa yeye na Wajumbe wake wa Kamati. Nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati walikuwa na moyo huo wa kunisaidia.

Mhe. Mwenyekiti, na wewe nakushukuru kwa kunivumilia, kwa kunisikiliza na nawashukuru Wajumbe wote kwa kunivumilia na kunisikiliza. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Hija Hassan Hija: (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa jioni hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na uhai, ili kuweza kutoa majumuisho ya michango ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenye ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kwa mwaka huu wa 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba Kamati yangu ilikuwa ikiwasikiliza kwa makini sana Waheshimiwa Mawaziri pale walipokuwa wakitoa majumuisho, ili na sisi tuweze kutoa mchango wa majumuisho, kwa vile ambavyo Kamati imeona na vile maelezo ya mawaziri yalivyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwatambue wale wote waliopata bahati ya kuchangia. Jumla ni Wajumbe 17 kama ifuatavyo:

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Asha Bakari Makame
3. Mhe. Nassor Salim Ali
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
6. Mhe. Saleh Nassor Juma
7. Mhe. Ashura Sharif Ali
8. Mhe. Mohammed Haji Khalid
9. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
10. Mhe. Salim Abdalla Hamad
11. Mhe. Ali Salum Haji
12. Mhe. Panya Ali Abdalla
13. Mhe. Rufai Said Rufai
14. Mhe. Hassan Hamad Omar
15. Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto
16. Mhe. Waziri wa Afya
17. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe waliochangia kwa jumla ni 17. Wajumbe wanawake ni 5, sawa na asilimia 29.4 na wanaume ni 12 ni sawa na asilimia 70.6. Kigezo cha asilimia 29.5 kinakwenda sambamba na ile asilimia ya wanawake wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, takwimu hii inashawishi Kamati yangu kwamba asilimia ya wanawake bado ibakie kuwa ni asilimia 30, kwa sababu ndio waliochangia.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niseme yale mambo ya utangulizi kwa jumla baada ya kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe kwamba tumekuwa na mashirikiano ya karibu sana na Waheshimiwa Mawaziri wote watatu kwenye Kamati yangu. Mawaziri wetu walikuwa wakiona kuwa tunawasaidia katika *level* ya mawaziri wote watatu walikuwa na upeo wa kuona kwamba lengo la Kamati ni kuwasaidia. Kama ni maksi basi ningesema wizara ambayo imetupa mashirikiano makubwa kwa mwaka huu wa fedha uliopita ni Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto chini ya Mhe. Zainab Mohamed ambapo Kamati yangu imesema kwamba tungewapa asilimia 98 ya mashirikiano. Kwa kweli kulikuwa hakuna dosari kila ambalo Kamati ililiomba kwao wao, walikuwa wakitupa kwa mujibu wa utaratibu na sheria za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara ya pili ambayo mashirikiano yalikuwa sio mabaya ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kamati imesema tungewapa asilimia 92 kwamba walikuwa na mashirikiano makubwa sana hasa Mhe. Waziri na Katibu Mkuu.

Wizara ya tatu ni Wizara ya Afya. Kamati imesema labda tungewapa asilimia 55. Ukiacha katika *level* ya mawaziri, kwa maana ya Waziri na Naibu Waziri. Kamati yangu ilikuwa ikipata tabu sana katika mashirikiano na watendaji wa Wizara ya Afya. Wapo ambao waliona kwamba labda Kamati inawasumbua, waliona labda Kamati inawabughudhi na hawakujua lengo la Kamati kwamba ni kuwasaidia kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, ningewashauri watendaji wa wizara hizi tatu, hasa wa Wizara ya Afya, wakatambua kwamba Baraza la Wawakilishi ndio muhimili wa usimamizi wa serikali na kwamba daima sisi tuna wajibu wa kutetea maslahi ya nchi kupitia fedha za walipa kodi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu mbali ya kuchangiwa na Wajumbe 17, lakini imepata hoja 46. Hoja 17 zimekwenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na hii ni sawa na asilimia 36.9. Hoja 21 zimekwenda Wizara ya Afya ni sawa na asilimia 45.7 na hoja 8 zimekwenda Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto sawa na asilimia 17.4.

Hoja hizo Mhe. Mwenyekiti, zinadhihirisha wazi kwamba Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ndio yenye hoja chache na ndio iliyo makini kwa kituo cha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Wizara ya pili yenye hoja chache ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yenye hoja 17, na hii inakwenda sambamba na ile takwimu yangu ya mwanzo kuwa, wizara ya pili kwa upande wa Kamati yangu ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Waheshimiwa Wajumbe wamehoji mara 17 na Wizara ya mwisho yenye hoja nyingi ni Wizara ya Afya yenye hoja 21, kila aliyenyanyuka hapa alikuwa haisahau Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, kipimo cha hoja hizi ni kwamba Wizara ya Afya ina tatizo ndani ya macho ya Kamati na ndani ya macho ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, sasa nianze kujibu hoja moja moja na nianze kwenye ile wizara ambayo imepata hoja chache sana, ambayo ni Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikimfuatilia kwa kina Mhe. Waziri, kimsingi yote aliyoyajibu ni sahihi na yameungwa mkono na Kamati yangu, hakuna aliloongeza wala alilopunguza na huu ndio umakini wa Mhe. Zainab Omar Mohammed, mama ambaye mimi nasema ni makini, ukimuona ni *iron lady* lakini bado akili yake ni makini sana.

Mhe. Mwenyekiti, yale yote ambayo ameyasema Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ni yale ambayo Kamati tulikubaliana. Tulivyomuelekeza ndivyo alivyotenda na pale penye mapungufu hasa ya kibajeti basi Mhe. Waziri alikuwa hasiti kusema kweli, kwamba hapa pana mapungufu ya kibajeti.

Lakini nimefurahi zaidi Mhe. Mwenyekiti, kwamba leo Mhe. Waziri amemthibitishia Mhe. Makame Mshimba kwamba jengo la *ZAYADESA* limepatiwa hati. Huu ndio uungwana, huu ndio umakini na huu ndio uwaziri ambao GNU wanautaka.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *One Stop Center*, Mhe. Waziri aliweka ahadi kwamba atafungua Pemba. Nikuthibitishie mbele ya Baraza hili kwamba Kamati yangu imeshuhudia kituo cha *One Stop Center* pale Chake Chake kinafanya kazi kama ambavyo kinafanya kazi cha hapa Unguja. Changamoto ziliopo Pemba ni sawa na ziliopo Unguja kwamba tumekosa mashine za DNA, tumekosa fedha za kuendesha vituo kwa ufanisi, lakini bidii za Waziri na watendaji wake

zimefanyika kwa umakini na Kamati yangu inampongeza kwa msimamo huo kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aliombwa na Wajumbe kwamba azingatie jumuia ya wanawake wajane na hakusita kusema kwamba na yeye ni mjane, kwa hivyo yuko makini sana. Kwa hivyo, yuko tayari kusimamia hili na mimi Kamati naunga mkono kwamba asimamie jumuia hii ya wanawake wajane.

Mhe. Mwenyekiti, suala la omba omba Mhe. Waziri pia amelizungumzia na Kamati inamuomba sana asimamie kwa kasi kubwa sera ya hifadhi ya wazee, ili iende sambamba na matakwa ya serikali ya kuwasaidia wazee wetu, tabia ya kuomba hadharani ni aibu na ni wajibu wa serikali kuwalinda wazee wetu. Mapinduzi ya Zanzibar yalikuwa na lengo la kuwanusuru watu wetu ili kuondokana na aibu ya hapa na pale.

Mhe. Mwenyekiti, suala la jumla kuhusu ufinyu wa bajeti kwenda kwenye wizara hii ni mkubwa. Lakini sifa moja ambayo wanayo wenzetu wa wizara hii ya ustawi wa jamii, wana umakini mkubwa wa matumizi yao, hakuna ubabaishaji, wakipata shilingi mia basi hutumia shilingi mia na wakipata shilingi elfu hutumia shilingi elfu. Kila mtu mwenye macho ya kawaida na hata yale macho ya kitaalamu basi anaona kwamba wizara hii hakuna ubabaishaji katika matumizi ya fedha. Mimi kwa niaba ya Kamati yangu tunawapongeza sana na wale ambao watabahatika kwenda kwenye Kamati hii baada ya uteuzi wa Spika, naomba wamsaidie sana Mhe. Waziri kwamba yeye ni mtu ambaye hana ubabaishaji kwenye matumizi, hasingizii kesi za meli kwamba tutanunua meli.

Kwa mfano, anasema nimepata shilingi mia na nimetumia shilingi mia au nimepata shilingi mia nimetumia tisini imebakia kumi. Hakuna masihara na hii ni dhahiri kwamba kwa sababu Waziri mwanamke, Katibu Mkuu mwanamke na muhasibu wake pia ni mwanamke. Wanawake katika mambo ya fedha ni waaminifu sana. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono na kwa kweli nampongeza sana Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, hoja ya msingi ya kwanza ni upungufu wa bajeti ya wizara, kamati inaunga mkono. Kama Mhe. Waziri alivyosema kwamba mara zote tumekuwa tukisema kwamba kama tunataka kuwekeza kwenye maendeleo ya nchi, basi tuwekeze kwenye masuala ya elimu na afya. Kwa bahati mbaya sana SMZ haijaelewa hilo. Tumekuwa tukizungumza elimu ni muhimu, lakini hatuwekezi kwa vitendo katika masuala ya fedha na upande wa afya na elimu kwamba twende katika utaratibu wa *millennium*.

Kwa mfano maazimio yale ya Abuja yanasema kwamba bajeti ya elimu isishuke kwa asilimia 20, lakini hivi leo sio zaidi ya asilimia 15. kwa hivyo, ni dhahiri kwamba serikali haijakubali kuwekeza katika suala zima la elimu nchini. Madhara yote hayo Mhe. Mwenyekiti yanayopatikana, pamoja na sababu nyengine mbali mbali, lakini zinatokana na uchache wa bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambapo kwa kweli kila wanavyopanga kunakuwa na ukwasi wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na upungufu huo ni lazima niwaambie, kwamba umakini wa matumizi ya fedha za umma ni lazima uwepo. Katika wizara ya elimu ofisi kuu Kamati yangu haina tatizo, lakini katika maeneo mbali mbali, likiwemo eneo la Mamlaka na mafunzo ya amali. Tulimwambia Waziri na leo tunasema hapa mbele ya Baraza kwamba kuna ubadhirifu wa fedha za umma, Kamati yangu haikuridhika katika matumizi ya fedha za umma katika ofisi ya mamlaka ya mafunzo ya amali na utaratibu wa kusubiri *PAC* sisi hatusubiri *PAC*, kwa sababu tumeona na tunasema na tunamuomba Mhe. Waziri achukue hatua.

Mhe. Mwenyekiti, tulimwambia Mhe. Waziri kwamba kuna haja ya kuchukua hatua katika Idara ya Fedha ya Mafunzo ya Amali, na hapa tunazungumza mbele ya Baraza hili tukufu, kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali katika Wizara yako kuna tatizo la ubadhirifu wa fedha, yaani matumizi ya fedha katika mamlaka ile ni ya ubabaishaji.

Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu Mhe. Waziri inakuomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba ukae makini katika hili, ili sura nzuri ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa upande wa fedha isiharibiwe na idara moja na hili ni jambo ambalo halipendezi.

Hoja nyengine iliyozungumzwa ni kuhusu matatizo ya ujenzi wa Skuli za Sekondari za Wilaya. Mhe. Mwenyekiti, tumemsikiliza Mhe. Waziri alipozungumza kwamba malengo ya serikali yalikuwa ni mazuri. Lakini nikiri kwamba Kamati inaamini kwamba ufanisi ni mdogo, kwa sababu tumemiliki malengo tu, lakini tumeshindwa kumiliki walimu, wanafunzi pamoja na vifaa vya kusomeshea katika skuli hizo.

Kwa hivyo, ni sawa na kumiliki koti na kofia na ukashindwa na kanzu ya kwenda kuolea bali sifa inakuwa ni ndogo. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kwamba Kamati yangu inaamini kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali utaratibu wake kukimbilia zaidi kwenye majenzi na kila kwenye mradi wa ujenzi basi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakuwa *very active*, lakini Mradi wa Ufanisi wa Elimu kidogo tunadharau. *(Makofi)*

Sasa hali hii wananchi wanaamini kwamba labda kwa sababu ujenzi unaweza kusababisha asilimia 10 kwa wahusika, jambo ambalo si zuri na wala Kamati yangu halikulifurahikia. Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kujenga skuli 16 na leo tukashindwa na ufanisi wa kusomesha wanafunzi wetu.

Vile vile kuhusu suala la ubovu wa mabanda ya Skuli ya Mwembeshauri na Lumumba, Mhe. Waziri ametolea ufafanuzi na bila ya shaka kuna dalili kwamba skuli hizi zitapatiwa mabati hivi karibuni, kama si leo kwa habari tulizozipata pengine itakuwa kesho. Kwa hivyo, nimpongeze Mhe. Waziri kwamba amesikiliza kilio cha Mhe. Nassor Salim Ali na skuli hizo zitapata ufadhili huo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni uwiano katika usahihishaji wa mitihani. Kimsingi Mhe. Mwenyekiti isijengwe picha kwamba labda Wawakilishi wanadai kwamba kuwe na uwiano baina ya Pemba na Unguja na wala sio hoja ya msingi kusema kweli.

Hoja ya msingi ukiangalia takwimu za sensa, kwamba mkoa wa mwanzo ambao unaoongoza kwa idadi ya watu ni Mkoa wa Mjini Magharibi, wa pili ni Mkoa wa Kaskazini Pemba, wa tatu

ni Mkoa wa Kusini Pemba, wa nne ni Mkoa wa Kaskazini Unguja na wa tano ni Mkoa wa Kusini Unguja. Kwa nini walimu hawa wengi watoke mjini na hiyo ndio hoja ya msingi, kwa nini tusipate uwiano wa Kusini Unguja, Kaskazini Unguja, Kusini Pemba na Kaskazini Pemba.

Kwa hivyo, sura iliyojengwa hapa si kwamba watu wanazungumza Unguja na Pemba, isipokuwa wanazungumzia uwiano uwakilishi wa mikoa, ili kuwaridhisha wale walimu na wanafunzi kwamba kweli mikoa yote imewakilishwa katika masuala ya kusahihisha, lakini wanaoshiriki ni watu wa mjini tu na Mhe. Mwenyekiti *mjini ni shule*.

Kwa mfano, upo uwezekano watu wa mjini wakajipendelea na hiyo ndio dhana ya watu kwa nini hatutoi uwakilishi katika mikoa yote ili kila mtu akaridhika kwamba walimu wangu walishiriki. Mhe. Mwenyekiti, hoja hapa sio Unguja na Pemba na mimi naamini hapa mjini wapemba ni wengi, lakini hoja ni uwakilishi wa mikoa katika masuala haya ya mitihani.

Jambo jengine ni kuhusu matatizo ya Skuli ya Ufundi Kengeja. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anikubalie kwamba skuli hizi za ufundi Zanzibar ni mbili tu; ni Skuli ya Ufundi Mikunguni na Skuli ya Ufundi Kengeja. Skuli ya Ufundi Mikunguni ina *departments* tano, yaani inasomesha *electrical*, *electronics*, *civil*, *chemistry* na *computer*, masomo hayo ndiyo yaliyokusudiwa kusomeshwa Skuli ya Ufundi Kengeja lakini jambo la ajabu Mhe. Mwenyekiti, kwamba Kengeja zinasomeshwa *departments* mbili tu ya *civil* na *electrical*. *(Makofi)*

Sasa kwa upande wa walimu Mhe. Mwenyekiti, Kengeja *departments* mbili hazina walimu, yaani zimekosa walimu kwa muda mrefu na walimu wanaosomesha sio waliokusudiwa kusomesha Skuli ya Ufundi Kengeja. Kwa nini Skuli ya Ufundi Kengeja wenye *departments* mbili ikose walimu, lakini Skuli ya Ufundi Mikunguni yenye *departments* tano ina ziada ya walimu. *(Makofi)*

Hii ni hoja ya msingi, kwamba ni dhahiri tunabagua baina ya skuli hizi mbili za ufundi na jambo hili Mhe. Mwenyekiti haliingii akilini kwamba skuli moja yenye *departments* tano walimu wamejaa, lakini hii nyengine yenye *departments* mbili walimu ni usumbufu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti hii ndio hoja ya msingi kwamba tuweke uwiano wa walimu katika skuli zetu za ufundi za Mikunguni na Kengeja.

Lakini jengine ambalo Skuli hii ya Ufundi Kengeja ni tatizo ni fedha za bajeti. Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu imesikitika sana kwamba Baraza hili limepitisha fedha tangu mwaka 2010 kwa ajili ya fedha kwenye Idara ya Umeme.

Mhe. Mwenyekiti, hadi Kamati yangu juzi inafika miaka mitatu nyuma fedha hizi hazijafika na ukiangalia Wizara ya Fedha, fedha hizi wameidhinisha Mhe. Mwenyekiti, lakini fedha zilikwama kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ndipo hoja inapokuja kwamba vipaumbele vya serikali kwenye Wizara ya Elimu vinazingatiwa labda kwa upendeleo au kwa vigezo ambavyo si vya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, natoa wito kwamba Mhe. Ali Juma Shamuhuna ni Waziri ambaye ninamuamini asimamie watendaji wake wagawe usawa katika idara zake mbali mbali Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, matokeo ya mtihani kuwa ma mjadala wa kitaifa. Kwa kweli hoja hii imetolewa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu na mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja na wala tusisubiri matokeo ya Tume ya Mhe. Mizengo Pinda (Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania), lakini ni vyema taifa likawa na mjadala wa kitaifa kwa nini wanafunzi wetu wakafeli. *(Makofi)*

Kwa nini nikasema hivyo, kwa sababu mazingira ya uchunguzi naamini yatakuwa tofauti baina ya Zanzibar na Bara, yaani sababu za matokeo mabovu ya Zanzibar ni tofauti sana na kule Bara. Kwa hivyo, kusubiri Tume ya Pinda Mhe. Waziri Kuu kuja na majibu ya uchunguzi itakuwa Zanzibar tumechelewa sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Mhe. Waziri aitishe mjadala wa kitaifa kwa ajili ya kujadili vipingamizi vilivyosababisha elimu yetu Zanzibar kushuka. Lakini nasema kwa mtazamo wa kawaida kama hatukuchukua hatua za haraka basi elimu itazidi kudidimia siku hadi siku hapa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mazingira ya usomeshaji katika skuli zetu ni mabovu. Kwa mfano, juzi hapa tumezungumza kuhusu masomo ya historia na Mhe. Waziri alikuwa akijibu hapa kwamba masomo ya historia yanasomeshwa mpaka madarasa ya chini. Lakini pengine mpango ndivyo ulivyo na tofauti na hali halisi na inawezekana watendaji wake hawampi ukweli katika masuala haya.

Kwa hivyo, nashauri Mhe. Mwenyekiti, kwamba hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba Wizara ya Elimu iitishe mjadala wa taifa juu ya kujadili suala zima la kuporomoka elimu kwa Zanzibar ni muhimu na Kamati inaunga mkono suala hili kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Matatizo ya Skuli ya Haile-Selassie na Jang'ombe na suala hili limezungumzwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Mhe. Mwenyekiti, kweli Kamati yangu ilifika Skuli ya Haile-Selassie na Jang'ombe na skuli ambayo ina wanafunzi zaidi ya 2000, inaendelea kushuka siku hadi siku kwenye viwango vya kupasisha.

Kamati ilipogundua Mhe. Mwenyekiti, iligundua kwamba skuli ile ina Kamati ya Skuli miaka 20 haijafanyiwa mabadiliko, kwa hiyo kamati ile kazi yake ni moja ni kuomba posho kwa ajili ya kufanya vikao, yaani Mwalimu Mkuu tupate posho, kazi ya pili Mwalimu Mkuu ambaye atakataa maelekezo ya kamati basi Mwalimu Mkuu huyo hafai na kamati tuliiambia pale kwamba kazi yenu kujisifu Mwalimu Mkuu tumemuamrisha a, b, c.

Kwa hivyo, tukaagiza Mhe. Mwenyekiti, kwamba Kamati hii ya Haile-Selassie iondoshwe mara moja na ichaguliwe nyengine kwa mujibu wa Kanuni za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. *(Makofi)*

Sambamba na hilo Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba pale kuna *open space,* yaani eneo lile ni la Skuli ya Haile-Selassie tukaomba kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kushirikiana na skuli kulitumia, kamati imegundua kwamba kuna wajanja wachache wanajitayarisha kulichukua eneo la Haile-Salassie kwa ajili ya kulitumia kwa maslahi yao.

Kutokana na hali hiyo, tuliagiza haraka sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba alishughulikie suala lile pamoja na Mwalimu Mkuu wa Skuli ya Haile-Selassie, ili wale wajanja wachache wanaolinyemelea kulichukua kwa ajili ya maslahi yao, basi waweze kugonga mwamba na akidharau suala hili mpaka bajeti likichukuliwa basi Kamati italia na Mhe. Waziri kwamba ndiye aliyesababisha eneo lile lichukuliwe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kuhusu Skuli ya Jang'ombe Kamati imesikitika na nimuombe sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba aende kule Jang'ombe akaangalie jaa liko chini ya dirisha la Mwalimu Mkuu, yaani jaa liko chini ya madirisha ya Skuli ya Jang'ombe na wanafunzi wanasoma na wala huwezi kukaa hata dakika tano usibane pua. *(Makofi)*

Sasa najiuliza hii Wizara ya Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Manispaa basi majaa yote hawayaoni mpaka pale Jang'ombe chini ya skuli. Kwa maana hiyo, naomba Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, akatembee na kuangalia na kama ni muungwana kweli kwa ajili ya afya za watu basi jaa lile liondoke mara moja katika Skuli ya Jang'ombe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia limezungumzwa suala la maslahi ya walimu na mimi naunga mkono kwamba walimu maslahi yao yaongezwe, kwa sababu walimu wengi Zanzibar wamepotea kwa sababu ya maslahi duni. Kwa mfano, wakati alipokuwepo Mhe. Haroun Ali Suleiman yeye alikuwa akitumia mbinu za kitaalamu na kuwadhibiti walimu wake, sasa labda ni jambo la kumuhoji alikuwa akifanya jambo gani, lakini leo walimu wengi wanaondoka hapa kwa sababu malipo wanayolipwa hapa ni madogo mno.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba tujenge hoja serikalini walimu wetu waongezewe maslahi, kwani bila ya maslahi ya walimu hakuna elimu Zanzibar.

Suala jengine ni kuhusu uvamizi wa Vyuo vya Kiislamu Unguja na Micheweni. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Kamati iligundua kwamba Chuo cha Kiislamu Unguja kimevamiwa na watu wamejenga miradi ya biashara na wengine wamejenga makaazi ya kawaida. Hali hii imetokana na ukosefu wa kuwepo na hati miliki.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kwamba ili kunusuru Chuo cha Kiislamu Unguja, basi ni kusimamia haraka sana hati mikili pamoja na kujenga uzio, ili wale wajanja wenye tamaa ya ardhi, maana wapo watu ardhi haiwatoshi, yaani wale wenye ujanja wa ardhi, basi tuwadhibiti wasije kukimaliza kile Chuo. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu suala la malipo ya walimu wa *TAP* Mhe, Waziri amezungumza. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba barua amepeleka Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Mwenyekiti, basi nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi ambaye ni Mtumbatu mwenzangu na ile barua aijibu haraka kwa ajili ya kuwapatia maslahi yao walimu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ambayo Mhe. Saleh Nassor Juma ni vilabu vya starehe kujengwa karibu na skuli. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Kamati imegundua kwamba Skuli ya Fidel Castro na Madungu, vimejengwa vilabu vya starehe ndani ya maeneo ya skuli, hivi ni nani aliyetoa kibali pale Madungu kujenga nyumba ya starehe.

Hivyo, tunakusudia sasa wanafunzi baada ya mapumziko wacheze mziki, kwa sababu eneo la serikali au Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini tumetoa kibali ndani ya maeneo ya skuli pamejengwa kilabu cha starehe. Sasa tunajiuliza labda tumebadilisha mtaala sasa baada ya kusoma tena jioni twende kwenye mziki, na hili si jambo zuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ningeomba kwa heshima kubwa kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, yule aliyejenga pale basi apatiwe fidia na halafu aondoke mara moja au labda mutwambie kwamba sasa baada ya kusoma usiku twende kwenye mziki itakuwa hakuna tatizo.

Jambo jengine ni kuhusu Chuo cha *SUZA Campus* ya Nkrumah kuhatarishwa na uvamizi wa maji. Mhe. Mwenyekiti, nadhani hili liangaliwe maji ya bahari yanakula eneo la chuo na kuna hatari chuo kile kuingiwa na maji wakati wowote.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu udhaifu wa mkandarasi kwenye ujenzi wa Skuli ya Paje Mtule, Dimani na Tunguu. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na lugha zote na tuwapambe na tufiche ukweli, lakini mkandarasi huyu ameshindwa kazi. Kamati imetembea zaidi ya mara mbili na amekwenda Mhe. Rais mara moja, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amekwenda mara moja na sote tumedanganywa.

Kwa hivyo, kwa kuwa upo mkataba wa makubaliano na wakati mwenzetu mkataba ameuvunja, basi sasa aondoke kwa maslahi ya taifa, kama itakuwa watu wanaridhika tafsiri ya Kamati itakuwa mkataba ule ni mbovu au si makini kwa upande wa serikali. Mhe. Mwenyekiti, Kamati hairidhishwi kwamba Rais, Makamu wa Pili, Waziri pamoja na Kamati pia idanganywe, lakini mkandarasi anatanua tena huyu ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakandarasi Tanzania.

Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri kuanzia sasa wakandarasi wa kupewa kipaumbele ni wale wazalendo wa nchi hii. Kwa mfano, tumeona ujenzi mzuri sana wa Kampuni ya *Quality Building* kule Pemba, pia tumeona ujenzi mzuri sana wa Kampuni ya *Rans* kule Pemba. Kwa hiyo, kwa nini tuwakwepe Wazanzibari wenye uwezo mkubwa na uchungu wa nchi hii na tuwapelekee wakandarasi *just* kwa kupendelea kitu fulani.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa ushauri wa Kamati mkandarasi huyu haraka sana aondoshwe na kama kuna fidia basi atulipe, ili serikali inusurike kula hasara katika jengo hili. Kwa kweli naamini kama serikali ndio ilifanya uzembe, basi serikali ingelipa, sasa kwa nini imuonee huruma mkandarasi ambaye anaitia serikali hasara.

Kwa maana hiyo, mama huyu aondoshwe na kama kuna fidia basi atulipe haraka sana na tabia ya kusema tusubiri Mwanasheria Mkuu atushauri kwa serikali hii ni miaka 40, na kama hivyo ndivyo basi naamini kama tutakula hasara. Mhe. Mwenyekiti, nasema kabisa ili niweke hakiba, kwa sababu kuna siku inaweza kutokezea, ili nije niwakumbushe kwamba nilisema. Mhe.

Mwenyekiti, mtindo huu wa kusema tusubiri kesho kwa tabia yetu ya Zanzibar itafika miaka 50 na huyu mama ataondoka na itakuwa kazi ya mcheza bao.

Suala jengine ni kuhusu ubovu wa Ofisi ya Baraza la Mitihani. Kamati imeshuhudia kwamba ofisi ile inatumiwa na wafanyakazi wetu wengi na jengo ni bovu, pia tulishauri kwamba wale watu wahamishwe kwa ajili ya kunusuru maisha ya watu wetu, hadi hii leo Mhe. Waziri bado hajafanya uhamisho huo. Kwa hivyo, Kamati inamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba afanye bidii sana ya kuwaondosha wale wafanyakazi wetu, ili kunusuru maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni kuhusu Bodi ya Mikopo na Mhe. Waziri nimesikiliza majibu yake lakini Kamati haikuridhika. Kwa kweli wanafunzi waliokopeshwa ni 1564, waliohitimu kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri ni 257 sawa na asilimia 16.4, ambao wamewachambua, maana yake hawawajui vyema ni watu 300, lakini tukisema wote tuwajue hao basi itakuwa ni watu 357 na asilimia 55.6.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imetoa zaidi ya bilioni 4, lakini bahati mbaya hatuwatambui nani tuliowapa, hii ni aibu kwamba tumetoa bilioni 4 kwa kuwapa Wazanzibari, lakini wazanzibari pamoja na serikali haiwatambui na inawatafuta. Hali hii mimi binafsi naamini kwamba fedha hizi zimepotezwa kinyume na utaratibu na wala haiwezekani Mhe. Mwenyekiti hata bila ya *computer* utumie karatasi tu, basi lazima tungewajua waliopewa mkopo huu, na serikali inajisifu kwamba hatuwatambui.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba hapa kuna dalili moja ambayo si nzuri, kwa hiyo namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba hii lugha kwamba hamuwatambui, basi mkafika pahala mukaturidhisha hamuwatambui au mumewasahau.

Mhe. Mwenyekiti, anatuambia Mhe. Waziri kwamba fedha iliyolipwa ni shilingi milioni 78 na hii ni sawa na asilimia 1.95, kwamba fedha za umma miaka 7 nyuma zimelipwa asilimia 1.95 na tumeridhika hatuna wasi wasi na huu ni mtihani mkubwa kwamba bilioni 4 zimekwenda na SMZ imelipwa milioni 78 tumeridhika kidogo kidogo mwendo wa kinyonga. *(Makofi)*

Kwa kweli nadhani ni vyema tuwe makini sana na mimi binafsi imani yangu ni kwamba hapa kuna mchezo mbaya ambao umechezwa, na kama haupo mchezo mbaya uliochezwa basi tuletee orodha ya wale waliopewa, na kama hapana orodha maana yake hamuwajui na ikiwa hamuwajui basi fedha zilitafunwa na hiyo ndio tafsiri yake. Sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba atusaidie maelezo, ili bajeti ikifika tupate ufafanuzi. *(Makofi)*

Jengine ni kuhusu ajira za walimu wawe na kipaumbele. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii inarejea pale kwenye takwimu kwamba tungetegemea sisi na serikali hii imesema humu ndani kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi una idadi ya walimu wengi ambao hawahitajiki na upungufu upo Pemba, Unguja Kaskazini na Kusini Unguja, sasa kwa nini walimu bado wapelekwe Unguja Mjini.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani Wizara izingatie pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, azingatie maeneo yenye upungufu wa walimu hasa Kusini Unguja na Kaskazini Unguja.

Sasa naomba nimalizie hoja moja kubwa ambayo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alizungumza, lakini kwa bahati mbaya Mhe. Waziri aliisahau au hakuitaja. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Mjumbe alizungumza hoja ambayo mimi binafsi inanifurahisha kwamba aliwataja wale wote waliochukua ardhi maeneo ya Kiwengwa, maeneo ambayo wanajimbo la Kitope walitenga kujenga skuli yao kwa ajili ya wananchi wa Kitope. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, haya ndio ambayo sisi tuliyazungumza na niliwahi kusema hapa kwamba kuna siku nitawataja, lakini Mhe. Mwakilishi amenitangulia na ninampongeza sana. Marekani walimpa Tunzo Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwamba ni Mwanamke Jasiri mwaka huu na mimi nampa Tunzo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba ni Mwanamme Jasiri mwaka huu, kwa kuamua kuwataja wale wote waliochukua ardhi ya serikali ndani ya nchi hii ni jasiri na mimi nitamkopi mwakani nitawataja wengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, watu wanachukua ardhi ya wananchi na halafu viongozi wanasema waliochukua ardhi wayamalize, yatamalizika wapi. Mhe. Rais anasema kila siku kwamba kila aliyechukua ardhi amalize mwenyewe aka! Kama ardhi amechukua Mshimba atamaliza vipi Mshimba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, natoa wito kwa niaba ya Kamati kama serikali iko makini basi kila aliyechukua ardhi ile arejeshe serikalini haraka kwa maslahi ya wananchi wa Kitope. Kwa mfano, baadhi ya wale aliowataja Mhe. Mjumbe hapa, basi wale wale wanazo ardhi Mwambe, Micheweni na hii ni aibu. Mhe. Mwenyekiti, ardhi ni mali ya serikali na hutolewa zaidi kwa maslahi ya umma sio kwa maslahi ya mtu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu inashauri kwamba wale waliochukua ardhi Kiwengwa kwa maslahi yao binafsi warejeshe haraka sana, vyenginevyo tuambiwe kwamba haki ile ya Mapinduzi ni kwamba ardhi ni mali ya serikali na maslahi ya umma basi imefutwa. Lakini inasikitisha kwamba wale ambao wametajwa hapa Unguja Kiwengwa ni wale wale wako Mwambe. Sasa ukichunguza basi utagundua wapo nchi nzima hii, Mhe. Mwenyekiti ni aibu na kwa kweli hali hii haiwezi kuvumilika.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hoja yangu kwenye Wizara ya Afya na ninaomba Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wanistahamilie, kwa sababu nina tabia ya kusema uwazi na wala sina tabia ya kuficha na huo ndio udhaifu wangu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli bajeti ya Wizara ya Afya ni ndogo, wamepata asilimia 56 kwa kazi za kawaida na asilimia 15 kazi za maendeleo. Lakini pamoja na udogo huu Mhe. Mwenyekiti Wizara ya Afya hakuna uwazi wa matumizi ya fedha za umma na Kamati imekuwa ikipata tabu sana unaomba *document* basi unatiwa kusini, kaskazini, magharibi na mashariki. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba ufanisi mzuri ni uwazi. Sasa iweje Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuwe na uwazi lakini wizara nyengine hakuna uwazi ni aibu. Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu haikuridhika kabisa na hali ya matumizi ya fedha Wizara ya Afya, yaani Idara ya Fedha ya Wizara ya Afya ina tatizo lazima Waheshimiwa Wajumbe tuseme wazi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, fedha zote za miradi Wizara ya Afya hakuna uwazi Kamati inadai siku tatu mpaka nne hakuna majibu, sasa kama wewe unayo nia safi na wala huna tatizo kwa nini ufiche *document* ya serikali. Kwa hiyo, Kamati inasisitiza kwamba matumizi ya fedha za umma Wizara ya Afya hakuna uwazi na wala sisemi kuna wizi, isipokuwa hakuna uwazi. Kwa maana hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba awe makini sana katika suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, upungufu wa dawa katika hospitali mbali mbali. Wakati Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema kwamba upungufu umeondoka. Lakini naomba nimueleze Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kuwa haya yote ambayo tumeyasema hayakutoka mdomoni mwangu wala mdomoni mwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu au Mhe. Mbarouk Wadi Mussa ama Mwakilishi mwengine. *(Makofi)*

Kwa kweli haya tumeambiwa na watendaji wa Wizara ya Afya na hayo ndio maana tukaandika, tofauti yetu ni kwamba tulikuwa hatuna chombo cha kurikodia tu, lakini maafisa wa Wizara ya Afya ndio waliotuambia kwamba upo upungufu wa dawa. *(Makofi)*

Sasa leo ukituambia kwamba upungufu wa dawa umeondoka basi itakuwa dawa zimekuja jana au leo, lakini maafisa wa Wizara ya Afya ndio waliotuambia kwamba upo upungufu wa dawa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya Kamati kugundua sasa baada ya kauli hiyo, basi tukaenda Bohari Kuu, Mhe. Mwenyekiti Mkurugenzi wa Bohari Kuu alituthibitishia kwamba upungufu wa dawa umeondoka, isipokuwa dawa za makali ya UKIMWI kwa sababu ya ongezeko la watumiaji hasa kutoka Tanzania Bara.

Kwa hivyo, Kamati ilipochunguza ikagundua kuna mgongano ndani ya Wizara ya Afya, kwamba wapo maafisa wanakusudia kumfelisha yule mama na Mhe. Mwenyekiti mimi ni muwazi sana na wala siwezi kuficha, watu *wanagombania ndizi wala mgomba si wao*. Kwa kweli mama yule anafanya kazi kwa ufanisi, lakini kuna watu wanataka cheo kwa nini uwe Bohari Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, dawa za makali ya UKIMWI ndio pungufu, lakini dawa zote zipo na Hospitali ya Mnazi Mmoja wanatuambia kuwa upungufu wa dawa upo kama si kuua kusudi tusemeje. Mwakilishi anatuua kusudi na hiyo ndio tafsiri yake hiyo, kwa sababu Bohari Kuu tunaambiwa dawa zipo na Mfamasia Hospitali ya Mnazi Mmoja anatuambia hakuna, maana yake ni kuua kusudi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni kazi yako kama utawalea watu wako ni sawa na sisi wajibu wetu kusema na kazi yetu itakuwa imekwisha.

Jambo jengine ni kuhusu upotevu wa kumbukumbu za wagonjwa ambalo amezungumza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwamba kuna upungufu wa *documents* za wagonjwa mbali mbali katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Mwenyekiti, suala hili Mhe. Waziri hata akatae ni kweli kwamba upo upungufu wa upotevu wa *documents* za wagonjwa, kwa nini zinyeshewe mvua kuna mchwa wamezila zimepotea wapi sijui, lakini upungufu Kamati imegundua kwamba upo upotevu wa *documents* za wagonjwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna suala zima la tatizo la ubovu wa vifaa. Mhe. Mwenyekiti, Kamati iligundua kweli kwamba kuna mashine tatu za *Ultra Sound* na *X-Ray machines* ni mbovu na mashine aliyosema Mhe. Mjumbe ya kupimia kensa ni mbovu, vile vile *lift* iliyotumia mamilioni ya fedha ni mbovu pamoja na *incinerator*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu kupitia kwangu nakataa katakata kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja haina *incinerator* na Kamati imekwenda chini ya bahari yaani taka zinachomwa ndani ya maji ya bahari. Kwa hivyo, kama ameambiwa ipo basi labda iwe imefika jana au juzi, lakini Kamati yangu mbele ya macho 20 yote tumeshuhudia plasta pamoja na taka nyengine mbali mbali za hospitali zinachomwa chini ya ufukwe wa Bahari ya Hindi.

Kutokana na hiyo, Kamati inaamini kwamba Wizara ya Afya haina chombo cha kuchomea taka labda kiwe kimekuja kuanzia jana, leo au juzi Mhe. Mwenyekiti huo ndio ukweli na lazima litengenezwe suala hili kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, posho maalum kwa wauguzi na *orderly*. Kamati yangu inashauri kwamba bajeti ya mwaka huu 2013/2014 basi izingatie posho la wauguzi kwa wafanyakazi wote wa Unguja na Pemba. Hoja kwamba haitwi kwenye *call* sio ya msingi, kwa sababu wale watu wanakaa hospitali kutoka asubuhi pengine mpaka usiku, kwa nini tusiwafanyie posho maalum kwa ajili ya kuwasaidia. Kwa hivyo, nadhani tusiwanyonge watu kwa hoja ambayo si ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni tatizo la mwananchi aliyefariki Rahaleo. Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati yangu tumepokea kwa masikitiko kifo cha mama Safia Francis baada ya tukio hilo ambalo lilitokana na matibabu yasiyo rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kifo hicho Kamati yangu inashauri kwamba ikachunguze na wala hatuwezi kuwaachia Wizara ya Afya peke yao, na kama walikuwa na nia nzuri wangetangaza kabla ya leo, lakini kama si Mhe. Nassor Salim Ali basi taarifa hii isingepatikana. *(Makofi)*

Lakini kifo hichi cha huyu mama kilichotokezea ni uzembe wa makusudi na Kamati yangu Mhe. Mwenyekiti inataka kufuatilia suala hili, basi nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba akubali tukalichunguze suala hili na watafutwe wataalamu wa afya na tuwemo angalau Wajumbe wawili wa Kamati tukathibitishe kwa nini mama alifariki kwa uzembe gani, ili tuweze kuwasaidia Wazanzibari.

Hoja ya kwamba watu wasitafute njia nyengine tutafanya baadae lakini hii iliyotokezea lazima tuigange. Kwanza tushughulikie suala hili ikiwezekana majibu ya kina tuyapate kwa Wazanzibari ili tuweze kupata ukweli wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, wizi wa milango Ofisi ya Mkemia Mkuu Maruhubi hili limezungumzwa, na Mhe. Waziri umekiri kwamba kuna wizi lakini Kamati inasikitika kwamba Polisi wamechunguza ni kweli mtu mwenyewe amekiri kwamba ameiba ni kweli, sasa tunasubiri nini. Nina hakika Wizara ya Afya mnamjua, nina hakika Polisi wanamjua na Kamati hii inamjua. Polisi kazi imemaliza zamani, mimi nimekwenda Polisi nimefuatilia mtu anajulikana tatizo nini? Basi Mhe. Mwenyekiti, tumlinde tu tumsamehe iwe basi lakini tusisingizie kwamba kuna uchunguzi, uchunguzi umekamilika zamani.

Mhe. Mwenyekiti deni la umeme katika vituo vya afya na maji hili Mhe. Waziri umezungumza ni kweli bajeti inayotengwa ya 20,000/- ni ndogo vituo vile vinatumia zaidi ya 80,000/- kama Mhe. Jussa alivyosema kwamba hiyo 80,000/- yenyewe ni ndogo, kuna haja ya kuongezwa fedha katika masuala haya. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba ajenge hoja kwenye bajeti ya Wizara mwaka huu kwamba kuna haja ya kupatiwa vituo hivi fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza huduma za afya vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni Kidongo Chekundu *hospital*, kamati imeeleza kwamba kuna tatizo na nikwambie Mhe. Waziri ni kweli kuna tatizo, mlo unaopatikana kule si wa uhakika na dawa si za uhakika, tatizo nini ni kwa sababu kuna changamoto ya fedha. Mhe. Mwenyekiti, haya ni maeneo ambayo Mhe. Waziri lazima ajenge hoja serikalini tuweze kupata fedha za kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, safari za wagonjwa nje ya nchi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amesema kwamba hana taarifa vizuri, lakini kama kawaida ya Kamati yangu nimenasa barua tatu hizi kutoka Ubalozi wa India. Mhe. Mwenyekiti, na hapa niwambie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba inaelekea pana tatizo, kuna watu waliokuwa hawana nia safi ugonjwa ni *deal*, kuna watu wengine wanaumwa wengine ndio mtaji wao kuumwa. Kuna barua tatu ambazo zimetoka Ubalozi wa India kwamba Wizara ya Afya Zanzibar hakuna uwazi, mnapeleka wagonjwa kimya mpaka mtu afariki ndio mna-*react*. Mhe. Mwenyekiti si maneno yangu ni maneno ya balozi wa India nchini Tanzania barua hizi hapa tatu, amempelekea Katibu Mkuu Wizara ya Afya mara tatu hajamjibu anamuomba nisaidie Katibu, kama shida ni ya Balozi shida ni yetu Mhe. Mwenyekiti lakini hakuna majibu kimya, kwa nini watu wanaficha mambo yao.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kama barua hana nitampatia barua tatu hizi hapa ambazo Balozi wa India anakunyenyekea wewe umsaidie maelezo kwa maslahi yako unashindwa kumpa maelezo, mpaka mwisho akakwambia kama hutaki basi ameshindwa ananyamaza kimya. Na taarifa ambazo tumezinasa kwenye Kamati yetu baada ya tishio hili sasa mnatafuta jengine kubadilisha kupeleka matibabu. Maana yake kila kitu mradi, kila kitu *deal*. Mhe. Mwenyekiti si jambo zuri Mhe. Waziri lazima ulifuatilie tupate ufafanuzi wa kina.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni ubovu wa jengo la Kitengo cha macho. Nimeona maelezo ya Mhe. Waziri amenileta pale kwenye mtandao, lakini nasema kwamba haya yametokana na midomo ya watendaji wako. Kamati yangu imeambiwa mbele ya Mkurugenzi wa Mnazimmoja kwamba mmetengewa milioni mia moja thalathini lakini mmelipa milioni 25 na jengo ni bovu, ada zote zimelipwa milioni 130. Kamati yangu inaangalia thamani jengo ni bovu mmewezaje fedha za umma milioni 130 lakini jengo ni bovu. Kwa hivyo kuna hali mbili Mhe. Mwenyekiti, kuna hali je fedha imefika na kama imefika kwa nini jengo ni bovu. Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri lazima afuatilie kwa kina tupate ufafanuzi katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, gari ya kubebea wagonjwa Wete/Mkoani Mhe. Hussein Makungu amezungumza majengo tangu mwaka 1990, magari mabovu tangu mwaka 1990 na lazima ufanye kazi ya kurekebisha udhaifu huo.

Mhe. Mwenyekiti jengine ni DNA *machine*, ninashukuru sana Mhe. Waziri amekiri kwamba hakuna DNA *machine*. Naomba kuchukua nafasi hii kuwaambia Wazanzibari kwamba Zanzibar

hatuna DNA *machine*, tuna DNA *associating machine* ambayo ni sehemu ndogo sana ya DNA *machine*. Kwa hivyo ni wajibu wa serikali sasa kutenga fedha kwa ajili ya kutafuta kifaa hicho kwa maslahi ya Wazanzibari hasa katika kesi za ubakaji. Ili Waziri wa Ustawi wa Jamii afanikiwe kwenye kesi hizi basi umpatie mashine ya DNA ili aweze kutatua matatizo haya.
Mhe. Mwenyekiti huduma za kujifungua waja wazito. Mhe. Mwenyekiti, napingana kabisa na maelezo ya Waziri. Kamati imetembea maeneo mengi, imekwenda Kivunge, imekwenda Mnazi Mmoja na hata Pemba mama wajawazito hawajifungui bila ya kutoa mchango. Kinyume kabisa na maelezo ya Mhe. Rais aliyoyatoa hapa Zanzibar. Sasa Kamati yangu inashangaa sana nimefuatilia mimi hapa Zanzibar, Spika wetu hapa ni Spika, kiasi miaka 20 hajawahi kutoa agizo kwa Wawakilishi na Watendaji wake likapuuzwa, lakini Mhe. Rais anatoa linapuuzwa.

Mhe. Mwenyekiti narejea kusema kwamba matibabu ya wajawazito kwa uzazi sio bure watu wanachangia, hujifungui mpaka uweke fedha ya watu mkononi mwanzo, kwa hivyo kama Rais amedanganywa sawa. Lakini Kamati imekwenda imeona na hakuna bure katika masuala ya uzazi kwa waja wazito. Mhe. Mwenyekiti, suala hili ningemuomba Mhe. Rais alichukulie kipaumbele kwa sababu yeye ni Waziri wa Fedha kama hoja ni Fedha basi yeye ndiye Waziri wa Fedha, la kama hoja ni ubadhirifu tu wa Wizara yenyewe basi tuambiwe. Lakini hatuwezi kutoa kauli za viongozi wakubwa halafu ikiwa hakuna utekelezaji. Mhe. Mwenyekiti, wanawake wanajifungua si bure ni kwa pesa mkononi.

Mhe. Mwenyekiti pesa za miradi ya maendeleo Pemba ni tatizo. Mhe. Mwenyekiti ni kweli tumeenda Pemba fedha za miradi ya maendeleo Pemba ni tatizo inawezekana kabisa Mwenyekiti ni udhaifu wenyewe wa Pemba, lakini inawezekana pia ni udhaifu wa Wizara nzima ya Afya. Kwa hivyo Kamati yangu inaomba suala hili Mhe. Waziri alifuatilie ili tuweze kupata ufafanuzi wa kina.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni tatizo la usafiri wa madaktari zamu za usiku. Mhe. Mwenyekiti Mnazi mmoja kuna matatizo. Madaktari wetu wanaoingia zamu za usiku hasa wanawake, wanapoondoka kazini muda saa sita usiku au saa saba, hulazimika kwenda kituo cha daladala Darajani kupanda gari jambo hili Mhe. Mwenyekiti, ni hatari kwa wafanyakazi wetu wa Afya. Kamati inashauri na inaomba sana bajeti ya mara hii lazima Wizara itenge fedha za kununua basi ili madaktari wetu wasafirishwe kutoka Mnazi mmoja hadi angalau kituo cha daladala ili tuwanusuru na wabakaji madhara mengine.

Mhe. Mwenyekiti, huu ndio wasia wangu kwa Waziri ili aweze kuufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inashangaa, inashangaa kwa sababu Mhe. Rais amekuja na utaratibu mpya, kila *quarter* ya mwaka Mhe. Rais anawaita watendaji wake kufanya mapitio ya bajeti zetu maarufu kwa bango kitita. Na kila Wizara inakwenda mara nne kwa mwaka. Wizara 16 maana yake inakwenda mara 64 kwa mwaka. Miaka miwili na nusu maana yake ni mara 160 tumekwenda kwa Rais. Suala kwa nini hatubadiliki. Kama Rais ameonana na Wizara zake mara 160 kwa miaka miwili na nusu na bado hali ni hii *business as usual* kwa nini hatubadiliki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeshauri kwamba tujipime, Mhe. Mgeni juzi alisema kwamba mwanadamu aliye kamili lazima ajitathmini mwenyewe ana mapungufu gani, lakini Kamati inatembea kwa mwaka mara 4 kila Kamati, Kamati 7 mara 28, miaka miwili na nusu mara 70 hizi ni fedha za serikali. Bango kitita 160 ni fedha za serikali lakini mambo yanazidi kuwa mabaya.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba kama si kosa uwaruhusu Wajumbe wako wajiulize pale walipo sisi ni wazima? Kama si kosa Mhe. Mwenyekiti, basi ungewaruhusu Wajumbe wako hapo walipo peke yake peke yake kila mtu ajiulize mimi ni mzima au ninaumwa?

Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo naomba kuwasilisha.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuiwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe pamoja na maelezo ya Katibu lakini tukiangalia muda hauturuhusu. Kwa hivyo basi naomba kuchukua nafasi hii kabla ya kuakhirisha Baraza kwanza nitoe tangazo.

Mhe. Mnadhimu wa Chama cha Wananchi CUF anawatangazia Wajumbe wote wa CUF wa Baraza la Wawakilishi waliomo humu, mara tutakapoakhirisha Baraza hili wao wabakie wana masuala muhimu wanatakiwa kujadiliana.

(Saa 1:40 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 17/04/2013 Saa 3.00 asubuhi)